

# MFUMO WA WILAYA

نظام الولاية

**Mwandishi:**

Ustadh Sayed Jawad Naqvi

**Mtarjumi:**

Dk. M. S. Kanju

**Kimehaririwa na:**

Ramadhani Salehe Kanju Shemahimbo

**Kimehakikiwa na:**

AlHaj Hemedi Lubumba Selemani

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ  
هُوَ الَّذِي بَعَثَ فِي الْأُمَّةِ رَسُولًا مِّنْهُمْ  
يَتَلَوُ عَلَيْهِمْ آيَاتِهِ وَيُزَكِّيهِمْ وَيُعَلِّمُهُمْ  
الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَإِنْ كَانُوا مِنْ قَبْلٍ  
لِفِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿١﴾

ترجمة

نظام الولاية

تأليف  
السيد الجواد نقوي

من اللغة الإنجليزية إلى اللغة السواحلية

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**  
AL-ITRAH FOUNDATION

**ISBN:** 978 - 9987 -17 - 047 - 0

**Mwandishi:**  
Ustadh Sayed Jawad Naqvi

**Mtarjumi:**  
Dk. M. S. Kanju

**Kimehaririwa na:**  
Ramadhani Salehe Kanju Shemahimbo

**Kimehakikiwa na:**  
AlHaj Hemedi Lubumba Selemani

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**  
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Julai, 2014  
**Nakala:** 1000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**  
**Alitrrah Foundation**  
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania  
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555  
**Barua Pepe:** alitrrah@yahoo.com  
**Tovuti:** www.ibn-tv-com  
**Katika mtandao:** www.alitrrah.info

---

---

# **YALIYOMO**

---

Neno la Mchapishaji .....	1
Utangulizi.....	3

<b>MLANGO WA KWANZA.....</b>	<b>5</b>
------------------------------	----------

<b>MFUMO WA WILAYA KWA MTAZAMO WA QUR'AN.....</b>	<b>5</b>
---	----------

Mwongozo na Lengo la Uumbaji .....	6
Mfumo – Njia ya Kufikia Ukamilifu .....	9
Qur’ani Tukufu – Silabasi ya maisha.....	12
Mfumo uliowasilishwa na Qur’ani Tukufu.....	13
Dhana potofu kuhusu Mfumo wa Wilaya .....	14
Ushia – Jina na Sura ya Uislamu, sio Madhehebu.....	15
Mageuzi ya Wilaya kutoka kwenye Mfumo kwenda kwenye midahalo.....	16
Uimamu (Uimamu) – ni Mfumo sio imani tu.....	17
Wilaya kama mfumo katika Qur’ani Tukufu .....	21
Tukio la Ghadir .....	24
Wilaya – ni Moyo wa Dini.....	25
Tangazo la Wilaya (Uongozi) .....	31
Wilaya – kukatisha tamaa juu ya maadui.....	35
Ni nini iliyokuwa hofu ya Mtume (saww)? .....	44

Wilaya – iligeuka kuwa sifa.....	49
Ummah wajitenga mbali na Wilaya kama Mfumo .....	51
Wilaya ya ambaye sio Ma’asum .....	53
Vita vya kisaikolojia juu ya Wilaya .....	61
Wilaya – suala lenye mwelekeo wa ubishani.....	63
Maono ya Allama Iqbal juu ya Wilaya .....	64
Baraza la ushauri la Shetani.....	66

**MLANGO WA PILI..... 79**

<b>IMAM KHOMEINI NA MFUMO WA WILAYA .....</b>	<b>79</b>
Imam – Moyo wa Umma .....	79
Imam Khomeini - ukweli ulio hai.....	80
Mafanikio makubwa ya Imam Khomeini .....	89

**MLANGO WA TATU .....** 99

<b>ATHARI YA MIFUMO YA UTAWALAISIYO YA KI-MUNGU JUU YA JAMII .....</b>	<b>99</b>
Mfumo wa Kiislam na Mifumo mingineyo ya Kijamii .....	99
Maagizo ya Waliu al-Faqiih na Kumfuta Marja mwingine.....	101
Qur an tukufu- chanzo cha uongozi.....	101

Wana wa Israili na Mfumo wa Firaun.....	104
Uhusiano wa Kihenga Haukuhakikishii Ulinzi.....	107
Du'a ya Arafah na Mfumo wa Wilaya .....	109
Sifa ya Kwanza ya Mfumo wa Kifirauni .....	113
Sifa ya Pili ya Mfumo wa Kifiraun .....	115
Musa (a.s.) – Mwokozi Dhidi ya Mfumo wa Firauni .....	117
Kwa nini Tujishughulishe na Mfumo Tawala Wetu? .....	118
Wanawake na Matukio ya Kisasa .....	119
Udikteta Chini ya Kivuli cha Demokrasia .....	121
Athari za Mfumo wa Kifirauni.....	121
Saamiri na Sanamu lake la Ndama .....	124
Musa na Haruni (a.s.).....	126
Wajibu wa Msingi wa Wanawake Wakati wa Ghaibu .....	128
Tatizo Kubwa la Umma Unaowasadidia Ma-saamiri .....	129
Wilaya – Mfumo Halisi na wa Kweli wa Utawala .....	130
Uimam kwa Mtazamo wa Allama Iqbal .....	133
Wajibu wa Wanawake Kwenye Mfumo wa Wilaya.....	134

**MLANGO WA NNE ..... 136**

**KUUHIFADHI MFUMO WA WILAYA ..... 136**

Kutoka Nje ya Njia Sahihi ya Dini .....	136
Jitihada za Kuung'oa Mfumo wa Wilaya Katika Zama Zetu .....	145
Uvamizi wa Tasnia ya Habari Kwenye Utamaduni .....	146
Kutanguliza dunia (Materialism) .....	146
Vyama vya Siasa na Watu .....	147
Magazeti Pinzani na Mfumo .....	148
Mahdawiyat (ufuasi wa Mahdi a.s.).....	149
Sufiya: .....	151
Anjuman al-Hujjatiyah.....	151
Utawa bandia .....	154
Mwenendo mbaya katika Maombolezo .....	154
Mahdi wengi wa bandia: .....	155
Kuuhifadhi Mfumo wa Wilaya: .....	157
Mamtuura – Jahili mchafu .....	159
Utaratibu wa Imam Haadi (a.s.) wa kuhifadhi Wilaya.....	164
Mfumo wa wilaya – Mfumowa uimamu na ummah.....	167
Maswali na majibu.....	173

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

---

## NENO LA MCHAPISHAJI

---

**K**itabu ulichonacho mikononi mwako ni tarjuma ya Kiswahili ya kitabu cha Kiingereza kiitwacho, *The System of Wilaya*. Sisi tumekiita, *Mfumo wa Wilaya*.

*Wilayah* maana yake ni uongozi, usimamizi, utawala au uendeshaji wa jambo au kitu. Maana mojawapo kati ya istilahi hii, *Kiislamu wilayah*, ni mfumo wa uongozi baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Na msingi wake ni kuanzia tukio la Karamu ya Ndugu (*aqrabaa*) mpaka tukio la Ghadir Khumm.

Katika kitabu hiki, mwandishi anatuelezea kwa ufasaha kabisa kuhusu suala la *wilayah* kwa kuzingatia aya za Qur’ani na hadithi ambazo zinazungumzia suala hili na maana yake.

Sisi tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya kielimu ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi katika akili za watu.

Kutokana na ukweli huu, taasisi yetu ya Al-Itra imeamua kuchapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Dkt. M. S. Kanju kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kukitarjumi kitabu hiki kutoka lugha ya Kiingereza, pia na wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera – Amin.

**Mchapishaji  
Al-Itrah Foundation**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

## UTANGULIZI

**P**amoja na sifa zote na shukurani kwa Allah Azza wa Jallah, Kituo cha Utafiti cha Kiislamu cha Bethat kina furaha ya kuwasilisha chapisho la tano la Kiingereza (na sasa kwa Kiswahili) juu ya kazi za Ustadh Syed Jawad Naqvi. Kitabu hiki kilichoko mikononi mwako ni utangulizi wa ufanuzi wa tukio la Ghadir Khum uliowasilishwa katika Qur’ani Tukufu. Kitabu hiki ambacho ni tarjuma ya hotuba ya semina iliyowasilishwa na Mwandishi kwa lugha ya Urdu, kina-wasilisha mtazamo wa Qur’ani juu ya suala la ‘Wilaya.’ Suala hili ambalo kwa ujumla hueleweka vibaya kwa watu wengi mionganini mwa wafuasi wa ‘Wilaya’ kama suala la imani tu, uonyeshaji wa mapenzi na shukurani. Inathibitishwa katika kitabu hiki kwamba ‘Wilaya’ ni mhimili wa dini ambao kwa kweli ni mfumo wa utawala ambao unahitaji utekelezaji katika jamii. Kwa ufasaha Mwandishi huyu anawasilisha fikra fulani zinazolezea mbinu za maadui wa Uislamu zilizotumiwa kugeuza na kupotosha ‘Wilaya’ kutoka kwenye ukweli wa maudhui yake halisi. Mbinu hizi zilifuatwa wakati wa tukio la Ghadir na vilevile hutumika hata leo. Kitabu hiki kime-lenga kufafanua baadhi ya mashaka ya kawaida na mitafaruku iliyoingizwa katika akili za kizazi chetu kichanga kuhusiana na suala la ‘Wilaya’ na hususan utawala wa Kiislamu na “Wilayatul-Faqih.”

Kwa mara nyingine tena moyo wa mwandishi huyu unatoa maoni ya hisia za moyoni yahusianayo na watetezi wa kihistoria wa “Wilaya” anaamsha nafsi ya ndani ya msomaji kwa kiasi cha ku-ziamsha kutoka kwenye usingizi mzito wa kutojali na kutofahamu

*Wilaya* kama mfumo wa utawala. Mwandishi ametoa uthibitisho wa kutosha pamoja na mbinu za kitaalamu za kuwasilisha ambapo kita-  
bu kinaishia na hitimisho kwamba katika zama za sasa wale ambao  
hawaungi mkono, hawahubiri au wanataka kukaa bila kuhusika na  
“*Wilaya*” kama mfumo wa utawala na hususan “*Wilayatul-Faqih*”  
kwa hakika ni zana katika mikono ya maadui, na kwa namna ny-  
ingine (bila kujijua) wanasaidia mwenendo wa maadui. Nini zaidi  
kitegemewe wakati mwandishi ambaye ni mahiri katika kutarjumi  
fikra za Allamah Iqbal, anawasilisha mashairi ya Allama Iqbal, ili  
kuthibitisha hoja yake kimantiki.

Insha Allah kitabu hiki kitakuwa kifumbua macho kwa wale  
wote ambao wana hamu na kiu ya uelewa mzuri na utambuzi wa  
suala la “*Wilaya*.”

## MLANGO WA KWANZA

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

### MFUMO WA WILAYA KWA MTAZAMO WA QUR'AN

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ  
يَأَيُّهَا الرَّسُولُ بَلَّغْ مَا أُنزِلَ إِلَيْكَ وَإِنَّ لَمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَّغْتَ  
رِسَالَتَهُ وَوَاللَّهُ يَعْصِمُكَ مِنَ النَّاسِ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ  
الْكَافِرِينَ

Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako; na kama hutafanya, basi (ni kama) hukufikisha ujumbe wake. Na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu makafiri. (Qur'an. 5:67)

## MWONGOZO NA LENGO LA UUMBAJI

Mada ya mjadala hapa ni Mfumo wa *Wilaya*. Umuhimu wa maarifa na kuwa na utambuzi juu ya jambo hili unaibuka kutoka kwenye mpango wa mfumo wa mwongozo ambao Mwenyezi Mungu ameuweka wakati na baada ya kuumba binadamu. Sehemu moja ya mfumo wa mwongozo ambao unahusiana na uumbwaji wa binadamu inajulikana kama Mwongozo kwa hulka asilia (*Hidayat al-Fitri*). Sehemu moja ya mwongozo imo ndani ya mwanadamu mwenyewe na nyingine iko nje yake ambayo inapatikana kupitia elimu, utambuzi, wahyi na ulinganjo (*tabligh*). Mahitaji yote juu ya uhai wa mwanadamu yanafikiwa kwa ujumla kwa mkusanyiko wa aina zote hizi za mwongozo wa ndani na ule wa nje. Na mkusanyiko wa zote hizi unajulikana kama dini. Dini ndio mwongozo wa binadamu. Lakini neno mwongozo linamaanisha nini?

Mwongozo ni kumpatia binadamu njia hizi, rasilimali, elimu, tarifa ambapo kwa kupitia hivi anaweza akafikia lengo la kuumbwa kwake. Ni muhimu kusisitiza kwamba njia yoyote inayowezekana, chanzo na elimu, mwelekeo unaomwongoza mwanadamu kwenye lengo lake la kuumbwa linakuja chini ya mwongozo.

Sehemu moja ya huu mkusanyiko wa mwongozo ni elimu na maarifa, hii ni kwa sababu mwanadamu hawesi kufikia lengo la kuumbwa bila ya haya. Hakuna mbadala wa elimu na maarifa ambao kupitia huo mwanadamu anaweza kufikia hilo lengo la kuumbwa. Ni muhimu vilevile kuainisha hilo lengo la kuumbwa. Lengo la kuumbwa ni kukutana na Mwenyezi Mungu (Liqaullah) - (Kwa maelezo zaidi juu ya hili rejea kwenye kitabu chetu kiiwacho Fal-safa ya Dini {‘Philosophy of Religion’}), na hilo ni sawa sawa kwa wote wanaume na wanawake. Wao wanatofautiana katika jinsia tu, bali lengo la uhai na uumbwaji ni lilelile, kwa vile lengo lina uhu-

siano na thamani ya asili ya mwanadamu na wala sio mwanadamu kama yeye tu. Kwa kawaida huwa tunalitafsiri kimakosa lile lengo la kuumbwa kwamba ni kifo au kuangamia kwa uhai, au kupata sehemu ndani ya pepo na neema za peponi. Neema hizi ni namna tu ya msukumo wa kufikia lengo halisi ambalo ni kukutana pamoja na Mwenyezi Mungu.

Huko kukutana au kuwa na muungano na Mwenyezi Mungu sio kwa kimwili kama vile kukutana mionganini mwa binadamu mbalimbali. Kukutana huku ni kwa hali tofauti na kunaweza kueleweka kwa msaada wa mfano huu. Kukutana huku ni kama kule kukutana kwa mwanafunzi na mwalimu. Lakini sio ule mkutano wa ana kwa ana wa mwanafunzi na mwalimu wake, ambapo anakutana na mwalimu na kumsalimia na mwalimu naye akamsalimia kwa kujibu salamu zake. Bali, badala yake hapa mwalimu inahusika na mtu mwenye ubora fulani, sifa na elimu. Mwanafunzi ndiye ambaye hana elimu katika kukutana kwake na mwalimu wake kwa mara ya kwanza, lakini anaanza kupata elimu kidogo kidogo kutoka kwa mwalimu wake na hivyo kunyanya kiwango chake cha ukamilifu wa elimu katika nafsi yake mwenyewe. Halafu, siku baada ya siku, ule umbali wa msingi wa elimu unaanza kupungua taratibu kati ya mwalimu na mwanafunzi. Katika siku ya kwanza, pale walipokutana, umbali huo ulikuwa mkubwa sana, kwa sababu huyo mwanafunzi alikuwa hana elimu japo kidogo kabisa, lakini baadaye akaianza safari yake ya kupata elimu. Matokeo yakawa ni kwamba, siku baada ya siku alikuwa anaupunguza urefu wa umbali huo kutoka kwa mwalimu wake. Kisha mwishowe inakuja siku ambayo anakuwa karibu sana na kwenye kiwango cha elimu aliyokuwa nayo mwalimu wake. Kwa kweli inatokea pia kwamba anakivuka kiwango cha ujuzi wa mwalimu wake. Kuzidi huku kwa ubora wa mwanafunzi juu ya mwalimu wake kunawezekana

tu wakati uhusiano huo ni baina ya viumbe wawili, bali sio pale uhusiano ukiwa ni baina ya kiumbe na Muumba.

Katika uhusiano kati ya kiumbe na Muumba, huyo kiumbe hawezi kamwe kumzidi Muumba; wala kiumbe kuweza kufikia ki-wango sawa na kile cha Muumba, lakini ni dhahiri kwamba anawenza kupata ukaribu bora kwa Muumba kiasi iwezekanavyo. Maana ya upatikanaji huu wa ukaribu au ujirani unaweza kueleweka kutokana na ukweli kwamba wakati wowote tunapotekeleza kitendo chochote cha kiibada, huwa tunaanza na manuizi (*niyyat*) ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu (*Qurbatan ilallah*). Hii ni kwa sababu dhati ya Mwenyezi Mungu ni mkusanyiko wa sifa kamilifu na bora na kilele chake (ambacho kwa uhalsia hazina ukomo), ambapo mwanadamu anaanza mahali ambapo hana sifa zozote. Pole pole anaanza kuzijenga sifa hizi, moja baada ya nyingine katika shaksia yake. Hii ndio tanayoiita kama Safari ya Ujirani (au ukaribu) na Mwenyezi Mungu. Na wakati mwanadamu anapofikia ile hatua ambamo anapata sifa zote zinazowezekana, hapo ule umbali kati yake yeche na Mwenyezi Mungu unapungua. Sasa, mwanadamu huyu uliyekuwa hajakamilika amekuwa binadamu kamili sasa na umbali na Mwenyezi Mungu kwa binadamu ambaye hakukamilika ni mkubwa sana ukilinganishwa na umbali wa mwanadamu kamilifu. Sababu ambayo kwamba Mitume, Maimamu na shaksia zisizotenda makosa (*maasumin*) wao wako karibu zaidi na Mwenyezi Mungu ukilinganisha na viumbe ni kwa sababu wao ni wakamilifu zaidi katika sifa zao kuliiko viumbe wengine.

Kufanya mukhtasari wa maudhui hii, kwamba dhati ya Mwenyezi Mungu ndio kilele cha ukamilifu, na hivyo ukaribu na Mwenyezi Mungu unapatikana tu pale mwanadamu anapoanza kuzikuza sifa hizi ndani ya nafsi yake mwenyewe. Kipimo cha ukaribu kita-kuwa juu ya msingi wa idadi ya sifa alizonazo katika shaksia yake.

Hatua hii ya mkuruba wa hali ya juu kabisa unaowezekana kupati-kana inaitwa “*Liqauallah*” (Kukutana na Allah) ambapo mwanadamu anakuwa mtu “mkamilifu.”

## **MFUMO – NJIA YA KUFIKIA UKAMILIFU**

Kuna njia mbili zilizofafanuliwa za kufikia ukamilifu, nazo ni Elimu na Matendo. **Bali mbali na haya, mwanadamu vilevile anayo haja moja zaidi ya muhimu, na haja hiyo ni mfumo.** Mwanadamu anaweza tu kufikia elimu na kutenda vitendo vyake chini ya kivuli cha mfumo. Ili kupata mawazo ya ni nini kinachomaanishwa, na nini lengo la mfumo, tunaweza kuchukua mfano wa familia. Familia ni namna ya zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu juu yetu sisi, ambayo umuhimu wake sisi hatutambui, na kwa kweli wengi wetu hawaichukulii hii kama ni tuzo ya Mwenyezi Mungu. Allah haku-waumba wanadamu kama wanyama. Familia kwa kweli ni mazingira ambayo hatuwezi kuyashuhudia kwa macho yetu, tunachokiona ni kuta na madirisha pamoja na watu wachache wanaoishi humondani ya kuta hizo na tunaiita hiyo kama ni familia. Wakati mwingi kunakuwa na nyumba lakini hakuna familia. Hili linatokea wakati watu wanaoishi chini ya paa moja hilohilo wamekasirikiana, wala hawawasiliiani, wala hakuna heshima ama haki kwa kila mmoja wao, hakuna wajibu juu ya kila mmoja wao na zaidi ya yote haya, bado wanakuwa hawaaminiani. Mahali pa namna hii ni nyumba lakini sio familia. Familia ni kile kitu kamili ambacho kinakuja kuwepo kutokana na watu wachache na baadaye kinazaliwa kizazi kutokana na wao. Kwa kweli inazaliwa kutoka kwenye mapaja ya familia hii, kama vile mapaja ya mama mzazi. Paja la familia ni kubwa zaidi kuliiko lile la mama, kwa sababu paja hili la familia ni mfumo. Mfano wa familia kama mfumo ni mahali muhimu sana pa kuanzia. Bila

ya mfumo huu wa familia, mwanadamu hawezi kuelimishwa na kujidhamishwa, hawezi kufanikisha safari yake ya kwenye ukamilifu; hawezi kufikia hali ya muungano na Mwenyezi Mungu. Mwanadamu, bila kujali ni mwanaume au mwanamke, mwenye elimu ama mjinga, iwapo anatoka kijijini au kwenye jiji kubwa; hawezi kupata elimu na ukamilifu bila paja la huu mfumo wa familia.

Mfumo wa familia unakomeshea mipaka yake kwenye kiwango cha watu wachache ambao wanaishi ndani yake, na kisha kwa kusaidiana wao kwa wao wanaleta uwepo wa mazingira ndani yake, na katika mazingira haya wanapata kujipanga, kuwa na nidhamu na kukua kiroho. Umuhimu wa familia ni kama mti wa matunda ndani ya bustani ambao unahitaji mambo fulani katika mazingira kwa ajili ya ukuaji na uhai wake, na familia hii ambayo hutimiza mahitaji haya. Kama familia ni nzuri, basi mti wenye maua na matunda unakuja kuwepo, lakini kama familia sio nzuri basi mimea na miti yenye sumu itachipuka. Huu ndio mfumo wa kwanza ambao ultolewa kwa mwanadamu, ambamo anapaswa kuishi humo kwa chaguo la hiari yake mwenyewe. Na kwa hiari yake na nia zake mwenyewe anafanya kazi zake kwa kupata manufaa kutoka kwenye mazingira haya ya familia. Familia sio muhimu kwa sababu tu kwamba mwanadamu hawezi kutimiza mahitaji yake kwa ajili ya ukuaji wa kimwili bila ya familia. Kwa kweli, ukuaji wa kimwili wa mwanadamu unafanyika hata bila ya kuwa na familia; kwa namna fulani hata mayatima wanaishi na kukua. Wale yatima ambao hawana wa kuwalisha na kuwapatia makazi, nguo, wao pia kwa namna fulani wanamudu kukua kimwili bila ya kuwa na familia. Ukuaji wa kimwili wa mwanadamu haukwami kwa kukosa familia. Msingi mkubwa wa kukua kwa mwanadamu ni ule ukuaji wa sifa za ubinadamu ndani ya nafsi yake, ukuaji wake wa kiroho na nidhamu ya nafsi yake. Wajibu wa familia ni zaidi hasa kwa ajili ya nafsi kuliko kwa ajili ya mwili. Hata mahusiano kati ya

mwanaume na mwanamke, pale wanapohitajiana ni kwa ajili hasa ya mahitajio ya kiroho kuliko ya kimwili. Kadhalika mtoto anawahitaji wazazi wake kwa ajili ya ukuaji wake wa kiroho zaidi kuliko ule wa kimwili. Kwa upande wa kimwili, ye yote yule anaweza akamlisha, na sio lazima alishwe na wazazi. Lakini ukuaji wake wa kiroho, elimu na ukamilifu hauwezi kufikiwa bila ya wazazi na mfumo wa familia. Hivyo familia kwa uhalisia ni shule na sio tu kituo cha kulishia, basi.

Ukuaji na maendeleo ya mwanadamu kiroho pia una mipaka yake ndani ya familia, hii sio kwa sababu familia ina mipaka, laa, ni kwa sababu vipimo na uwezo wa nafsi ya binadamu ni vya hali ya juu kabisa kiasi kwamba familia haiwezi kutimiza mahitaji ya nafsi hiyo. Nachukulia mfano hapa wa baadhi ya mimea ambayo hupandwa kwenye vyungu vya maua ambamo vinakua kwa kiasi fulani cha muda. Baada ya muda huo, mimea hiyo haiwezi ikakua zaidi ndani ya chungu, sasa inahitaji kuhamishiwa kwenye bustani au shambani. Hii ni kwa sababu inapaswa kuendelea kukua na kuwa miti yenyne nguvu na kuzaa matunda, na hili haliwezekani kutoka ndani ya kijichungu kidogo cha maua. Familia ni muhimu kwa ukuaji wa mwanadamu, lakini wajibu na umaarufu wake unaishia kwenye mipaka ya uwezekano wa chungu cha maua. Hii ina maana kwamba mwanadamu huyu katika hatua fulani ya ukuaji wake anahitaji mfumo mkubwa zaidi ya huu mfumo wa familia. Bila ya mfumo mkubwa kuwepo mwanadamu kamwe hawezi kufikia ukamilifu. Huu mfumo mkubwa unaweza kuitwa jamii au Umma. Namna ambavyo kuna sharia na kanuni ndani ya familia, huu mfumo mkubwa zaidi wa jamii ama Umma kadhalika unahitaji seti ya kanuni na taratibu ili kujenga mazingira. Hili pia ni paja la elimu kwa ajili ya wanadamu.

## QUR’AN TUKUFU – SILABASI YA MAISHA

Mada iliyo kwenye mjadala ni “Mfumo wa Wilaya” katika mtazamo wa Qur’ani.

Qur’ani Tukufu ni Kitabu cha Mungu kwa ajili ya mwongozo na fursa ya wanadamu. Ni Kitabu cha mwisho ambacho ni mfumo kamili wa sera kwa ajili ya maisha ya mwanadamu. Haiwezekani kwamba kitu chochote ambacho ni muhimu kwa ajili ya mwongozo wa mwanadamu kiwe hakimo katika Kitabu hiki Kitukufu. Ili kupima ukubwa wa mwongozo uliomo katika Qur’ani Tukufu na kuenea kwake, ni muhimu kwanza kupima ukubwa wa mipaka ya maisha ya wanadamu wenyewe. Ni kanuni ikubaliwayo kwamba kila kitu kinachohusishwa na wanadamu hakiwezi kupimwa mpaka kwanza uhai wa wanadamu upimwe na kuchambuliwa. Dini ni kwa ajili ya wanadamu na kwa hiyo ili kuitambua dini ni muhimu kwanza kumtambua mwanadamu. Sasa hivi ziko itikadi nyingi, fikra na dini zilizopo ulimwenguni, msingi nyuma ya wingi huu ni kwamba zote zina mtazamo tofauti kuhusu kuumbwa na kuwepo kwa wanadamu. Ni sharti la wajibu la madhehebu zote hizi kuelezea mipaka ya wanadamu kabla ya kuchapisha silabasi ya maisha kwa mujibu wa itikadi zao. Kwanza lazima wawasilishe uhalisia wa wanadamu na kumtambulisha mwanadamu mbele ya wanadamu. Uislamu kama dini na kwa bayana kuititia Qur’ani Tukufu umekamilisha kazi hii. Na kwa vile kutokana na mwelekeo huu unaweza tu kutambua mahitaji halisi ya wanadamu, ilikuwa ni lazima vilevile kuelewa mahitaji ya wanadamu ambayo hutimizwa na dini.

Hii ndiyo sababu ya msingi ya tofauti kati ya dini mbalimbali, je mwanadamu ni mada tu au mada na nafsi. Je uhai wa wanadamu huisha kwa kufa au huendelea zaidi, na je uhai kabla ya kifo ni wa asili ya kibinagsi tu au ni wa kijamii. Hivi ni vitu ambavyo kwamba

kama dini haiwezi kuelezea mtazamo wake haiwezi kuchapisha silabasi ya maisha yenyewe kutegemea juu ya itikadi za dini hiyo. Na hii ni kazi iliyofanywa na Qur’ani Tukufu; kwanza ilimtambulisha mwanadamu, ikamtafsiri mwanadamu, ikaelezea mipaka na uhalisi wake; na kisha pamoja na hili halikadhalika ikawasilisha mipaka ya mwongozo. Kwa vile maisha ya mwanadamu hayaishii kwake yeye mwenyeye, na Qur’ani yenyewe imewasilisha vipengele vyatya maisha ya mwanadamu, na vilevile imeonesha mfumo wa kijamii kwa ajili ya mwanadamu.

## **MFUMO ULIOWASILISHWA NA QUR’ANI TUKUFU**

Maisha kwa ujumla huhitaji mfumo, jinsi ambavyo maisha binafsi ya mwanadamu yanavyohitaji nidhamu na utaratibu wa itifaki, na halikadhliku maisha ya kijamii ya mwanadamu pia huhitaji mfumo. Maisha yenyewe nidhamu na yaliyopangwa vizuri yana uwemo wa kupokea mwongozo, na maisha ya aina kama hiyo ni yale yaliyopatiwa fursa. Hii sio mahususi tu kwa ajili ya Uislamu kama dini, hata dini nyingine yoyote au madhehebu tu ya mwanadamu, haiwezikani kwao kutayarisha katiba kwa ajili ya wanadamu bila kufikiria vipengele vyatya kijamii vyatya wanadamu. Na hususan wakati katiba inalenga kujumuisha maisha ya kijamii ya wanadamu, basi ni lazima kuelewa kadiri za kijamii za mwanadamu kama kiumbe.

Mfumo ambao Qur’ani Tukufu imeuleta kwa ajili ya maisha ya kijamii ya mwanadamu hujulikana kama “**Mfumo wa Wilaya.**” Ni kawaida kwamba chini ya kimvuli cha ustaarabu mwanadamu anaweza tu pia kuishi maisha yake binafsi. Mfumo huu huu katika msingi wa dhahiri fulani zilizomo humo vilevile hujulikana kama

**“Mfumo wa Uimamu na Umma”.** Ingawa maana ya Uimamu na *Wilaya* ni tofauti, lakini kwa vile *Wilaya* ni msingi wa mwanzo wa Uimamu, kwa hiyo kwa matokeo hayo Uimamu na *Wilaya* imetokea kuwa ni majina mawili kwa mfumo huo huo.

## DHANA POTOFU KUHUSU MFUMO WA WILAYA

Mfumo wa *Wilaya* leo ni mfumo usiofahamika ulimwenguni, kwa Waislamu wenyewe na hususan kwa kundi lile ambalo huchukulia *Wilaya* kama neema na utambulisho kwao, hata kwao *Wilaya* kama mfumo haitambuliwi. Kwa kweli *Wilaya* au Uimamu huwasilishwa tu kama imani, na jinsi kitu chochote kinavyowasilishwa pia kitatambuliwa katika misingi hiyo hiyo. Kuanzia ujio wa Uislamu tofauti ambazo zimejitokeza kati ya makundi zimeacha athari juu ya Uislamu, na moja ya athari ya hizi tofauti ilikuwa ni *Wilaya* ambayo ilikuwa ni mfumo uliobadilishwa kuwa suala la kiimani linalojadilika. Wanachuoni na wanatheolojia wanaizungumzia *Wilaya* kama suala linalohusika na Theolojia, sababu ikiwa ni tofauti ambazo zilianza mwanzoni na zilikuwepo katika historia katika muundo huu au mwingine na zipo hata hadi leo. Tofauti na midahalo hii na mabishano yanayohusika na tofauti hizi yamebadilisha kabisa mwelekeo wa suala hili (*la Wilaya*). Namna ilivyowasilishwa ilibadilisha *Wilaya* kuwa suala la imani na theolojia na kwa kuikubali imani hii mtu anaweza kuwa muumini, na kwa njia hii haki na wajibu za *Wilaya* na Uimamu vilevile zinakuwa zimefikishwa (yaani, kwa kukubali tu Uimamu na *Wilaya* kama imani). *Wilaya* kama mfumo haikuwasilishwa na pia haikukubaliwa kama suala linalohusika na mfumo wa utawala. Namna Ma’asumin (as) walivyowasilishwa *Wilaya* ilikuwa ni mfumo na tunazo rejea mbalimbali kuthibitisha hili,

kwa vile mjadala wetu umewekwa juu ya Qur'ani Tukufu nitaliweka suala hili katika utajo wa Qur'ani yenyewe. Lakini kwa kuonesha tu kwamba Ma'asumin (as) vilevile wameiwasilisha *Wilaya* kutoka kwenye Qur'ani, chanzo cha wazi kabisa kuthibitisha kwamba *Wilaya* sio imani tu, bali ni mfumo, ni kutoka kwenye hadithi ya Imam Ridha (as).

## **USHIA – JINA NA SURA YA UISLAMU, SIO MADHEHEBU**

Ni sawa na uelewa wetu usio sahihi kuhusu Ushia kama madhehebu. Ushia kamwe haujawa madhehebu. Ulikuwa na bado ni sura ya Uislamu, lakini ulibadilishwa kuwa madhehebu. Leo bado pia katika akili zetu tunaitikadi kwamba Ushia ni madhehebu ya Uislamu kama madhehebu nyingine. Lakini hili limetokea wakati ambapo jina na ukurasa wa kwanza wa Uislamu vilibadilishwa na kuwa moja ya tawi au madhehebu ya Uislamu. Hapa ndipo ncha ya ugwe ilipoachwa na njia ikapotea. Tunaweza kuliona kama jambo la dhahiri ambalo kuna vitabu mbalimbali vilivyojazwa kwa hoja hizi zinazohusika na uanzishwaji wa Ushia. Mashia na wasio Mashia wote wameshughulika katika kubishana juu ya chanzo cha madhehebu ya Shia, ni katika mwaka gani tofauti hizi zilianza na lini na vipi. Ni wazembe kuhusu habari hii kwamba Ushia ulianza wakati ule Uislamu ulipoanzishwa. Haya ni mazungumzo yasiyo na maana kutafuta ni mwaka gani madhehebu ya Ushia yalijitokeza. Utengenezaji wa jina ultokea pamoja na utengenezaji wa suala hili. Siku ambayo Uislamu ulizaliwa; vilevile jina lilijitokeza pamoja nao. Hili pia huhitaji maelezo kwamba Ushia sio madhehebu bali ni jina la Uislamu. Tunahitaji kurejea, marejeo ya Umma kuelekea kwenye chanzo cha Uislamu. Imamu Khomein (ra) alikuwa akisema kwamba Umma unahitaji kurudi

kwenye Uislamu wa kweli, kile ambacho tunacho leo katika jina la Uislamu ni kitu ambacho hutupa sisi hisia ya kutosheka na kuridhi-ka; na hili huhitaji kupitia juu ya njia ya kurejea ili kuelekea kwenye Uislamu halisi, ambao Imamu Khomein (ra) mwenyewe ameupa jina la Uislam halisi wa Muhammad (saww). Anasema Umma lazima urudi kwenye Uislamu halisi, na kama wakirudi, basi Ushia utaonekena kama jina la Uislamu.

## **MAGEUZI YA WILAYA KUTOKA KWENYE MFUMO KWENDA KWENYE MIDAHALO**

Halikadhalika kwa Uimamu kama tukiuangalia katika mtazamo wa midahalo na mabishano, basi Uimamu utageuka kuwa somo la Theolojia. Pamoja na tofauti zote ambazo zilijitokeza kuanzia ujio wa Uislamu, sayansi nayo ikaendelea sambamba nao, ambayo jukumu lake lilikuwa ni kujadili, kuzungumza, kuwasilisha ushahidi na kad-hakika juu ya tofauti hizo, na elimu hii inajulikana kama Theolojia. Nyanja ya midahalo na ujuzi wa midahalo huweza kuchukuliwa kama moja ya elementi za elimu hii ya Theolojia. Mdahalo maana yake makundi ya pande zote za mada iliyo chini ya mjadala, hu-wasilisha uthibitisho wa kimantiki na kiusomi ili kuunga mkono na kuthibitisha madai yao. Leo midahalo ambayo tunayoionna ikitokea katika nchi yetu (Pakistan) haiwezi kuchukuliwa kama midahalo ya Kiislamu, ni kitu kingine kabisa. Mdahalo maana yake ni kuwa na midahalo ya kimantiki na kielimu, kutetea imani yako dhidi ya mtu mwengine yejote au kukana imani za wengine kwa uthibitisho wa kielimu na kimantiki. Kwa sababu ya Theolojia, *Wilaya* imegeuka kuwa nukta ya midahalo. *Wilaya* au Uimamu kama mfumo wa utawala kwa ajili ya ukombozi wa Umma wa Kiislamu kamwe haujazungumziwa katika midahalo ya suala hili, kwa hiyo *Wilaya*

imebakia tu imani na rangi yake yote imebadilika. Juhudi yote ili-kuwa ni kumfanya mtu aafikiane na kukubaliana juu ya *Wilaya* kama imani kwa kutoa ushahidi. Lakini mara mtu anapoikubali vilevile hatukujihusisha kuhusu ni *Wilaya* ya picha gani anaichora katika akiili yake. Hivi ndivyo *Wilaya* au Uimamu ilivyogeuzwa kuwa nukta ya mdahalo wakati ambapo Qur’ani Tukufu imetambulisha *Wilaya* kama mfumo kwa ajili ya mwongozo wa mwanadamu. Chanzo bora ambacho kuthibitisha hili ni hadithi ambayo wasimuliaji wengi wamechapisha, na pia marehemu Kulayni vilevile ameliainisha hili katika *Usulul-Kaafi*.

## **UIMAMU – NI MFUMO SIO IMANI TU**

Hadithi hii inatokana na Imam Ali Ridha (as) wakati alipohamishwa kutoka Madina kwenda Khurasan kwa maelekezo ya Maamun, ambayo yalifanya chini ya mpango maalum. Akiwa njiani kwenda Khurasan sehemu ijulikanayo kama Mard aliitoa hadithi hii. Hadithi mbili ni maarufu sana wakati wa safari hii ya Imam (as), alitoa hutuba nydingi na hadithi kadhaa katika safari hii, na kwa kweeli hata kabla ya kuanza kwa safari yake kutoka Madina alichukua hatua mbalimbali kuwafanya watu wawe na habari hii, kwa mfano aliwataka waliokuwa karibu naye kuandaa mkusanyiko wa maombolezi kwa ajili yake wakati alipokuwa anaondoka, lakini licha ya yote haya watu hawakuelewa kile Imam (as) alichotegemea kutoka kwao, na walifanya tu kile alichosema kama ibada tu. Wakati wa safari Maamun aliamrisha kwa nguvu kabisa kwamba Imam (as) asifanywe apitie maeneo yale ambayo wapo wafuasi wa imani ya *Wilaya* na Uimamu. Na chini ya maelekezo haya vilevile Maamun alitamka mahususi kwamba katika mazingira yoyote Imam (as) kamwe asiruhusiwe kupitia mji wa Qum. Inafaa kutafakari hapa

kwamba unyeti wa mji wa Qum ni wa kihistoria na kama Imamu Khomein (ra) alivyokuwa akisema kwamba kama wewe mwenyewe huna uwezo wa kukamata chochote, basi tazama kwenye maeneo nyeti kwa ajili ya maadui, hapo utatambua nguvu zako. Vitu vile ambavyo ni nyeti kwa maadui, basi uwe na hakika kwamba vitu hivi ni vya maana na vya muhimu wa hali wa juu sana. Unyeti wa Qum kama tunavyoona ni wa kihistoria hata ingawa wakati huo Qum ili-kuwa sio kituo cha elimu ya kidini kama ilivyo leo. Ulikuwa ni mji tu wa kawaida, lakini bado Imamu (as) hakuruhuiswa kupitia Qum. Kulikuwa na baadhi ya miji ambayo kwamba ilikuwa na wafuasi wachache wa *Wilaya*, na moja ya miji hiyo ni huu wa Mard. Wakati Imamu (as) alipoingia katika mji wa Mard aliwauliza watu kuhusu mada motomoto za namna ya majadiliano pale. Watu walimjibu kwamba mijadala zaidi na midahalo ni juu ya suala la Uimamu. Ki-sha Imamu (as) akajibu na haya ni maneno ya hadithi ilioandikwa kwamba rangi ya uso wa Imamu (as) ilibadilika, ni kwa kitu gani wanajua kuhusu ukweli wa Uimamu?

Baada ya hili ye ye mwenyewe alianza kuelezea Uimamu na aka-wasilisha kanuni na vipengele vya msingi vya Uimamu. Maneno ambayo kwamba Imamu (as) aliwasilisha yalikuwa:

إِنَّ الْإِمَامَةَ زَمَانُ الدِّينِ وَنِظامُ الْمُسْلِمِينَ وَصَلَاحُ الدُّنْيَا وَعِزُّ  
الْمُؤْمِنِينَ

**“Hakika Uimamu ni uongozi wa dini, mfumo wa Waislamu, wema  
wa dunia na heshima ya Waislamu...”**  
**(Usulul-Kafi, Juz. 1, Kitabul Hujjah, Uk. 200)**

Na akasema kwamba ngome ambayo Allah ameifanya kwa ajili ya ulinzi wa Waislamu ni “Uimamu.” Na maneno bora zaidi, ya hali

ya juu na ya kimbunguni miiongoni mwa kauli hizi ilikuwa ni namna ambavyo amewasilisha Uimamu kama mfumo:

إِنَّ الْإِمَامَةَ زَمَانٌ الدِّينِ وَنِظَامُ الْمُسْلِمِينَ وَصَلَاحُ الدُّنْيَا وَعِزٌّ  
الْمُؤْمِنِينَ

**“Hakika Uimamu ni uongozi wa dini, mfumo wa Waislamu,  
wema wa dunia na heshima ya Waislamu.”**  
**(Usulul-Kafi, Juz. 1, Kitabul Hajjah, Uk. 200)**

Hii inaonesha kwamba Uimamu ni jina la mfumo, sio imani tu. Imani humaanisha kitu ambacho huhitaji tu kukubaliwa na moyo na kuleta imani juu yake. Ingawa imani vilevile hupata kuunganishwa katika vitendo, lakini kwa dhahiri hapa jaribu kuelewa kwamba Uimamu sio imani tu ambayo tunatakiwa tu kuikubali.

Sio kama Utume, ambapo watu fulani walitumwa na Allah Azza wa Jallah na lazima tuwakubali na kuwa na imani kwao kama Mitume. Na hivyo vilevile hapa Allah Azza wa Jallah ameteua watu kumi na wawili kama Maimamu na lazima tuwaamini kama Maimamu na haki za Uimamu zinafatiliwa tu kwa kuwakubali na kuwaamini kama Maimamu. Hii sio kweli, hii haitoshi kwa mtu kuwa mfuasi wa Maimamu kumi na wawili, pamoja na hili muunganisho pamoja na Uimamu bado haujasimama, kiunganisho ambacho Allah amekianzisha kwa ajili ya Umma na Imamu. Katika *Nahjul Balaghah*, Amirul Mumminin (as) pia ametumia neno Uimamu kwa ajili ya Mfumo wa Umma, neno Umma limetumika hapa:

## فَرَضَ اللَّهُ ..... نِظامُ الْإِمَامَةِ

“Uimamu ni mfumo wa Umma”

(*Nahjul Balaghah, semi ya 252*)

Hii ina maana ni mfumo ambao umewekwa na Allah ili kuedesha mwenendo wa binadamu, ambao huhitaji mfumo. Kwa kukusanya tu taarifa fulani kuhusu mfumo au kuwa na imani nao na hautekelezi. Mfumo huhitaji utekelezaji. Mpaka mfumo utekelezwe na kusimamishwa vinginevyo madhumuni au malengo yake yatakuwa hayakufikiwa, na mwanadamu hawezi kupata faida zote za mfumo huo.

Ili kuelewa haya vizuri tunaweza kuchukulia “Uimamu” kama sawasawa na mifumo mingine ambayo ni matokeo ya akili za watu, na hii ni mifumo mbadala iliyofanywa na wanadamu ambayo kwa mujibu wa istilahi ya Qur’ani huitwa “Ndama wa Samiri.” Waktati Allah Azza wa Jallah anapotambulisha kitu na kama wanadamu watatengeneza kitu cha kwao wenyewe, basi Qur’ani hufananisha vitu hivyo vilivyotengenezwa na mwanadamu na “Ndama wa Samiri.” Mifumo iliyotengenezwa na wanadamu dhidi ya mfumo uliol-etta na Mitume ni “Ndama za Samiri.”

Ni katika kundi gani itatupasa kuweka Uimamu kwa ajili ya kulinganisha na kitu kingine kile? Kwa vile Uimamu ni mfumo wa Mungu utawekwa dhidi ya hiyo mifumo ya wanadamu ambayo ili-kuwa ni, na bado ni matokeo ya fikra binafsi za wanadamu. Mifumo kama ukomonisti, demokrasia ambazo zilikuwa ni ubunifu wa akili za wanadamu husimama dhidi ya mfumo wa Uimamu, na Qur’ani Tukufu hufananisha mifumo hii iliyofanywa na wanadamu na mfano wa kadhia ya “Ndama wa Samiri.”

Watu kwa urahisi hukubali na kufuata “Ndama” hao, lakini wachache sana huvutiwa na kufuata njia iliyowasilishwa na Mitume. Kwa hiyo, Mtume Musa (as) aliwalingania watu kufuata mfumo wa Mungu kwa miaka kadhaa na ni wachache kati yao waliovutiwa nao, lakini chini ya wiki moja ya juhud, ule Umma ambao Musa (as) alikuwa ameufanya wenye kuabudu Mungu Mmoja, Samiri ali-wafanya waabudu Ndama. Watu kama Samiri wanafahamu vizuri sana saikolojia ya wanadamu na hivyo wana kipaji na ujuzi wa kupoeteza watu kutoka katika njia ya Allah Azza wa Jallah na kuwafanya waabudu “Ndama.”

Hivyo rejea nyingi kama hizo zipo katika Qur’ani Tukufu na hadithi za Maasumin (as) kwamba Uimamu na *Wilaya* ndio mifumo na sio kama imani tu.

## **WILAYA KAMA MFUMO KATIKA QUR’ANI TUKUFU**

Qur’ani Tukufu imezungumza kuhusu suala hili kwa wingi; hii ni kwa sababu Allah Azza wa Jallah ametumia jina “Walii” kwa ajili ya dhati Yake Mwenyewe pia.

اللهُ وَلِيُّ الَّذِينَ ءَامَنُوا

**“Allah ni mlinzi wa wale walioamini...” (Q. 2:257)**

Dhati ya Allah Azza wa Jallah ni mamlaka juu ya ulimwengu wote, lakini hususan kwa ajili ya mwongozo wa wanadamu sura ya Ubwana nayo pia ni *Wilaya*. Kuna muundo mmoja wa jenasi ya

*Wilaya* ambayo ni kwa ajili ya kila kiumbe katika ulimwengu, lakini pia kuna muundo mmoja zaidi bayana wa *Wilaya* ambao ni kwa ajili ya waumini. Kuna *Wilaya* moja zaidi iliyoanishwa katika Qur’ani ambayo husimama dhidi ya *Wilaya* hii bayana ya Allah Azza wa Jallah kwa ajili ya waumini. Katika Qur’ani Tukufu *Wilaya* hii inajulikana kama *Wilaya* ya Taghuti (*Wilaya* ya Shetani).

وَالَّذِينَ كَفَرُوا أُولَئِكُمْ أَلَّا طَغُوتُ<sup>٤</sup>

“...Lakini walio kufuru walinzi wao ni mataghuti...” (Q. 2:257)

Wale ambao hawaamini au wako nje ya mipaka iliyowekwa na dini; vilevile wako chini ya muundo fulani wa ulinzi (utawala) na ulinzi huo ni wa Taghuti (shetani). Hivyo hata kama mtu ataikimbia *Wilaya* ya Allah Azza wa Jallah bado ataishia kwenye muundo fulani wa utawala (ulinzi), kwa hiyo hakuna njia ya kuikwepa *Wilaya*. Mtu ambaye hayuko tayari kuikubali *Wilaya* ya Allah Azza wa Jallah lazima apime kwamba ni *Wilaya* ya nani mbali na ya Allah ambayo ameifuata. Popote aendapo lazima anahuksika na *Wilaya*. Na kama ukwepaji ni kutoka *Wilaya* ya Allah, basi lazima ajue kwamba *Wilaya* ya Taghuti inamsubiri. Kwa hiyo mkanaji wa *Wilaya* asifikirie kwamba yuko nje ya *Wilaya*, tofauti pekee ni kwamba sasa yuko chini ya *Wilaya* ya Taghuti. Qur’ani Tukufu pia inasema kwamba Allah Azza wa Jallah ni **Walii** (Mlinzi) wa waumini na wale ambao sio waumini wako chini ya ulinzi (utawala) wa Taghuti.

Inafaa kutaja hapa maana ya neno “**Kufr**” ambalo huja kwa kushirikiana na *Wilaya* ya Taghuti. Qur’ani Tukufu imetumia neno “**Kufr**” kwa uhusiano wa ukataaji au ukashajiji wa kitu. “**Kufr**” ka-

tika elimu ya *Theiolojia* hurejea katika kuutaja ukafiri. Ufafanuzi na maana zilizoelezwa na elimu hiyo ni majaribio yao wenyewe na matokeo, ambayo sayansi imeyahubiri na hii ni huduma stahiki ambayo sayansi hizi imefanya. Halikadhalika filosofia au mantiki imefafanua istilahi mbalimbali katika muktadha yao wenyewe, lakini istilahi zilizotumika katika Qur'ani zina nafasi zao zenyewe na haziwezi kubadilishwa na ufanuzi utokanao na sayansi. Hatuwezi kurejea kwenye sayansi ili kutafsiri maana ya istilahi iliyotumika katika Qur'ani Tukufu. Beramu tulizotengeneza kwa ajili ya ufanuzi wa “Kufr” ni tofauti na kile Qur'ani Tukufu inachokitaja kama “*Kufr*” kama ukushaji au ukataaji. Kama hapa:

نَّؤْمِنُ بِعَصْرٍ وَنَكُفُّرُ بِعَصْرٍ

“...Tumeamini baadhi na kukataa baadhi...” (Q. 4:150)

Hii ina maana kuamini baadhi na kukanusha baadhi. Hii huwataja waumini kama wale wanaofanana na Mbuni<sup>1</sup>, si waumini wa moja kwa moja wala wakanushaji wa moja kwa moja, ambapo humaanisha kwamba ni waumini kwa kiasi cha imani yao na katika mambo mengine ni wakanushaji. Hivyo, “*Kufr*” haina maana tu ya ukafiri; inaweza kugawanyika katika makundi mbalimbali.

Allah Azza wa Jallah alianzisha mfumo wote wa *Wilaya* kwa ajili ya ubinadamu na pia akatumia jina la Walii kwa ajili ya Dhati Yake Mwenyewe na vilevile akaupa mfumo wa kijamii jina la *Wilaya*. Allah Azza wa Jallah vilevile alianzisha “Awliyau” (walinzi) kwa ajili ya mfumo huu. Historia ya *Wilaya* katika Qur'ani Tukufu ni kubwa mno na ya zamani, lakini kwa ujumla huichukulia katika muundo

<sup>1</sup> Kwa watu wa Persia na mashariki ya mbali humuona mbuni ni kama nusu Kuku na nusu yake ni Ngamia.

wa kikomo sana. Mimi pia naanza mjadala juu ya *Wilaya* kutokana na nukta hiyo hiyo ambayo tayari ipo kwenye akili zetu, na hiyo ni tukio la Ghadir.

## TUKIO LA GHADIR

Tukio la Ghadir ni tangazo la *Wilaya* na tafsiri ya Qur'an ya tangazo hili lina utekaji wa hali ya juu na uvutiaji kwa vile lina nukta mbalimbali za kutafakari zilizooneshwa na Qur'an Tukufu. Sio kwamba *Wilaya* haikujadiliwa na Qur'an kabla; tangazo hili au Qur'an haikuelemisha popote kuhusu suala la *Wilaya*. Suala hili la *Wilaya* kama mfumo lilikuwa sehemu ya Qur'an kuanzia mwanzo wake kabisa na mwanzo wa kushuka kwake. Lakini hapa katika tukio hili la Ghadir ukamilishaji wa dini vilevile ulitokea pamoja na *Wilaya*.

Hii ni nukta muhimu sana ambayo wakati jengo linapokamilika mipaka yake pia hutajwa kama *Wilaya*, ambapo humaanisha ukubwa wa mamlaka ya eneo hilo.

Aina ya msisitizo uliopo kuhusiana na *Wilaya* haupo kwa ajili ya vitu vingine vyovyyote. Namna ambayo Mtukufu Mtume (saww) alivyoelezea na kuwasilisha dini, haikuwasilishwa baadaye kwa njia ile ile. Ilitokea katika muundo usioeleweka sawasawa na hali hiyo hiyo ilitokea kwetu sisi Mashia ambao sisi ni wadai wa kuwa ni wafuasi wa *Wilaya*, na kwa hakika ni suala la *heshima* kwetu sisi kwamba Allah Aza wa Jallah ametuhesabu sisi miongoni mwa wafuasi wa *Wilaya*. Sehemu moja salamu za Ghadir pia husema kwamba wakati waumini wanapokutana katika siku ya Ghadir, lazima wawe na shukurani na fahari kuhusu hili na kusalimiana kwa maneno haya:

الْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِي جَعَلَنَا مِنَ الْمُتَّمَسِّكِينَ بِوِلَايَةِ أَمِيرِ الْمُؤْمِنِينَ  
وَالْأَئِمَّةِ الطَّاهِرِينَ عَلَيْهِمُ السَّلَامُ

“Shukurani zote ni za Allah ambaye ametujaalia sisi kuwa pamoja na wale ambao wameshikamana na *Wilaya ya Amirul Muminin* (as) na Maimamu watakatifu, amani iwe juu yao.”

## **WILAYA – NI MOYO WA DINI**

Maandalizi na mpangilio ambao kwamba “*Wilaya*” inawasilishwa na kujadiliwa na Qur’ani Tukufu huonesha umuhimu wa suala hili. Kabla hatujaingia kwenye mjadala juu ya kipengele hiki ya jinsi “*Wilaya*” inavyowasilishwa na Qur’ani Tukufu, ni muhimu kutafakari juu ya nukta hii kwamba moyo wa dini ni “*Wilaya*.” Dini huzunguka katika mzingo wa “*Wilaya*.”

Kuna baadhi yetu ambao siku zote hujaribu kuelewa masuala ya dini kupitia hadithi, usahihi wa simulizi na misemo. Ili kuona kama kitu ni cha ukweli au ni katika misingi ya dini, hukimbilia kwa wabobezi wa fani ya hadithi ili kuchimbua na kutafiti kuhusu wasimuliaji wa hadithi, na kuhakikisha usahihi wa hadithi, hivyo, wengi wetu tumejihusisha katika aina hiyo ya uchambuzi ili kuhakikisha usahihi wa masuala mbalimbali ya dini. Ingawa hii pia ni njia ya kuthibitisha lakini ni mbinu ngumu sana na ya kuchosha, na wakati mwingi sehemu kubwa ya maisha ya wanachuoni hutumika katika kuchunguza maisha ya wasimuliaji wa hadithi. Mchakato huu huanza na mpangilio halisi wa kidini ulio chini ya uchambuzi. Kutokana na mpangilio wa kidini huiendea hadithi inayohusika na hilo, na kutokana na hadithi hiyo huangalia wasimuliaji wa hadithi hiyo na kuona watu wengi wenye jina kama hilo hilo la msimuliaji, ki-

sha huishia katika kuchunguza maisha ya watu wote hao, na lazima wachambue tabia za wasimuliaji hawa, na baada ya kufanya hivi hutambulisha na kuthibitisha iwapo msimuliaji ni mwaminifu au la. Baada ya kumthibitisha msimuliaji, huja kwenye hadithi yenewe na kisha kutokana na hadithi hiyo huja kwenye maana yake halisi. Madhumuni haswa ni kuja kwenye maana yenewe, lakini ili kufika hapo lazima wafanye juhudhi mbalimbali na kwa hiyo njia hii ina changamani (magumu) mbalimbali.

Njia nyingine ya kutambua masuala ya kidini ni kuilewa kwa mwenendo wake. Sharti kwa ajili ya hili ni kwamba mwanadamu lazima awe na ujuzi wa mwenendo wa dini. Tuna ujuzi wa tabia ya vitu vingi. Kwa mfano kama tukikutana na mtu kutoka Lahore katika sehemu nyingine ya ulimwengu, basi bila hata ya kuuliza anwani na nasaba yake, kwa kusikiliza tu maneno machache kutoka kwake tunaweza kutambua kwamba anatokana na mji wetu. Mifano mingine inaweza kuwa ya baadhi ya aina maalum ya chakula, mifano hii itakuwa rahisi kuilewa kwa sababu huenda tusiwe na ujuzi sana wa silika ya vitu vingine, lakini tuna ujuzi sana wa chakula. Kila aina ya chakula ina ladha na mtindo wake, mara tu mtu anapoonja chakula anaweza kutambua chanzo chake. Siku hizi chakula kutoka Magharibi hutambuliwa kwa urahisi kwa vile kina ladha yenyekiwiango, hivyo hata bila ya kuangalia boksi la baga (*burger*), tunaweza kujua chakula hicho kinatokana na mlolongo gani wa chakula.

Halikadhalika dini hii ina mwenendo wake; ina utamu na ladha yake. Sasa ni juu ya kiwango cha ujuzi na utambuzi wa mtu kuitambua. Wamekuwepo *Fuqaha* (wanasheria) wengi na *Mujtahidin* (watafiti) ambao tunaweza kuwapa jina la watambuzi wa dini. Miiongoni mwa hawa alikuwa ni mwenye kitabu *Fiqhul-Jawahir*, ni kitabu chenye kuaminika zaidi katika *Fiqh* yetu. Hiki ni kitabu ambacho wanachuoni wote wakubwa, Marja, *Fuqahai* na *Mujta-*

hid wamejifundisha. Kwa maneno mengine hakuna kitabu kingine juu ya Fiqh ambacho ni chenyе kutegemewa kama hiki ambacho kimewahi kuandikwa hadi leo. Ingawa kuna vitabu vingi vikubwa na vidogo juu ya Fiqh lakini hakuna hata kimoja hadi leo ambacho kimechukua nafasi ya *al-Jawahir*. Mtu huyu ambaye anajulikana kama *Sahibul-Jawahir* (mwandishi wa kitabu Jawahir) ameuelewa mwelekeo wa dini na hii ndio sababu Imamu Khomein (ra) amekuwa mvutiaji wake mkubwa na ana imani kubwa juu ya mtu huyu. Imamu Khomein alitoa wosia kwa wanachuoni na wanafunzi kwamba lazima waichukulie *Fiqhul-Jawahir* kama mhimili wao wa mafunzo ya Fiqh na kwa kutumia mbinu ya *al-Jawahir* watafanya watagundua hukumu za sharia na Ijtihad (utafiti). Faqihi huyu mwandishi wa kitabu *al-Jawahir* vilevile ametoa hukumu ileile ambayo mafaqih wengine wengi wameitoa, lakini Fiqh yake ina kitu cha kiheshima.

Katika *al-Jawahir* mna vitabu vidogo mbalimbali na mionganoni mwa hivi kuna sura moja ya Jihad. Katika sura hii; kwa maelezo kamili na kwa wazi ametamka kwamba: “**Mtu ye yote ambaye ha-vutiwi na dhana ya Wilayatul-Faqih katika macho yangu bado kabisa hajaipata ladha ya Fiqh.**” Ni muhimu kutafakari hapa na kukumbuka kwamba *Fiqhul-Jawahir* ni Fiqh yetu ya kawaida ili-yokubali kuendelea, na *Sahibul-Jawahir* ni Faqihi wa zamani sana ambaye amesoma Najaf na wanasheria wengi wakubwa walikuwa wanafunzi wake na hata vizazi vingi vijavyo vya wanasheria watakuwa pia mionganoni mwa wanafunzi wake. Mtu wa kiwango kama hicho, mwanasheria mkubwa anasema kwamba mtu ambaye hakubali *Wilaya* ya Faqih hajapata kabisa ladha ya Fiqh. Hii ndio sababu Imamu Khomeini (ra) akaagiza kumfanya ye ye kama mhimili wa Fiqh yetu. Wamekuwepo na wapo watu wengi wa maana lakini ni wachache sana mionganoni mwao ambao walikuwa wanaitambua dini kwa silika yake.

Watu kama Shahid Ayatullah Murtadha Muttaahhari, Imamu Khomein (ra) na Shahid Baqir Sadr ni mionganoni mwa wale wachache ambaao ni watambuzi wa dini kwa silika yake. Wanaweza kutambua kutokana na silika ya dini iwapo kitu kilichosemwa ni sehemu ya dini au la. Halikadhalika mashairi ya Allama Iqbal yana mtindo mahususi na silika. Sio muhimu kwamba mtu lazima afungue kitabu na kutuambia kwamba mashairi haya ni kazi ya fasihi ya Allama Iqbal; tunaweza kutambua kutokana na mwenendo wa mashairi yenye. Kama kitu kilichosemwa kinahusiana na uamsho basi hicho ni shairi la Iqbal na kama kitu kilichosemwa ni cha kuwafanya watu wachoke na wanyamaze, basi hata kama mtu huyo aape kwa Qur'an hatuwezi kukubali kuwa kimesemwa na Allama Iqbal. Hii ni kwa sababu Iqbal alikuwa mwanamapinduzi ambaye aliamsha watu wala hakuwa mhubiri wa dini ya kulala na uchovu. Alikuwa ndiye yeye mwenyewe aliyekuwa ameamka na alikuwa akiwafanya watu watanabahi na kuamka. Yeye mwenyewe alisema:

*“Kumfanya mtu aanguke kwa kutoa huduma ya vimeo  
ni rahisi kwa kila mtu.*

*“Ewe mhudumu wa baa, furaha halisi itakuwa  
kumsaidia mwenye kuanguka.”*

Iqbal hakuwa mshairi mlevi kama washairi wengine wengi ambaao huwahudumia walevi katika mashairi yao na kuwafanya watu walale. Iqbal alikuwa mtu ambaye alikuwa akiondoa athari za vimeo juu ya wale ambaao walikuwa wamelewa. Hivyo mtu ambaye ana uzoefu wa mwelekeo wa kazi za Iqbal anaweza kwa urahisi kutambua maneno yake.

Moyo wa dini ni “Wilaya” na kila kitu kutoka kwenye dini kina rangi ya “Wilaya” ndani yake. Sio kwamba “Wilaya” ni kitu king-

ine na dhidi ya kitu fulani. Kama kuna Upweke wa Mungu katika dini basi hicho pia huwa na rangi ya “Wilaya” ndani yake. Utume, Uimamu, Kiyama, Ibada, Sheria, Maombolezo, Misikiti, Huseiniya, mikusanyiko na maandamano kila kitu kina rangi ya “Wilaya” ndani yake. Kila kitu kina rangi na silika ya “Wilaya” ndani yake, na kutokana na mwenendo huu wenyewe tunaweza kuona kwamba hili ni suala la dini. Kama kitu hakina mwelekeo wa “Wilaya” ndani yake unaweza kusema kwa kujimini kabisa kwamba hiki sio kitu cha kidini.

Huu ni ukweli kwamba “Wilaya” ni moyo wa dini, na Allah Azza wa Jallah ameifanya mhimili wa dini. Sio kwamba nasema yote haya kwa fikra zangu mwenyewe ili kuamsha hisia zako, haya ni maneno ya Maasumin (as), na Allah *Azza wa Jallah* ambaye Mwenyewe ni Walii wa waumini ameelezea kwamba Wilaya ni mhimili wa dini na dini inazunguka katika mzingo wa “Wilaya.” Kuna kitabu cha Shi’ah cha kuaminika cha hadithi kinachoitwa “Wasailus-Shi’ah” na katika jalada la kwanza la kitabu hicho linalohusu masharti ya ibada, mwandishi wa kitabu ametengeneza Sura ambayo ina hadithi nyingi zenye kuhusika na “Wilaya,” moja mionganoni mwa hizo ni hadithi mashuhuri sana, nayo ni:

**بُنِيَ الْإِسْلَامُ عَلَى خَمْسٍ: عَلَى الصَّلَاةِ وَالزَّكَاةِ وَالصَّوْمِ  
وَالحَجَّ وَالوِلَايَةِ**

**“Uislamu umejengwa juu ya misingi mitano: Sala, Zaka, Saumu,  
Hija na Uimamu.”**

(Wasail-us-Shia/Usul-e-Kaafi, Juz. 2, Uk. 18)

Kuna hadithi mbalimbali sawa na hii hapo juu, na Maasumin (as) wameirekebisha hadithi hiyo hapo juu kwa kusema kwamba nguzo zote hizo tano hazifanani, moja ya nguzo hizo ndio nguzo ya msingi na mzizi wake, zilizobakia ni nguzo zinazofuatia. Maasumin (as) wanasema kwamba nguzo ya muhimu zaidi na ya msingi wa Uislamu ni “*Wilaya*.”

Msisitizo na kiwango cha ulinganiaji kwenye “*Wilaya*” hauonekani kwa kitu kingine chochote. Hivyo hili lazima liwekwe juu ya akili zetu kwamba mwenendo, mhimili na rangi ya dini kati-ka uhalisi ni “*Wilaya*”. Hatuwezi hata kuitenganisha dini kwenye sehemu mbalimbali ili kusema baadhi ya sehemu zinahusiana na “*Wilaya*” na nyingine hazihusiani, sio hivyo, zote na kila suala na elementi ya dini ina rangi ya “*Wilaya*” juu yake. Kuanzia na Tauhid mpaka suala la mwisho la Uislamu kila kitu kina silika ya “*Wilaya*” juu yake. Wakati kila kitu kina uelekeo wa “*Wilaya*,” basi Allah *Azza wa Jallah* vilevile kwa ajili ya mwongozo wa wanadamu ametumia jina la “Walii” kwa ajili Yake Mwenyewe na ameuita mfumo uliundwa kwa ajili ya wanadamu kama “Mfumo wa *Wilaya*.” Kisha kwa ajili ya mfumo huu Allah *Azza wa Jallah* aliwateuwa “Mawalii” (Walezi), akawatambulisha kwa wanadamu na vilevile kwa uwazi akaainisha kwamba msikubali uongozi wa yejote yule mbali na hawa. Hii ni kwa sababu ni ukweli kwamba kama huwezi kuwakubali kama viongozi wako basi lazima utamkubalia mtu mwagine kama kiongozi wako. Kama unajaribu kutoka nje ya “*Wilaya*” basi vilevile utaishia kwenye “*Wilaya*” pamoja na tofauti moja tu kwamba kwa kuikwepa “*Wilaya*” ya Allah unaishia kwenye “*Wilaya*” ya Shetani. Hakuna njia ya kukwepa kutoka kwenye “*Wilaya*”, amma uwakubali Walezi walioteuliwa na Allah au vinginevyo Shetani atakuwa Mlinzi wako.

## TANGAZO LA WILAYA

Ilielekezwa kwa Mtukufu Mtume (saww) kutangaza “Wilaya” na halisia zake, msisitizo na maandalizi ambayo kwamba Qur’ani Tukufu imeliainisha hili yaweza kueleweka kutokana na Aya zake tu:

يَتَأْمِنُهَا الْرَّسُولُ بَلَغَ مَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ

“Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako...”  
(5:67)

Kuna nukta nyingi za tafsiri na ujumbe halisi ndani ya Aya hizi. Imeelezwa kwa Mtukufu Mtume (saww) kufikisha na kwamba pia alitiwa kwa jina la “Ewe Mtume.” Hili hudokeza kwamba huu ni ufikishaji wa ujumbe ulioaminishwa kwa mtu ambaye ni Mjumbe wa Allah. Katika usafanuzi wa maneno mengine inasemekana kwamba ujumbe ambao unaubeba mabegani mwako na uko katika ulinzi wako ambao kwamba umeteuliwa kama mlinzi wake, hivyo kwa wewe kuwa Mjumbe wa Allah fikisha ujumbe huo. Ujumbe huo ambao umeteremshwa kupitia kwako na Mola wako ni mfumo ambao lazima ufikishwe kwa watu. Na sambamba na hili pia ilisemwa:

وَإِنْ لَمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَغَتِ رِسَالَتِهِ وَلَمْ

“...Na kama hutafanya, basi utakuwa hukufikisha ujumbe wake...”  
(5:67)

Kauli “**Kama hutafikisha hili**” kwa Kiarabu katika Aya hii katika uwasilishaji wa kawaida inaweza pia kutafsiriwa kama “Kama hutafanya hili.” Katika hali ya kinahau ni fasihi ya kweli inayokubalika kwamba aina ya msemo kama huo hutumika kwa mtu ambaye amefanya kama hivyo kabla, hii ina maana kwa mtu ambaye alipewa ujumbe ili kuufikisha hakufanya hivyo wakati uliopita. Hivyo inakumbushwa kwake kwamba usifanye kama ulivyo fanya kabla wakati ulipoambiwa kufikisha ujumbe lakini ukashindwa kuufikisha, hivyo usifanye kosa kama hilo sasa.

Lakini aina kama hiyo ya matendo haionekani katika shaksia ya Mtukufu Mtume (saww) wala katika Qur’ani Tukufu, katika hadithi au mahali popote katika historia. Aina kama hiyo ya tabia mbaya hailingani na dhati tukufu ya haiba yake Mtukufu Mtume. Huu ni ukweli uliothibitishwa kwamba kamwe haijawahi kutokea kwamba Mjumbe alipewa ujumbe na *Allah Azza wa Jallah* na akashindwa kuufikisha. Na hususani hali ambayo kwamba Mjumbe alielezwu jinsi ya kufikisha ujumbe huo, kamwe sio hali ngumu, wakati ambapo Mjumbe alifikisha ujumbe wote katika hali ngumu na ya mashaka. Kwa kweli hali ya kuchoka na uchovu ambayo kwayo alikuwa akiifikisha ujumbe wote ilimfanya hata Allah Aza wa Jallah amwachishe kuchukua tabu hiyo na maumivu.

لَعَلَّكَ بَذَخُّ نَفْسَكَ

**Huenda ukaiangamiza nafsi yako...” (Q. 26:3)**

Qur’ani inamuuliza Mtume (saww) kwamba kwa nini anaiweka nafsi yake katika hatari kwa ajili ya kuwaongoza watu, kwa ajili ya kufikisha ujumbe? Allaha *Azza wa Jallah* Mwenyewe ilibidi aseme

kwamba sio lazima kujichosha kiasi hicho, weka juhudini tu katika kiasi kinachowezekana. Hii inathibitisha kwamba Mtume huyu (saww) alikuwa sio aina ya mtu ambaye amewahi kuonesha uzembe wowote au tabia ya uchovu katika kufikisha amri za Mungu na ujumbe. Basi kwa nini Qur'ani inasema "Kama usipofanya hivi!"

Tafsiri ya hili inaweza kueleweka hali kadhalika pamoja na tabia ya nyakati zilizooneshwa na wanadamu wakati ambapo kitu fulani kimekusudiwa kwa mtu fulani lakini kinasemwa kwa mtu mwingine. Hii ni moja ya metholojia zilizochukuliwa na Qur'ani Tukufu wakati ambapo vitu vingi vilivyokusudiwa kwa ajili ya watu vimeelekezwa kwa Mtukufu Mtume (saww), na utaratibu huu unakubaliwa vizuri kiasi kwamba katika mifano mingi katika Qur'ani mzungumziwa aliyekusudiwa hasa ni mtu mwingine. Lakini kwa nini utaratibu (metholojia) kama huo umefuatwa, kwa nini Qur'ani isimtamkiele moja kwa moja? Pengine Qur'ani haiwachukulii kuwa ni wenye kufaa kuzungumziwa moja kwa moja kama pale Qur'ani inaposema:

ـ قُلْ يَتَآمِنُهَا آلُّكَافِرُونَ ـ

“Sema! Enyi makafiri!”

Qur'ani inamwambia Mtume "**Mtume sema! Enyi makafiri!**" Qur'ani haiwaambii moja kwa moja makafiri. Huenda umepata kuona wakati kuna mgogoro kati ya mume na mke, na hata kama wamesimama kwa kukaribiana wanawasiliana kuitia watoto. Ingawa wanasiliza maneno ya kila mmoja wao lakini hawawasiliani moja kwa moja, mume anamwambia mtoto kumwambia mama yake. Huu ni uthibitisho wa kukasirikiana wenyewe kwa wenyewe. Halikadhalika Qur'ani inamwambia Mtume kuwaambia makafiri kwa

sababu hawafai kwetu sisi kuwaambia moja kwa moja. Kwa hiyo, aina hii ya metholojia inafuatwa na Allah *Azza wa Jallah* katika mifano mingi.

Katika hali hii ya Ghadir iliamuliwa kwamba Mtume (saww) wakati akiambiwa kufanya kitu hatafanya, kwa hiyo, ilisemwa kwa kupitia kwa mtu mwingine, ilikuwa inasemwa kwetu kwa kupitia njia isiyo ya moja kwa moja kwamba kama kazi hii haitakamilishwa basi madhumuni ya Utume yatakuwa hayakukamilika.

Nukta ya pili ambayo huja katika sehemu hii ya Aya ni kwamba kwa nini hakutakuwa na chochote kitakachokamilika kama ujumbe huu hautafikishwa? Mjumbe amefikisha dini kamili, matendo yote ya wajibu, mambo yaliyopendekezwa, yaliyokatazwa, mambo yasi-yopendekezwa, kanuni za ibada, yote na kila kipengele kidogo kidogo cha masuala ya kidini kilifikishwa katika miaka hii ishirini na tatu ya mwisho. Wakati mwingine baadhi ya wanachuoni wanasema kwamba dini ni pana sana na kuthibitisha upana wa dini wanankuu mfano kwamba dini imeelezea pia adabu za kuingia chooni. Wakati dini imekwenda mpaka kwenye kipengele kidogo kama hicho cha maisha, basi vipi kuelekea mwishoni inasemwa kwamba kama ujumbe huu haukufikishwa utakuwa hujafikisha chochote?

Hii ni kwa sababu ujumbe unaotaka kufikishwa sasa ni wa muhimu zaidi, mengine yote yaliyobakia yoyote yale yawayo ambayo yamefikishwa mpaka sasa ni jengo lakini ujumbe huu ndio nguzo zake. Jengo linaweza kusimama tu juu ya nguzo zake, kama nguzo hazikusimamishwa basi na jengo pia litakuwa halikusimamishwa na kwamba jengo hilo lisilo na nguzo, vitu vya kulisa idia lisimame na msingi, basi litaanguka. Hivyo Mtume (saww) aliambiwa kuifanya kazi hiyo sasa kwa sababu ambayo kwamba dini itakuwa

ya kudumu milele na itakuwa imara. Yeye (saww) lazima awasilishe ngome ya dini, kuta za nje za dini. Na ngome hii ya dini ni “Mfumo wa Wilaya.”

## **WILAYA – NI KUWAKATISHA TAMAA MAADUI:**

Ili kuelewa ugumu huu tunahitaji kurejea kwenye Aya nyingine am-bayo iliteremshwa mara tu baada ya Mtume (saww) kutoa tangazo hilo (kufikisha ujumbe huo):

الْيَوْمَ يَعِسَى الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ دِينِكُمْ فَلَا تَخْشُوْهُمْ وَأَخْشُوْنَ

**“...Leo waliokufuru wamekata tamaa katika dini yenu, basi msiwaogope na mniogope mimi...” (Qur'an. 5:3)**

Sasa ni muhimu kusisitiza zaidi juu ya habari hii kwamba Qur'ani ilifanya maandalizi yote ili kufikisha umuhimu wa ujumbe huu. Na imesemwa kwamba kama ujumbe huu hautafikishwa basi hakuna kitakachokuwa kimefikishwa au katika maneno mengine pia inaweza kusemwa kwamba kile ambacho kimefikishwa kabla haki-tadumu iwapo ujumbe huu hautafikishwa. Kwa mfano kama unaambiwa kuweka pesa katika benki, na ukiwa kama mtu mwenye akili finyu, unakwenda kwenye benki na kuweka pesa zile juu ya meza ya benki na kuondoka. Sasa kama unaulizwa iwapo umeweka pesa zile benki, utasema kwamba ndio nilifika benki na kuweka pesa zile juu ya meza. Ingawa umefikisha pesa zile benki, lakini hukuzikabidhi kwa mtu anayehusika au mwenye wajibu pale. Kwa hiyo ufikishaji

huu ni sawa na kutofikisha kamwe kwa sababu sasa wakati utakapofika benki tena pesa zile hazitakuwa pale juu ya meza ya benki.

Hii miaka ishirini na tatu ya kuhubiri dini, kushuka kwa Qur’ani Tukufu, aya, sheria ndogo ndogo za dini na chochote kile ambacho Mtume (saww) alikifanya ilikuwa sasa akikabidhi kwenye ulinzi wa mtu fulani. Hii ni kwa sababu kama hutakabidhi kwa mtu fulani, kama humfanyi mtu fulani kuwa mlinzi wa kitu hicho, basi utaona kwa miaka michache hakuna kitu kitakachobakia. Kama ujumbe huu wa “Wilaya,” ujumbe wa mtu fulani kuwa na mamlaka ya kidini na mlinzi hautafikishwa, basi kila kitu chochote kilichofikishwa kabla kitakuwa hakina maana na hakuna dalili ya dini itakayobakia katika maisha ya watu. Kwa hiyo dini hii ilikuwa ikabidhiwe kwa mtu fulani, lakini kwa nani?

Hapa ndipo tunapohitaji kuelewa nukta ya kiuchambuzi. Maana yake ni kwamba Mtume (saww) hateui tu mtu hapa. Sio kwamba mtu mmoja anaondoka na mtu mwingine anachukua nafasi yake. Ni nukta muhimu ambayo tunahitaji kutafakari juu yake na kufikiri.

Maadui walikuwa na matumaini ya kuivunja dini kuanzia mwanzo kabisa. Walifanya kila kitu kiwezekanacho kwa juhudini kubwa sana ili kuivunja dini hii. Maadui siku zote wana tabia ya kawaiida kwamba hawaachi jani lolote bila kugeuzwa katika uadui wao. Kama hawafanyi kitu basi uwe na hakika kwamba ni kwa sababu hawana uwezo wa kufanya kitu hicho. Imamu Khomein (ra) alikuwa akisema kwamba, kama Marekani haifanyi vitu fulani bali hututishia tu kwamba watafanya hivyo, kuwa na hakika kwamba hawawezi kuvifanya hilo. Kama ilikuwa inawezekana kwao kufanya, basi wangelifanya hilo mara kumi hadi leo. Hii ni kwa sababu hawana subira ya kiasi hicho wala ndoto ya kutokufanya vitu fulani ambavyo kwamba wana uwezo wa kufanya. Hawafanyi tu vitu vile ambavyo kiuhalisi hawana uwezo wa kuvifanya.

Hata leo hii hali ni hiyo hiyo; watu nje ya Jamhuri ya Kiislamu ya Iran wana hofu, wanatishwa na wanahesabu siku ni lini Marekani itaishambulia Iran. Lakini kama ukienda ndani ya Iran na kuwaliza kuhusu hali yao, wanasema hakuna cha kuhofia, kwa sababu tunawaelewa maadui wetu vizuri sana na vilevile tunajua nguvu zetu. Kama wangkuwa na uwezo wa kutushambulia wangelifanya hivyo. Katika maneno mengine, hakuna mtu anayeweza kumeza mfupa uliomkwama kooni kwa muda wa miaka ishirini na tisa (baada ya mapinduzi). Hawana uwezo wa kumeza mfupa huu vinginevyo wan-geumeza zamani, na kwa vile mfupa huu umekwama kooni mwao, basi wao wamechanganyikiwa.

Sio kwamba hali hii ipo kwa Marekani tu, huu ni uhalsia wa kihistoria. Katika historia yote ya Uislamu chochote ambacho maadui wangeweza kufanya dhidi ya dini wamekifanya. Chochote ambacho hawakufanya basi kilikuwa nje ya uwezo wao. Maadui wa Uislamu wakati wa ujio wa Uislamu walifanya kila linalowezekana mijini Makka. Kitu kimoja walichokuwa hawakielewi ambacho kilikuwa ni matokeo ya uchambuzi wao kuhusu Uislamu kama dini, ilikuwa kwamba ni dini iliyoanzishwa na mtu binafsi. Siku zote maadui hu-fanya uchambuzi kutoka nje; hawaji ndani ya Uislamu na kuona uk-weli. Hufanya uchambuzi wao kutoka kwenye vyombo vyahabari; na kutohana na wanachuoni walionunuliwa wenyewe elimu ndogo hu-jaribu kuifahamu dini. Kama wakija ndani ya dini na kujaribu kuifa-hamu dini watapata picha tofauti. Uchambuzi wa nje amba maadui wa zama hizo walifanya ilikuwa kwamba mhimili wa dini hii ni haiba ya Mtukufu Mtume (saww). Kwa vile haiba hii ina nguvu sana ina watu mbalimbali walioambatanishwa kwake na mpaka wakati hali hii inajitokeza hatuwezi kufanya kitu chochote. Hivyo, walibuni mipango ili kuangamiza haiba hii. Walijaribu kila linalowezekana na hata walifikia kiwango cha kumuuya, na kwa matokeo ya hili

lile tukio la usiku wa hijira – kuhama – likatokea. Hawakufanikiwa katika mipango yao yote, lakini bado hawakukata tamaa.

Kuvunjika moyo kwa maadui ni tofauti na kushindwa kwao. Walijaribu mitego yote inayowezekana na mbinu, waliweka vikwazo na kumzingira Mtukufu Mtume (saww) katika bonde la Abu Talib, waliwatesa masahaba wa Mtume (saww), na walifanya kila lililowezekana lakini bado hawakukata tamaa. Kama mbinu moja iliyotumika ilishindwa mara moja walitayarisha nyingine, hata baada ya kutofanikiwa katika hili bado kamwe hawakukata tamaa. Kwa mfano walipigana vita vya Badr, wakashindwa, lakini mara moja walianza matayarisho kwa ajili ya vita vingine. Hata baada ya kushindwa katika vita kamwe hawakukata tamaa na hii iliendelea kwa muda wa miaka ishirini na tatu ambapo Mtume (saww) alinyanya bendera ya dini na maadui pia walidhamiria kuiangusha chini. Vilevile maadui walikuwa wakienea pamoja na kuenea kwa Uislamu. Ni ukweli kwamba kama mji hauna maadui wa dini basi ichukulie hiyo kwa hakika kwamba mji huo hauna dini ya kweli ndani yake. Vyote maadui na dini vitaenea sawia. Leo vilevile tunaona hali hiyo hiyo, katika hali hiyo wametengeneza vituo vingi vya dini bandia na vichomozo, lakini bado wakati tukiwaona maadui na kutokana na harakati za maadui tunafahamu ni sehemu gani ya ulimwengu inapatikana dini ya kweli.

Uhasama wa maadui uliendelea kujitokeza siku hata siku, lakini hawakukata tamaa, hii ni kwa sababu wamefanya uchambuzi wa kipumbavu usio sahihi wa hali inayohusiana na kuenea kwa Uislamu kunakofanywa na Mtukufu Mtume (saww). Kama Imamu Sajjad (as) vilevile anavyosema kwamba, “**Shukuran ziwe kwa Allah ambaye amewafanya maadui kuwa wapumbavu.**” Wakati Rais Ahmedinajad alipokwenda UNO kutoa hotuba yake, alianza hutuba yake mbele ya wote wale amba moja kwa moja au kwa njia isiyo

ya moja kwa moja ni maadui wa Uislamu kwa maneno hayo hayo ya maombi ya Imamu Sajjad (as). Huu ni ukweli kwamba wakati mwingine maadui hufanya matendo makubwa ya kipumbavu. Hata ingawa kile Yazid alichofanya kilikuwa ni kitendo cha kikatili cha dhulma na ukandamizaji, lakini huu ulikuwa ni upumbavu mkubwa wa Yazid, ambao ulishia katika kuanguka kwake. Hivi ndivyo ambavyo siku zote maadui huishia kwa kufanya upumbavu na upuuzi. Kuna uwezekano kwamba kwa ajili ya upumbavu wa maadui wafiasi wa dini pia huathirika, lakini hata marafiki wa maadui na wao pia mwishowe huathirika.

Upumbavu wa wapinzani wa Mtukufu Mtume (saww) ulikuwa kwamba walifikia hitimisho kwamba mhimiili wa dini ya Uislamu ulikuwa ni mtu mmoja, mtu huyu mmoja, yaani Mtukufu Mtume (saww). Kama mtu huyu kwa namna yoyote ataondolewa kutoka kwenye njia, basi dini hii pia itatoweka. Hili nalo pia kimsingi ni sahihi kwamba kama watu wanakuwa mhimiili wa dini au kitu kingine chochote, mara tu mtu yule anapokuwa nje ya njia, akifa au akiuliwa shahidi, vituo na vyama hivyo pia hufa, na hii ni kwa sababu mhimiili ulikuwa ni mtu. Wakati wote wa kuwepo mtu yule mambo yote huenda vizuri, mara tu mtu huyo anapoondoka basi hakuna kitu kinachobakia.

Huu ulikuwa ni uchambuzi potofu ambao uliwafanya wasikate tamaa licha ya kushindwa katika mapambano mengi. Walikuwa na matumaini makubwa kwamba hata kama hawataweza kumuua Mjumbe huyu, lakini siku moja atakufa. Hii pia ni kwa sababu Mjumbe huyu alikuwa yeche mwenyewe akisoma aya ya Qur’ani ambayo inasema kwamba:

إِنَّكَ مَيْتٌ وَأَهْبَطُهُمْ مَيِّتُونَ

“Kwa hakika wewe utakufa, na wao watakuwa.”

Maadui walikuwa wanajisikia kuridhika na kufurahi wakati wanaposikia aya hii ambayo inasema kwamba kama walivyo watu wengine Mtume (saww) pia siku moja atautoka ulimwengu huu. Na mara tu Mtume (saww) atakapotoka katika ulimwengu huu walikuwa na imani hii kwamba Uislamu nao utafikia mwisho wake, na kama haiwi hivyo; watautikisa kiurahisi na Uislamu utatoweka. Kwa hiyo, baada ya kushindwa kote walikuwa wakisubiri siku hii wakati shaksia hii ya Mtukufu Mtume itakapoondoka katika ulimwengu huu, hiyo itakuwa ndiyo siku ambayo taa ya dini itazimwa na hawatahitajika kufanya kitu chochote. Hili ndilo lililokuwa tumaini lao la mwisho.

Inafaa kutafakari namna ya aya zilivyoshuka pale Ghadir Khum. Kwanza ilisemwa “**Ewe Mjumbe fikisha ujumbe**,” kama ukishindwa kufikisha basi utakuwa hukifikisha chochote, kila kitu kilichofanywa kabla kitakuwa bure, hakina maana.

Kisha wakati ujumbe ulipofikishwa, aya hii iliteremshwa:

الْيَوْمَ يَبْسَ أَلَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ دِينِكُمْ

“...Leo waliokufuru wamekata tamaa katika dini yenu...”  
(Qur'an. 5:3)

Leo ni siku ya kukata tamaa kwa makafiri na maadui wa Uislamu. Kwa nini maadui leo wamekata tamaa? Kwa kweli wakati wa

safari hii, Mtume (saww) alisema kwamba hii ni Hajja yangu ya mwisho na sitakuwepo katika Hijja ijayo kwani huu ni mwaka wa mwisho wa uhai wangu. Sasa kipi kilichowafanya maadui wakate tamaa, walipaswa kufurahi kwani walikuwa wanasubiri wakati huu ambapo Mtume (saww) anaondoka katika ulimwengu huu. Qur’ani Tukufu inasema kwamba huko nyuma walikuwa wakishindwa lakini kamwe hawakukata tamaa, lakini leo wamekata tamaa kwamba dini hii haiwezi kuangamizwa. Kadhiya hii, tangazo hili la “Wilaya” liliwafanya wakate tamaa ya kuivunja dini hii. Nukta kubwa leo imedhihirishwa kwao. Kwamba Allah *Azza wa Jallah* aliisimamisha dini na akamfanya Mtume (saww) kama Mlinzi wake, mwenezaji na mwendeshaji, lakini hakuifanya dini kuwa yenye kutegemea juu ya haiba ya Mtukufu Mtume (saww). Lakini Allah *Azza wa Jallah* alifanya mhimili wa dini hii kuwa ni Mfumo, na leo dini hii ime-upata mfumo huo. Na madhehebu au itikadi ambayo hupata mfumo haiwezi kutoweka, haiwezi kuvunjwa. Ile ambayo haina ngome imara inayoizunguka, haina mipaka imara inayoizunguka inaweza kuteketezwa. Lakini leo ngome imara imejengwa kuuzunguka Uislamu, na ngome hiyo ni “Wilaya”.

Hivyo, pia husemwa katika hadithi kwamba:

وَلَا يُؤْتِي اللَّهُ عَزَّ ذِي عَذَابٍ مَنْ فَرَّ هُنَّ أَنْجَانٌ

**“Wilaya ya Ali Ibn Abu Talib ni ngome yangu, na mtu aingiaye katika ngome hii atasalimika kutokana na adhabu yangu.”**

(Uyuni Akhbar Ridha)

*Wilaya ni ngome ya Allah *Azza wa Jallah* iliyofanywa kwa ajili ya Uislamu. Jambo hili lazima liangaliwe kwamba hata maadui wa-*

natambua jambo lilolengwa kwa ajili ya nguvu ya dini, kwa hiyo, walikata tamaa na wakawa wamevunjika moyo kwamba sasa hawawezi kuivunja dini hii. Sasa, dini hii haiwezi kukoma kwa sababu imepata msingi imara.

Baada ya kueleza kwamba leo makafiri wamekata tamaa, kisha ikashuka aya isemayo:

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمْ  
آلَّا إِسْلَامَ دِينًا

“...Leo nimewakamilishia dini yenu na kuwatimizia neema yangu na nimewapendelea Uislamu kuwa dini...” (al-Maidah; 5:3)

Mambo mawili yalijitokeza; moja maadui walikata tamaa na pili dini ilikamilishwa. Kile ambacho dini ilihitaji ilikipata na sasa haiwezi kutoweka. Ni muhimu hapa kuelewa kwamba kwa maandalizi yote haya Allah *Azza wa Jallah* aliihifadhi dini, lakini kwa wafuasi wa dini njia ni tofauti. Sio kwamba wafuasi wanapaswa kufikiria kwamba wao pia sasa wamehifadhika kwa vile dini iko salama. Wafuasi wa dini wanahitaji kufanya mahesabu yao wenyewe na lazima waingie ndani ya ngome ili kuwa salama. Wanahitaji kutembea ndani ya ngome hii na sio kufikiri tu kwamba kwa sababu Allah *Azza wa Jallah* ametangaza kwamba dini imekamilishwa na kuwa salama, wafuasi nao pia wafikirie kwamba wamesalimika na kukamilishwa. Wafuasi wanahitaji kukubali na kuja chini ya mfumo huu wa “Wilaya”, wanahitajika kuutekeleza mfumo huu katika maisha na jamii yao, na lazima waishi maisha yao chini ya mfumo huu. Kama wakifanya hivi basi maadui wa Uislamu watavunjwa moyo

na wafuasi na kukata tamaa kutokana nao kwa namna walivyokata tamaa kutokana na Uislamu.

Katika siku ya Ghadir maadui walikata tamaa kutokana na dini lakini hawakukata tamaa kutokana na wafuasi wa dini. Kwanza mbinu yao ilikuwa ni kuwaweka mbali watu na dini lakini sasa wamebadilisha mbinu zao, sasa mbinu yao ni kuwaweka mbali wafuasi na “*Wilaya*”, mbali na ngome hii na mbali na msingi huu.

Hii ilikuwa mbinu ya pili ya maadui ili kuwaweka watu mbali na ngome hii. Hata kama dini ikibakia bila “*Wilaya*” dini hiyo haionyeshi tofauti yoyote, iwapo ipo au la. Matendo yote ya ibada za dini, ibada bila “*Wilaya*” hakufanyi tofauti. Hata kama Hijja inatekelezwa bila “*Wilaya*” haitaleta tofauti yoyote. Lakini kama vitu hivi vinafanywa chini ya mwamvuli wa “*Wilaya*” basi vyenyewe vitakuwa na athari zao hususan juu ya maadui wa Uislamu. Kwa hiyo maadui walibadilisha shabaha yao na kuelekea kwenye “*Wilaya*” na kufanya juhud zao zote ili kuwaweka watu mbali na “*Wilaya*.”

Imamu Razi ni mwanachuoni mashuhuri wa Sunni ambaye pia ameandika katika tafsiri yake kwamba Allah awalaani Bani Umayyah ambao wameleweweka watu mbali na “*Wilaya*.” Huu ulikuwa ni udhalimu wao mkubwa na uchupaji wa mipaka kwamba walikuwa wakiaweweka watu mbali na “*Wilaya*.” Imamu Razi alikuwa akijulikana kwa jina la *Kiongozi wa Wenye shaka*, ambaye alikuwa akiangalia kila kitu kwa shaka, hata aliweza kuona kosa hili la Bani Umayyah kwamba walikuwa wakiaweweka watu mbali na “*Wilaya*”. Na hili limekuwa katika zama zote, ni urithi wa Bani Umayyah kuwaweka watu mbali na “*Wilaya*.”

## NI NINI ILIYOKUWA HOFU YA MTUME (SAWW)?

Tatizo moja katika mlango wa “Wilaya” lilikuwepo kwa wale wenye kuhutubiwa wenyewe, na hili lilikuwa ndio tatizo halisi la “Wilaya”. Hii ndio sababu Qur’ani ilisema kwamba kama hukufanya hivi, basi itakuwa hakuna kilichofanyika. Jambo moja ambalo lilikuwepo katika moyo ulioongoka wa Mtukufu Mtume (saww) pia lilitambulishwa na Qur’ani Tukufu. Katika aya hiyo hiyo Allah *Azza wa Jallah* anasema kwamba:

فَلَا تَخْشُوْهُمْ وَآخْشُونِ<sup>٤</sup>

“...basi msiwaogope na mniogope mimi...” (Qur'an. 5:3)

Allah *Azza wa Jallah* anamwambia Mtume (saww) kwamba usiwaogope watu, bali niogope Mimi tu. Hapa tena lazima tusimame na kutafakari kwamba wasikilizaji ambao mionganini mwao Mtume (saww) anawatolea tangazo hili sio maadui, wote ni watu wa dini. Na pia sio watu wa dini wa kawaida, ni wafuasi wa dini imara sana na wenyewe nguvu. Wote walikuwepo pale kwa ajili ya Hijja. Hijja sio kitendo kinachofanywa na kila Mwislamu wa kawaida; hufanywa na wale tu ambao wana mahusiano makini kuhusu dini, kwa sababu Hijja huhitaji pesa nyingi, muda na juhudini. Wale ambao ni wana-dini wa kawaida hawatumii pesa katika Hijja, hupendelea kufanya mambo mengine katika jina la dini.

Siku hizi inazungumzwa katika magazeti na wengi mionganini mwetu vilevile husema kwamba ni bora kujenga hospitali, bara-

bara na madaraja kuliko kupoteza pesa katika Hijj na Maombolezo. Kwa ukweli wala hawafanyi hivyo. Hatuwaoni wale ambao hawasafiri kwa ajili ya Hijja wakitumia pesa zao katika kujenga barabara na madaraja, kuna watu wachache tu ambao huandaa programu za Maombolezo na kutumia pesa kwa ajili hiyo, wengi hawafanyi hivyo, wanashiriki tu, lakini kisha pia hawatumii pesa katika mambو mengine. Sio lazima kwamba kujenga barabara na mahospitali lazima tuache Maombolezo. Kama unataka kujenga madaraja, kukarabati barabara, basi fanya hivyo, lakini usifanye hivyo kwa kuzuia Maombolezo. Kuna watu kama hao ambao hufanya kazi ya kunong'oneza kama ile ya "Khannas" (jina lililotumika kwa Shetani katika Qur'ani Tukufu ambaye hupoteza waumini kwa minong'ono ya kiovu). Leo kazi hii ya "Khannas" inafanywa na vyombo vya habari, ambavyo hupenyeza minong'ono ya uovu mionganoni mwa watu.

Kama ilivyotajwa kwamba watu wa kawaendi hawaendi Hijja, wale tu ambao ni makini sana katika kutekeleza wajibu nyingine zote za kidini ndio hutekeleza Hijja. Watu wengi wanaosafiri kwa ajili ya Hijja ni wale ambao hujaribu kutokufanya dhambi yoyote, ingawa kuna uwezekano wa watu wachache ambao pia hufanya Hijja na kisha hushughulika na riba vilevile. Wakati huo walikuwa watu wazuri kweli ambao walikuwa pamoja na Mtume (saww) katika Hijja. Na pia hali haikuwa kwamba walikuwa wanatasafiri kwenda Hijja, kwa kweli walikuwa wanarudi kutoka Hijja, baada ya kufanya toba makini. Na wale ambao wametubia *Allah Aza wa Jallah* husamehe dhambi zao na moja ya adabu za Ka'aba Tukufu ni kwamba mtu lazima aombe kusamehewa pale. Na kwa vile *Allah Aza wa Jallah* huwapenda wale ambao hutubia na kuomba msamaha, hivyo lazima tulifanye hilo kuwa ni mazoea kwa ajili ya kuomba kusamehewa dhambi zetu hata kama tuko nyumbani.

Mahujaji hawa wanarudi kutoka Hijja, baada ya kusamehewa dhambi zao walikusanyika katika uwanda wa Ghadir Khum. Imetajwa katika hadithi kwamba wakati wa safari yote hii ya kwenda Hijja na kurudi, Mtukufu Mtume (saww) alitoa hotuba nne. Mtume (saww) alikwisha toa hotuba tatu kubwa kabla ya hotuba hii ya Ghadir; moja ilikuwa Khayf, ya pili Mina na ya tatu ilikuwa Arafah. Hivyo alikwishaweka mazingira mazuri, kuwaandaa kwa ajili ya suala hili na baada ya kufanya maandalizi yote haya alitangaza kiini cha ujumbe. Nukta hii kubwa na kiini hiki cha ujumbe huu ultolewa Ghadir Khum, sehemu moja karibu na Juhfa. Ni muhimu kusisitiza juu ya ukweli huu kwamba Mtume (saww) alitoa ujumbe huu miongoni mwa Umma wake, kwamba pia haukuwa Umma wa kawaida, ulikuwa Umma wa wachamungu na watiifu ambaao walikuwa wanatekeleza Hijja chini ya uongozi na maelekezo ya Mtukufu Mtume (saww). Ni wale ambaao walitayarishwa kwenda popote walipoambwa kwenda na Mtume (saww). Mtume (saww) alizoea kuwatuma kwenye vita na walikwenda. Wengi wa waliokuwepo hapa Ghadir Khum ni wale ambaao wamepigana vita na kutoa huduma zao kubwa kwa ajili ya Uislamu hapo kabla.

Wengi wa masahaba wa Mtume kwa kweli walikuwa watu mashuhuri sana wenyе huduma kubwa sana na kwa moyo mmoja walikuwa tayari kutoa muhangaa maisha yao kwa ajili ya Mtukufu Mtume (saww) na wengi walishafanya hivyo kabla. Walihatarisha maisha yao katika vita vya Badr na Uhud, na walikuwepo Ghadir. Lakini ugumu wa “Wilaya” ni wa aina ya tofauti. Ugumu wa “Wilaya” ni tofauti, hauhusiani na watu kuwa wachamungu au la. Hata kama watu ni wanadini au hata kama wakiwa sio wanadini ugumu bado upo. Hii ndio sababu leo Mtume alikuwa na hofu juu ya wachamungu waliokuwepo mbele yake. Alikuwa hawaogopi washirikina; hofu yake pale kwenye uwanda wa Ghadir Khum

ilikuwa kutoka kwenye hadhara ya wachamungu waliokuwa pale mbele yake.

Hofu hiyo ilikuwa ni hofu gani katika moyo wa Mjumbe wa Allah (saww) mpaka *Allah Azza wa Jallah* akawa asema kumwambia kwamba ‘usishaogope hao bali niogope Mimi, na Allah atakulinda.’ Hofu hii vilevile imejadiliwa huko nyuma na Qur’ani Tukufu katika suala la Mtume mwingine. Imezungumzwa katika mijadala inayohusiana na Mtume Musa (as). Wakati wachawi walipokuwa wametupa kamba zao ziligeuka kuwa nyoka na kisha Musa (as) akatupa ya kwake fimbo, nayo pia iligeuka kuwa nyoka mkubwa, na Musa (as) akapatwa na hofu pale.

Hii ni nukta ya kutafakari ili kuelewa ni aina gani hii ya hofu. Umati uliokuwepo pale walikuwa ni wanawake wa kawaida na watoto kutoka sokoni, hawakuwa na hofu ya kamba kugeuka nyoka, lakini Musa (as) alikuwa na hofu. Walikuwa wanatambua kwamba wachawi hawa si chochote bali ni wachezaji tu wa jukwaani na kwa hiyo walikuwa hawana hofu. Si watoto, Firauni wala wachawi na hakuna mtu mwingine yejote aliyekuwa na hofu ya mandhari zile, lakini Mtume wa Allah (saww) aliogopa onyesho hili. Kwamba Musa (as) pia hakuwa Mtume wa kawaida, alikuwa Mtume shujaa na jasiri, mtu mchangamfu sana. Hapa hata mtu wa kawaida anaweza kufikiri kwamba hofu hii haikuwa hofu juu ya nyoka, hofu hii ilikuwa ni kutokana na jambo jingine kabisa.

Imo kwenye *Nahjul Balaghah*; Imamu Ali (as) ametoa ufanuzi wa kadhia hii. Musa (as) hakuwa na hofu ya maisha yake kwamba nyoka wale watamuumu; hofu hii haikuwa katika moyo wa Musa. Hofu hii ilikuwa ni hofu ile ile ambayo kila kiongozi wa kimungu anayo katika moyo wake. Hofu hii ya Musa ilikuwa; “wapinzani wangu ni hawa wachawi, ambao wanaonesha mazingahombwe yao na mimi ninawasilisha muujiza,” na wale ambao watachukua ua-

muzi na kutofautisha kati ya Musa na wachawi ni watu wa kawaida. Kama kiwango chao cha akili hakitanyanyuliwa basi hawatakuwa na uwezo wa kutofautisha kati ya mazingahombwe na muujiza. Matokeo yake yatakuwa kwamba wanaweza pia wakafikiria mazingahombwe ya wachawi kama ni muujiza, au muujiza wangu kama ni mazingahombwe. Hivyo amma wanaweza pia wakanifikiria mimi kama mchawi au wakawachukulia wachawi wote kama mitume.

Amirul Muminin (as) anasema katika *Nahjul Balagha*, khutba Na. 4 kwamba: “Musa hakuwa na hofu kwa ajili ya nafsi yake mwenyewe. Isipokuwa alitambua ujuzi wa wajinga na njia ya upotovu.” Hii ina maana kwamba isije ikatokea kwamba kwa ajili ya kiwango chao cha chini cha uelewa na akili, ujinga ukaanza kushamiri na upotovu ukaanza kutawala.

Mtukufu Mtume (saww) pia alikuwa na hofu kama hiyo kwamba nimeona uzoefu wa magumu hayo katika uelewa wa masuala ya kawaida ya dini, na leo ninawasilisha mhimili, silika na moyo wa dini. Leo ninawasilisha nukta ya ukamilishaji wa dini, ninawakilisha kile ambacho kitawakatisha tamaa maadui. Hofu ambayo Mtume (saww) alikuwa nayo ilikuwa ni hii kwamba leo ninawasilisha msingi muhimu sana wa dini ambao unawafanya maadui wachanganyikiwe, lakini vipi kama watu hawa watatafsiri vibaya kile ambacho ninakiwasilisha na kama wataichukulia “*Wilaya*” hii kama kitu kingine, basi nini yatakuwa matokeo yake.

Hivi pia ndivyo ilivyotokea, hofu ya Mtukufu Mtume (saww) ikawa kweli. Mjumbe aliwasilisha kwao Mfumo wa “*Wilaya*”, walisisikia tangazo hilo. Lakini je walielewa kile kilichokusudiwa kueleweka? Je, walielewa kile ambacho kilifikishwa kwao na Mtukufu Mtume (saww)? Je, kimetokea kile ambacho *Allah Azza wa Jallah* na Mjumbe Wake walichotaka kitokee? Kilichotokea kilikuwa ni kitu tofauti.

## **WILAYA – ILIGEUKA KUWA SIFA**

Kila mtu alijitokeza mbele baada ya tangazo hili na kusema: “*Bakhin, Bakhin*”, na hii inasimuliwa katika historia. Hata mtu mmoja kwa jina Hissan ibn Thabit, ambaye alikuwa mshairi aliandika shairi la kwanza kusifia “*Wilaya*” na akapata sifa kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww). Hema lilitengenezwa na Mtukufu Mtume (saww) aliwataka wote kutoa kiapo cha utii na kuonesha ahadi zao kwa Amirul Muminiin (as). Kila mtu alikwenda kwenye hema na kusema “*Bakhin, Bakhin*”. Kwa ujumla tunalitafsiri hili kama Baraka, ambapo sio kweli. Baraka pia ni neno la Kiarabu, kama Qur’ani inavyosema kwamba tuliteremsha Qur’ani katika usiku uliobarikiwa, au tunaweza kuona kwamba *Allah Azza wa Jallah* anasema kwa ajili Yake Mwenyewe: “Baraka kwa Allah (*Fa Tabarakallaha*) kwa aji-li ya uumbaji bora kama huo.” Hata Waarabu wakimpongeza mtu husema: “*Fabarakallahu.*” Mubaraka haimaanishi “*Bakhin, Bakhin*”. Kwa Kifursi “*Bakhin, Bakhin*” maana yake ni “*Baah, Baah*” na kwa Urdu ina maana ya “*Wah, Wah*”, na kwa Kiingereza inaweza kutajwa kama “*wow*” au hata kushangilia kwa kupiga makofi “*clap-pings*.” (Kwa Kiswahili inatajwa kama “Wawaa, Hongera”).

Wakati tunapopenda kitu tunasema “*Wow*” kwa Kiingereza au “*Wah, Wah*” kwa kifursi au kupiga makofi. Hata hivyo nani mwinge-ine awezaye kuwa mzoefu zaidi na “*Wah, Wah*” kuliko jumuiya ya Mashia wazungumzaji wa Urdu?

Hii ilikuwa ndio hofu ya Mtukufu Mtume (saww). Kwa upande mmoja “*Wilaya*” ni kituo, kiini, mhimili na mfumo wa dini na waliohutubiwa pia ni watu wazuri, ni wachamungu, lakini suala hili sio rahisi kiasi hicho. Ujumbe unaowasilishwa sio kitu cha kawaida. Mtume (saww) alikuwa na wasiwasi kwamba kama nikiwasilisha ujumbe huu na wasielewe dhati ya ujumbe huu na wakauchukua

ujumbe huu kwa maneno tu ya kufurahia tu ya “Hongera,” kupiga makofi au “Wah, Wah,” na “wow,” kisha nini kitatokea? Basi “Wilaya” inaweza kuishia kwenye shangwe tu, “Hongera,” kupiga makofi au “Wah, Wah,” na “wow,” daima, na mpaka Siku ya Mwisho itakuwa ni sifa tu ndizo zitakazokuwa zinatolewa kwenye “Wilaya” na hatua ya kweli ya utekelezaji wa “Wilaya” kama Mfumo haitachukuliwa.

Kila mtu hapa alifanya “*Bakhin, Bakhin*” na kuondoka. Tukio hili lilitokea mwezi 18 Dhil Hajj, mwaka wa 10 Hijiriyah, na kifo cha Mtume kilitokea mwezi 28 Safar mwaka wa 11 Hijiriyah, na baada ya miezi miwili na siku kumi hali ikabadilika kabisa. Baada ya siku hizi sabini, Bibi Fatima (as) alipiga hodi katika mlango wa kila mmoja. Fatima (as) hakuwataka wachomoe panga zao, aliwataka tu watoke nje na kutoa maelezo, wasimulie tu hadithi ya Ghadir au wathibitishe tu kwamba walikuwepo pale Ghadir, lakini hakuna aliyetoka nje. Leo baada ya miaka 1400 tunapowataka watu wazungumze kuhusu “Wilaya” hawazungumzi. “Wilaya” ni mlango unaosikitisha wa Uislamu ambao baada ya miezi miwili na siku kumi watu walijibu kwamba kumbukumbu zao ni dhaifu na hawakumbuki chochote. Hii ndio hofu iliyokuwa katika moyo wa Mtume (saww). Hapa ndipo ambapo tunaweza kushuhudia ukandamizaji juu ya dini, uonevu juu ya “Walii” na dhulma juu ya “Wilaya”. Amirul Muminin (as) ndiye yule mtu aliyekandamizwa ambapo Bibi Fatima (as) alisahau maumivu yake mwenyewe baada ya kushuhudia hali ya kudhulumiwa kwa Ali (as). Leo watu wanauliza ni kwa nini Amirul Muminin (as) hakuchomoa upanga wake kupigania haki yake? Ali (as) alisimama lakini Bibi Fatima (as) alimkataza na akasema kwamba, Ali leo mimi ndio mtetezi wa “Wilaya”, leo mimi ndio mchokozaji wa “Wilaya”, leo nataka kwenda na kuchukua maelezo ya “Wilaya” kutoka kwa Umma. Alipiga hodi kila mlango lakini hakuna aliyetoka.

Mtu mzima mmoja ameandika kitabu kwa jina la “*Summal Ajab*” (Ajabu ya kushangaza) ambacho ni kijitabu kidogo. Katika kitabu hiki mwandishi ameandika baadhi ya matukio ya kushangaza ya historia ya Uislamu na akaonesha kushangazwa kwake. Anasema kwamba ninashangaa kuona kwamba katika siku moja Bibi huyu anapiga hodi kwenye milango ya watu wa Madina kutoka nje kushuhudia lakini hakuna aliyetoka nje, na kisha inakuja siku nyingine watu wanaitwa kuja kuchoma moto mlango wa Bibi Fatima (as), kila mtu alitoka nje. Kwa muda huu mfupi ni kitu gani kilitokea kwa watu, je, wote walitowekea wapi baada ya tukio la Ghadir? hii ndio iliyokuwa hofu ya Mtukufu Mtume (saww) ambayo ilitokea kuwa kweli baadaye.

## **UMMA WAJITENGA MBALI NA *WILAYA* KAMA MFUMO**

Hawakuweza kuelewa ile dhati ya “Wilaya” na wakati walipotakiwa kueleza maana yake, walitoa maelezo mepesi sana kama vile “Urafiki” au “Mapenzi.” Je, Mtume (saww) baada ya maandalizi yote hayo na ushukaji wa aya hizo, alikuwa anatangaza urafiki au mapenzi? Huu ndio wasiwasi uliomshughulisha Mtume (saww) kwamba Umma unaweza ukaishiliza maana ya “Wilaya” mpaka kwenye urafiki na mapenzi tu, hawatasonga mbele katika kuusimamisha kama mfumo.

“Wilaya” ni mfumo wa kimungu kwa ajili ya mwongozo wa Wanadamu. Ni mfumo bora sana ambao una khususia (kazi maalum) zake wenyewe. Sina nafasi ya kuzitaja taaluma za mfumo huu hapa na kuulinganisha na mifumo mingine ya utawala. Hili lilikuwa ni tangazo la mfumo wa utawala wa kimungu, lakini Umma hawakuubali katika njia hii, waliutafsiri kimakosa. Hawakwenda ka-

tika njia ile ambayo Mjumbe (saww) alitaka waichukue. Hatua ya kwanza waliyochukua ilikuwa ni kujitenga na “*Walii*” huyo. Wacha ajitokeze ye yeyote kutokana na “*Answar*” (Wasaidizi wa Madina) au “*Muhajirin*” (Wahamiaji kutoka Makka) kuwa kiongozi, lakini Walii wa kweli asijitokeze.

*Wilaya* haukuwa mfumo uliofanywa na *Allah Azza wa Jallah* kwa ajili ya siku moja au mbili, ulikuwa ni mfumo wa utawala kwa ajili ya Umma baada ya kufariki Mtukufu Mtume (saww) mpaka Siku ya Hukumu. Mfumo huu pia ulikuwepo kabla ya Ghadir na upo palepale daima. Vilevile madhumuni ya kadhia ya Ashura yalikuwa ni kuurudisha Umma kwenye mhimili wa “*Wilaya*” kwa vile watu walijitenga mbali na Ghadir. Wakati watu wanajitenga mbali na Ghadir, Ashura inajitokeza. Vilevile moyo wa Ashura ni “*Wilaya*.<sup>1</sup>” Wakati watu wanapojitenga wenyewe mbali na “*Wilaya*” walijitumbukiza kwenye Ukhilifa (*Khilafat*), na kutoka kwenye “Ukhilifa” mfumo ulibadilika kuwa Ufalme (*Mulukiyat*), na kutoka kwenye Ufalme ulibadilka kuwa Uyazidi (Yazidiat). Viwango hivi vitatu vya uangukaji chini vilitokea katika jamii baada ya kujitenga mbali na “*Wilaya*,” na Uyazidi (*Yazidiat*) ulikuwa msiba. Hapa ndipo Ashura ilipokuja na kuwaambia watu kwamba ukombozi wenu upo tu kwenye “*Wilaya*.<sup>2</sup>”

Mfumo wa “*Wilaya*” upo mpaka Siku ya Hukumu. Hauwezi kusimamishwa kwa kifo cha Mtukufu Mtume (saww) wala kusimamishwa kwa ghaibu ya Maasum (a.t.f.s). Ilikuwa ni uamuza wa kimungu kwamba Mjumbe (saww) lazima asariki. Lazima aende kwenye ghaibu ya kudumu, lakini “*Wilaya*” ilikuwa hai, ipo na mfumo huu ulikuwepo mionganoni mwa Umma.

Kama Maasum akienda kwenye hali ya ghaibu kwa muda maalumu, bado mfumo wa “*Wilaya*” unaendelea kuwepo, na hata kama Maasum akienda nyuma ya mapazia ya ghaibu kwa muda usio na

kikomo basi pia mfumo wa “*Wilaya*” bado unadumu. Hairuhusiwi sisi kugeuza nyuso zetu mbali na *Wilaya* imma kwa sababu ya kifo cha Mtume (saww) wala kutokana na ghaibu ya Maasum.

## ***WILAYA YA AMBAYE SIO MA’ASUM***

Kuna watu ambao wanachukua nafasi ya “*Khannas*” (Mashetani wanaonong’oneza) na kusababisha mashaka kwenye akili za watu. Mnong’ono mmoja wa kishetani ambao walitengeneza ulikuwa wakati wa kifo cha Mtukufu Mtume (saww) kwa kuwaweka watu mbali na “Walii” Maasum ambaye alikuwepo. Na kitendo kingine cha kishetani kilianza dhidi ya yule asiyekuwa Maasum ambaye alikuja wakati wa ghaiba ya “Walii” Maasum. Haya ndiyo ambayo yalimshughulisha Mtukufu Mtume (saww) kuhusu “*Khannas*” ambaye atakuja kuwepo ili kuleta mashaka mionganoni mwa watu dhidi ya “*Wilaya*.”

Swali la kwanza ambalo tutawasilisha kwa hawa mashetani mionganoni mwetu linapaswa liwe: Ni vipi Mtukufu Mtume (saww) alivyokuwa “Walii?” Ni vipi Amirul Muminin alivyokuwa “Walii?” Hakuna anayekuwa “Walii” kwa kuchaguliwa na watu, wala hakuna mtu anayepoteza hadhi ya *Wilaya* kwa kuvuliwa na watu. “Walii” anatengenezwa na Allah Azza wa Jallah na anatoka kwa Allah Azza wa Jallah, hata kama ulimwengu wote ukimkubali ni “Walii” na hata kama asikubaliwe na mtu yejote bado yeye ni “Walii.” Kama watu wakimkubali kama “Walii” ni kwa faida yao wenywewe. Ni kama hata ulimwengu wote wakimkubali Allah Azza wa Jallah au wasimkubali kama “Walii” haileti tofauti yoyote. “*Wilaya*” ya Allah haina masharti ya kukubaliwa au kukataliwa na viumbi.

Wakati kipindi cha ghaiba kilipoanza na punde “Wilaya” ya asiyé Maasum ilipotajwa, baadhi ya watu wakaanza kuweka minong’ono ya kishetani. Inapaswa ifahamike kwamba “Wilaya” (Ulinzi) katika muundo wa ukamilifu wake ni wa Allah Azza wa Jallah, lakini kutoka kwa Allah ikaja kwa Mitume (as) na Maasumin (as). Lakini kuna baadhi ya watu wakati huo ambao walikataa hata kumkubali Maasum kama “Walii” wao. Kaulimbiu ambayo Khawarij waliileta ilikuwa **“La Hukm Illa Lillah”**, hii maana yake ni kwamba **“Hakuna hukumu nyingine kuliko ya Allah”**. Ili kuthibitisha hoja yao hii waliwasilisha aya ya Qur’ani Tukufu ambayo inasema:

إِنَّ الْحُكْمَ إِلَّا لِلَّهِ

“...Hapana hukumu isipokuwa ya Allah tu...” (Qur. 12:40)

Waliitumia hoja hii kwamba Qur’ani imesema kwamba hakuna mtu yejote anayeweza kuhukumu kuliko Allah, hivyo hawatakubali mamlaka, uongozi au utawala wa mtu yejote. Amirul Muminin (as) alisema kuhusu hili:

كَلِمَةُ الْحَقِّ يُرَادُ بِهَا بَاطِلٌ

“Maneno ni ya kweli lakini makusudio ni ya uwongo.”

Nini walichokuwa wakikifanya na aya ya Qur’ani? Wanaikataa “Wilaya” ya “Walii” yule ambaye kwamba ushahidi wake ni Qur’ani yenye. Baada ya kusoma aya ya Qur’ani ambayo kwa uwazi imesema kwamba mtu ambaye anatoa sadaka katika hali ya Rukuu

ni “Walii” wenu, sasa wanatumia aya nyingine ya Qur’ani kukataa “Wilaya” ya “Walii” huyu. Qur’ani inatoa ushahidi kwamba baada ya Mjumbe wa Allah Aza wa Jallah (saww) “Wilaya” ni ya Maimamu Maasumin (as).

Amirul Muminin (as) alikuwepo Kufa kama Mtawala na ampeleka Malik Ashtar kama mwakilishi wake huko Misr. Malik Ashtar ni “Walii” mteule wa Amirul Muminin (as) mahususi kwa ajili ya eneo moja la kijografia. Sasa, kama watu wa Misri wanazungumza katika lugha ile ile kama ya wale wa leo, kwa vile Malik Ashtar sio Maasum hatuko tayari kumkubali yeye kama “Walii.” Mtu huyu asiyeh Maasum inajuzu kumfuata kwa vile ameteuliwa na Maasum. Kama baadhi ya “Khannas” huko Misri wangesimama na kusema kwamba Malik Ashtar sio Maasum na kwa hiyo hatutasikiliza maelekezo yake, basi Amirul Muminin (as) angesema nini?

Amirul Muminin (as) kwa uwazi anasema katika *Nahjul Balaghah* kwamba mtu ambaye anakataa utii kwa Malik Ashtar anakataa utii kwangu, na mtu ambaye si mtii kwangu si mtii kwa Allah Azza wa Jallah. Kama Maliki anaweza kuwa “Walii” kwa uteuzi wa Maasum basi hakuna tofauti yoyote iwapo anateuliwa kama “Walii” kwa ajili ya eneo au kwa ajili ya zama mahususi. Kama kuna kipindi cha ghaiba na akawepo Malik Ashtar kwa ajili ya zama hii, ni kwa ajili ya hili imetakiwa kumfuata Malik Ashtar, sasa kama baadhi ya “Khannas” wakija na kusema kwamba yeye sio maasum basi “Walii” Maasum angesema kwamba anahusiana na mimi na mtu ambaye anamkataa huyo ananikataa mimi.

Kuna hadithi sahihi zinazopatikana juu ya “Wilaya” na uongozi wakati wa kipindi cha ghaiba kwamba (*Wilaya*) ni ya Faqih (wanachuo wanasheria). Kuna hadithi zinazopatikana juu ya hili kutoka kwa Imam Hujjah (a.t.f.s) mwenyewe. Badala ya kwenda kwenye hadithi, nitasimulia kisa kimoja kuthibitisha hoja hii kimantiki. Sasa,

usije ukaamua kitu chochote hasi (kuhusiana na masuala ya madhe-hebu) au kuchukua kisa hiki mwelekeo tofauti.

Mwanachuoni mmoja wa Shia alikuwa akisafiri kwa njia ya barabara. Alipita kwenye mji mmoja mdogo na kwa vile ilikuwa usiku alilazimika kuchukua hifadhi pale. Mji ule ulikuwa na Msikiti wa Sunni na mwanachuoni yule aliwaomba waangalizi na wanachuoni wa pale ili wamruhusu apitishe usiku ule Msikitini pale. Walisema watamruhusu kukaa humo kwa masharti kwamba mwanachuoni huyo wa Shia aahidi kwamba hatazungumza masuala ya mabishano kati ya Shia na Sunni. Mwanachuoni yule wa Shia akawa hana jinsi ila kukubali kuahidi na akae pale usiku ule. Walichukua ahadi kutoka kwa mwanachuo yule wa Shia, lakin i wao wenyewe hawakujifunga na ahadi ya chochote kile. Hata hivyo walimpa mwanachuoni yule wa Shia chakula na wakawa na mazungumzo kidogo naye, baada ya hayo walimuuliza swalii la kuhusu kwamba ni nini maoni yake baada ya Khalifa wa kwanza. Mwanachuoni yule wa Shia alikuwa katika wakati mgumu kwa vile aliahidi kutozungumza kitu chochote cha ubishani. Baada ya kufikiri kwa muda kidogo, alijibu kwamba kwa aonavyo yeye Khalifa wa kwanza alikuwa na akili zaidi kuliko Mtume (saww). Wote walishikwa na mshangao, kwa sababu kila mtu anamheshimu Mtukufu Mtume (saww) na kumchukulia kama kiumbe bora wa viumbe wote, na kwa hakika Sunni wanayo heshima ya hali ya juu sana kuhusiana na Mtukufu Mtume (saww). Walishangazwa mnoo na kauli hii na wakafikiria kwamba kuna sababu nyuma ya hili ambapo walimtaka mwanachuoni yule wa Shia kufafanua. Mwanachuoni wa Shia aliwaliza kwamba wakati Khalifa wa kwanza alipokaribia kuondoka ulimwenguni hapa iwapo alifanya maandalizi kwa ajili ya mrithi wake na uongozi kwa ajili ya Umma au aliondoka bila kufanya maandalizi yoyote? Walijibu kwamba bila

ya shaka alifanya maandalizi na akachangua mrithi wake na hakucha Umma peke yake. Mwanachuoni wa Shia aliendelea kuwa uliza iwapo ni kiongozi yule ambaye anafanya maandalizi kwa ajili ya Umma wake wakati akiwa hayupo ndiye mwenye akili zaidi au kiongozi yule ambaye hafanyi maandalizi yoyote wakati anaondoka ulimwenguni hapa? Mara moja walitambua hoja ya mantiki ambayo mwanachuoni yule wa Shia aliyokuwa akiielekea, na kwa hiyo walisimamisha mjadala ule kwa kusema wote tuache kuzungumza kuhusu masuala yenyе ubishani.

Unaweza ukafikiri wewe mwenyewe kwamba hiki ni kitu cha akili ya kawaida. Unaweza hata kumuuliza mtoto au mtu asiyе mchamungu, hili wala sio suala la Sunni au Shia. Ni suala la Umma wote kwamba kiongozi wao anakaribia kuondoka ulimwenguni hapa na hafanyi maandalizi yoyote kwa ajili ya wakati wa kutokuwepo kwake na anauacha Umma peke yake? Hii ndio hoja ya mjadala ambayo tunaitoa kuthhibitisha uteuzi wa Amirul Muminiн (as) kama “Walii,” hivyo kama Mtukufu Mtume (saww) hawezi kuondoka ulimwenguni hapa kama hivi bila kuteua kiongozi baada yake, basi vipi itawezekana kwa mtoto wa Mtume (as) anakwenda kwenye ghaiba na hii pia ni kwa kipindi kisichoainishwa kwa kuuacha Umma peke yake wenyewe bila ya mlinzi.

Kwa vile hili haliwezekani, hivyo ye ye Mahdi (a.t.f.s) alifanya maandalizi na maandalizi hayo yalikuwa ni ya “Wilaya,” lakini “Wilaya” ya asiyeko Maasum. Ni ukweli kwamba ni “Walii” tu ndiye anayeweza kumfanya mtu mwingine kuwa “Walii.” Allah Aza wa Jallah ni “Walii” na aliwfanya wengine kuwa “Mawalii” (Wal-inzi). Kama asemavyo Allah Aza wa Jallah:

إِنَّمَا وَلِيْكُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا أَلَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ  
 الْزَّكُوْةَ وَهُمْ رَاكِعُونَ

**“Hakika walii wenu hasa ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na  
wale walioamini ambao husimamisha Swala na hutoa Zaka wakiwa  
wamerukui.” (Surat al-Maidah; 5:55)**

Wakati Allah Azza wa Jallah anapomfanya mtu kuwa “Walii,” Yeye anasema kwamba ingawa ni Mjumbe wangu lakini ni “Walii” wenu na yule anayetoa sadaka akiwa katika hali ya rukuu vilevile ni “Walii” wenu. Wakati “Walii” akiondoka ulimwenguni hapa kwa kifo, basi huacha “Walii” mwengine nyuma yake, halikadhalika wakati “Walii” akienda kwenye kipindi cha ghaiba basi yeye vilevile huacha “Walii” nyuma yake. Hii ni kwa sababu “Wilaya” ni mfumo wa utawala na unahitaji mlinzi na mwenye mamlaka katika kila zama ili kuilinda dini. Wakati “Walii” akimtuma mtu kama mwakilishi wake basi yeye pia ni “Walii”, kama ambavyo Malik Ashtar alipelekwa kama “Walii” kwa ajili ya eneo hilo tu la Misri.

Maadui wa “Wilaya” walitumia juhudini kubwa ili kubadilisha maana ya “Wilaya,” kwa kugeuza kituo cha “Wilaya,” wakati mwengine wanageuza asili halisi ya “Wilaya,” lakini yote haya yanatege-mewa kutoka kwa maadui. Jambo la kushangaza ni kwamba hata kama ulimwengu wote ukijitenga mbali na “Wilaya,” lakini vipi jumuiya ambayo ilikuwa inasikiliza Ghadir katika maisha yao yote ikae mbali na “Wilaya.” Hakika hili ni jambo chungu la kushangaza. Allah Azza wa Jallah ni shahidi juu ya ukweli huu kwamba milango ambayo Bibi Fatima (as) alipiga hodi mjini Madina bado hodi inapigwa hadi leo na yeye. Kuna watu mahususi ambao milango yao in-

apigwa hodi hata leo na Sayyida Fatima (as). Anawaambia kwamba mlifunga milango yenu na hamkutoa ushuhuda kwenye mfumo wa “Wilaya” wakati ule, lakini angalau basi katika zama zenu fungueni milango yenu na angalau katika zama zenu fungueni midomo yenu.

Hii ndio hofu aliyokuwa nayo Mtukufu Mtume (saww) kwamba Mola wangu kama umma huu unachukuwa suala hili la msingi la “Wilaya” kwa wepesi basi matokeo yake yatakuwa nini? Allah Aza wa Jallah akasema kwamba Mjumbe wangu usiwe na hofu nao, niogope Mimi na tangaza ujumbe huo. Dini imekamilishwa na sasa tangaza “Wilaya,” anzisha mfumo wa “Wilaya” na uelezee kwa watu. Hata kama wale Maasumin kutoka katika kizazi chako ambao Allah Aza wa Jallah atawateua kama “Mawali” Wake watabakia wakiwa wametengwa katika nyumba zao, watadhulumiwa, lakini bado wakati utakuja ambapo bendera ya “Wilaya” itanyanyuliwa tena. Ni hadithi ya Imamu Sadiq (as) kwamba: **“Mtu atajitokeza kutoka katika mji wa Qum, ambaye atahuisha utajo wetu halisi, ambaye atarudisha mambo yetu kuwa hai tena na ambaye atawalingania watu kwenye mfumo wa Allah Aza wa Jallah.”** Mtu huyu atawaambia watu kuachana na Ndama wa Saamir na kuja kwenye mfumo wa Mungu wa utawala.

Demokrasia ni ndama wa Saamir. Inawezekana wakati mwanafunzi wa dini kama mimi nikisema haya unaweza ukafikiri kwamba mimi najua nini kuhusu Demokrasia, na wanachuoni hawa havataki Demokrasia ndio maana wanaizungumzia kinyume chake. Ngoja niwaambieni kuititia maneno ya mtu safi aliye elemika vizuri (Allama Iqbal), mtu ambaye alitoa ile fikra ya Pakistan. Na yule mtu ambaye ametoa fikra ya Pakistan hakuwa mtu mtupu ambaye angetoa fikra ya taifa na kututaka sisi tuunde taifa lakini asitufahamishe kuhusu mfumo wa kisiasa wa taifa hili. Alitoa wazo la taifa hili na vilevile sambamba na hilo akatufahamisha kuhusu mfumo wa

kisiasa kwa ajili ya taifa hili. Hakusema kwamba undeni taifa kwa jina la Uislamu na kisha likabidhini kwa Saamir. Alijua wazi kabisa kwamba Saamir wengi watakuja na Ndama zao wakiwataka watu kuabudu ndama hawa, na watu wataanza kufanya hivyo. Wakati mwingine watakuja na ufalme, wakati mwingine na Udikiteta, kisha na demokrasia. Lakini Allama Iqbal kwa wazi alisema kwamba, kile ambacho taifa linahitaji ni utekelezaji wa Uislamu kama mfumo. Hatuhitaji mabaraza ya ki-Sufi ya ma-Saamir wa kidini, hatuhitaji dini ya kuabudu masanamu ya Azari, lakini tunachotaka ni dini ya “Shabbir.” Na dini ya “Shabbir” (Imamu Husein (as)) ni mfumo wa “Wilaya”.

Taifa hili linahitaji dini ya Imamu Husein (as), mfumo wa Uimamu na Umma (Uongozi na taifa). Nashangazwa kwamba Umma wetu ambao ulikuwa umehusishwa na “Wilaya” tangu vizazi, leo hii wanashangazwa kuhusu mfumo wa “Wilaya.” Leo wakati Mfumo wa “Wilaya” umeanzishwa, wakati bendera ya “Wilaya” inapepea tunapaswa tuwe watu wenyewe furaha sana. Lakini huu ni mgogoro mkubwa wa “Wilaya” kwamba zaidi wale waliokuwepo kule Ghadir na wanahuishwa na tukio la Ghadir, ndio hao ambao hawajali na kukaa wakizembea kuhusu “Wilaya”. Wale ambao walitoa sifa na kusema “Bakhin, Bakhin” (na leo wale wanaosema “Hongera, Hongera” na kulikubali tukio hilo) walikuwa ndio watu ambao wakati ulipofika walikaa kimya. Ndio watu ambao Bibi Fatima (as) anapiga hodi kwenye milango yao. Ndio watu ambao binti ya Fatima (as) alitoa khutba kule Kufa dhidi yao. Usifikiri kwamba Kufa ulikuwa mji mdogo, ulimwengu wote ni Kufa, na ndani ya huu ulimwengu wote wa Kufa binti ya Fatima (as) anasimama imara na kutoa khutba akiseema kwa nini mnakaa mkizembea kuhusu “Wilaya”, kwa nini mko kimya, kwa nini mmeichukulia dini kwa wepesi namna hiyo, ni wapi

mtafikia pamoja na uzembe huu, mtapata nini, kwa nini mnnavutiwa mno na Ndama wa Saamir na kujitenga na Mfumo wa Allah Aza wa Jallah kwa sababu tu ya kunong'ona kwa shetani?

## VITA VYA KISAIKOLOJIA JUU YA “WILAYA”

Mbinu moja zaidi inayotumika dhidi ya “*Wilaya*” ni shinikizo la kisaikolojia. Pambano lenye matokeo mazuri na pambano rahisi kabisa kupigana ni vita vya kisaikolojia. Hiki ni kitu ambacho kinaelekea kwenye kilele chake siku hizi, vite vita katika Marekani, Muungano wa Ulaya na Jamhuri ya Kiislamu ya Iran. Kuna watu wanaosema ni nini ambacho kitatokea kama vita vitaanza katika Magharibi na Iran, kiuhalisia vita tayari vinaendelea kupiganwa. Vita havina maana tu ya milipuko, vita katika Magharibi viko katika hali ya kisaikolojia. Vita vya kisaikolojia maana yake ni kudhoofisha ari ya upande mwingine, kwa kuweka shinikizo. Kwa kuweka shinikizo upande mwingine huonesha udhaifu wake na hatimaye hulazimika kutoka nje ya uwanja wa mapambano. Hii ilikuwa na bado ni hatari zaidi kuliko vita vya risasi na kuna wataalamu wa aina hii ya vita waliopo sasa ambao wanajua vizuri sana mchezo upi wa kucheza na kwa wakati gani.

Wataalamu hawa wa vita vya kisaikolojia wana ujuzi mkubwa mno wa udhaifu wa wafuasi wa “*Wilaya*”. Kama tujuavyo katika vita vya Siffin mtaalamu wa vita hivi (Amr ibn Aas) alibuni mpango kama huo ambapo aliletu Qur’ani katika ncha za mikuvi. Mtaalamu huyu alielewa vizuri sana kuhusu upinzani wa mabadiliko wa wafuasi hawa wa “*Wilaya*” kule Ghadir katika vita hivi, na matokeo yake ni kwamba walimwacha “Walii” wao akiwa ametengwa. Mtaalamu huyu alielewa kuhusu majibu ya wafuasi wa “*Wilaya*” pale Ghadir. Kwa mfano chukua suala la Hassan ibn

Thabit ambaye aliandika shairi la kwanza kabisa katika kumtambua Amirul Mumini (as) kule Ghadir na kupokea shukurani kuto-ka Mjumbe wa Allah Azza wa Jallah (saww). Lakini baada ya kifo cha Mtukufu Mtume (saww) Hassan hakumuunga mkono Ali (as). Licha ya kuandika mashairi, tenzi, wakati alipotakiwa kushuhudia tukio la Ghadir hakujitokeza kwenye uwanja wa mapambano ya “Wilaya.” Na sio hilo tu, wakati Ali (as) alipokuwa Khalifa wa nne wa Waislamu wakati huo vilevile kila mtu alipokula kiapo cha utii kwa Ali (as), Hassan hakufanya hivyo na akaondoka zake kwenda Damascus. Hii inathibitisha kwamba sio kila mtu ambaye aliisifia “Wilaya”, kuandika mashairi na kaswida angebakia imara na kujikita katika msingi wa kiutendaji wa “Wilaya”. Sio kwamba kila mtu kama huyo anaweza kuvumilia shinikizo ambalo huja juu ya “Wilaya” na kwa wafuasi wa “Wilaya.”

Mtihani wa “Wilaya” ni mgumu sana na wafuasi wengi wanakimbia wakati muda haswa wa mtihani unapokuja. Mchezo mmoja rahisi sana waliocheza kule Siffin ulikuwa kuleta Qur’ani katika ncha za mikuki na “Walii” aliendelea kuwasihhi wasidanganyike kwa hili lakini bado walidanganyika kwa ulaghai huo. Matokeo ya kutomsikiliza “Walii” ilikuwa ni uharibifu walioufanya ambaou umekuwa hauna matengenezo mpaka mwisho wa dunia. Yote hii ilikuwa kwa ajili ya shinikizo la kisaikolojia ambalo ha-wakuweza kulivumilia.

Siku hizi vilevile kitu kama hicho hicho hutokea. Amr ibn Aas wa zama zetu wanakuja kwenye mimbari na kuwasilisha aya za Qur’ani katika muundo uliopotoshwa, wanawasilisha hadithi katika mtindo wa kubuniwa na upotoshaji, na wafuasi wa “Wilaya” hawachukui muda kudanganyika nao. Ni kitu kile kile iwe Qur’ani imewekwa kwenye ncha za mikuki au aya za Qur’ani zinapotoshwa dhidi ya “Wilaya.” Mwalimu wangu anayeheshimika Ayat-

ullah Jawwadi Amouli alifafanua maelezo ambayo hufanya moyo utetemeke. Anasema: **“Jumuiya yoyote ambayo hudanganyika wakati Qur’ani inanyanyuliwa juu ya ncha za mikuki, siku moja watashuhudia kichwa cha “Walii” wao juu ya ncha ya mikuki.”** Hii ni kweli kwa sababu tu ya kudanganyika kule Siffin; matokeo yake ni kwamba kichwa cha Imamu Husein (as) ambaye ni “Walii” kilionekana juu ya ncha ya mkuki katika masoko ya Kufa.

## **“WILAYA” – SUALA LENYE MWELEKEO WA UBISHANI**

Mbinu nyingine ya kisaikolojia ni kwamba wanaibainisha “Wilaya” kama suala la kiubishani. Wakati ule mtu anaposikiliza kwamba hili ni suala la kiubishani linashusha chini msukumo wake. Hivyo watu hufikiri kwamba kwa vile wanachuoni wanahitilafiana katika suala hili, hakuna sababu ya kujuu au kujitumbukiza ndani ya suala hili. Nimewasimulia kauli ya mwandishi wa kitabu *al-Jawahir*. Yule mwanasheria (Faqih) ambaye vitabu vyake hukubaliwa kujifunzia kwa ajili ya wengine ambao huwa ma-Faqih. Anasema kwamba mtu ambaye hayuko tayari kukubali “Wilayatul-Faqih” hajaonja Fiqh kabisa. Baada ya kujuu yote haya bado wanakuja na kusema kwamba hili ni suala la kiubishani, kwanza kabisa hatuzungumzii kuhusu “Wilaya” (hususan “Wilaya” ya zama zetu, ambayo ni “Wilayatul-Faqih), kisha wakati wanapokuja kuzungumza pia wanasesma ni suala la kiubishani ambalo kwalo baadhi ya watu wanaliamini na baadhi hawaamini.

Sasa ikiwa hii ndio mantiki inayotumiwa ili kuwa mbali na “Wilaya” basi jua suala hili lilikuwepo tangu awali kabisa. Ni wach-

ache tu walioikubali “*Wilaya*” baada ya Ghadir, wengi wao waliachana nayo. Huu ulikuwa ndio msiba wa “*Wilaya*” kuanzia siku ya mwanzo ya kutangazwa kwake. Kama ukiambiwa kwamba “*Wilaya*” ni suala la ubishani kuanzia mwanzo wake hasa, basi ndio utaiacha “*Wilaya*” ya Amirul Muminin (as)? Bila shaka utajibu kwamba; hata kama ulimwengu wote wanaiacha sisi kamwe hatutaicha. Hii halikadhalika ni haki ya “*Wilaya*,” kwamba hata kama ulimwengu wote naiacha sisi kamwe hatuiachi. Mantiki hiyo hiyo pia hutumika kwa “*Wilaya*” ya wale ambao wameteuliwa na Maasum (as), hata kama ulimwengu wote ukisema ni suala la kiubishani basi vilevile lazima useme kwamba hata kama ulimwengu wote ukiiacha sisi kamwe hatutaicha.

Hii ndio hatua ngumu zaidi wakati wafuasi wa “*Wilaya*,” wafuasi wa Ghadir wanapokuwa wazembe na wasioijali “Wilayatul-Faqih.” Hii ndio iliyokuwa hofu ambayo Mjumbe wa Allah Azza wa Jallah (saww) alikuwa nayo katika siku ya Ghadir.

## **MAONO YA ALLAMA IQBAL JUU YA “WILAYA”**

Tunahitaji kuona vipi mtu mzima huyu mashuhuri Allama Iqbal anavyowasilisha Uimamu na *Wilaya*. Anasema kwamba fedheha mbaya mno kwa Waislamu ni kwamba wameuchukua Uislamu lakini ha-wakuuchukua kama mfumo, maana yake ni kwamba wamepuuza vi-pengele vyta kisiasa vyta dini. Wakati ambapo fedheha kwa watawala imekuwa kwamba wamechukua siasa lakini wakaiacha dini. Allama Iqbal anasema kwamba kama dini inatenganishwa na siasa basi kilichobakia ni ukatili na ushenzi (maana yake umwagaji damu). Na kama siasa inatenganishwa na dini basi kilichobakia ni baraza la

Masufi lijulikanayo kama “Baraza la Sufi”. Ukatili na udhalimu sio siasa, wala Baraza la Sufi sio dini.

Baraza la Masufi (Baraza la Sufi) ni kama kituo kile cha ibada ambacho hakina uhusiano na jamii. Na kituo hiki kinaweza kuwa kitu chochote; inaweza kuwa Msikiti, Husainiyah, au Madrassa. Hata kama ni shule ya elimu ya kidini, lakini kama haina uhusiano na jamii basi hii pia ni “Baraza la Sufi.” Kama ni Msikiti ambako swala huswaliwa lakini Msikiti ule hauna uhusiano na jamii au kama ni mimbari ambapo Majalis husomwa na hauna uhusiano na jamii basi ni “Baraza la Sufi.” Hivyo siku hizi dini na siasa vilipotengenishwa, kimoja kikageuzwa kuwa baraza la Masufi “Baraza la Sufi” na kingine kikageuzwa kuwa ushenzi. Nani ataivunja njia ya ushenzi? Nani ataleta ukombozi kwa wanadamu kutokana na ushenzi? Dini ya Baraza la Masufi kamwe haiwezi kuleta ukombozi kwa wanadamu kutokana na ushenzi. Aina hii ya dini ni aina ya dini isiyojihuisha na siasa. Ni mtu kama Imamu Khomein (ra) ambaye alijitokeza na kuugonga ushenzi na kuwafanya washenzi waonje vumbi. Lakini kufanya hivi wewe mwenyewe lazima uachane na dini ya kibinafsi isiyo ya kujishughulisha, yaani ya “Baraza la Sufi.” Lazima ujitekeze na kuingia kwenye uwanja wa mapambano. Katika uwanja wa uvumilivu na harakati. Lazima uje kwenye uwanja halisi wa Ghadir. Lazima ufungue mlango amba Bibi Fatima (as) alipiga hodi. Katika historia yote ni huyu mtoto wa Fatima (as) Faqih huyu mmoja, Imamu Khomein (ra) ambaye alifungua mlango amba mama yake alikuwa akipiga hodi tangu miaka 1300 iliyopita. Imamu Khomein alielewa kile ambacho kwa kweli kilitokea kule Ghadir na asili ya Ghadiri. Alisema “Labbaik,” nimekuja kwenye wito wa Bibi Fatima (as). Mimi ni muunga mkono wa “Wilaya”. Imamu Khomein aliwaambia watu watoke nje ya “Baraza la Sufi” na wakubali dini ya Imamu Husein (as).

## BARAZA LA USHAURI LA SHETANI

Kuna shairi lililoandkwa na Allama Iqbal katika mkusanyo wake wa “*Armaghan-i-Hijaz*.” Shairi hili la ki-Urdu linaitwa “*Iblis ki Majlise Shura*” (Baraza la ushauri la shetani). Hili ni shairi lenye kuelemisha ili kuelewa mifumo ya kisiasa ya shetani na mwelekeo ambao kwamba mifumo hii inalipeleka taifa (umma). Ingawa shairi hili lil-iandikwa kabla ya zaidi ya nusu karne, maana yake ni mbichi/mpya kabisa kiasi kwamba baada ya kulisoma huonekana kama limeandikwa leo.

Mada ya shairi hili ni kwamba Shetani aliiita kamati ya wawakilishi wake wote kutoka maeneo mbalimbali ya ulimwengu. Aliwakaribisha na akawauliza kuhusu hatari inayoikabili mifumo ya kisiasa ya kishetani ya udikiteta na ubeberu. Baadhi ya wawakilishi wake walisema kwamba hatari kubwa mno kwa mifumo hii ni kutoka kwenye Demokrasia, baadhi wakasema Ujamaa, na baadhi wakasema Ukomonisiti. Baada ya hili shetani alimjibu kila moja wao akikanusha maneno yao na kuwakosoa kuhusu kuchukulia kwao mambo kwa wepesi na upumbavu. Aliwaambia ninyi wote ni wapambavu ambao hamuwezi kuona kwamba Demokrasia si chochote bali vazi ambalo mimi mwenyewe nimelishona na nikaufanya udikiteta kulivaa. Shetani aliwaambia wanafunzi wake kwamba Demokrsia ni ndama wa Saamiri na Shetani mwenyewe ni Saamiri wa ndama huyu. Ujamaa na Ukomonisiti vyote ni ndama za Saamir. Shairi ni refu mno na kwa hiyo nawasilisha tu kifungu chake cha mwisho. Ni muhimu kuwaelewa maadui na kile amba-cho maadui wanachochukulia kama mhimili wa dini.

Taarifa ya mwasilishaji wa mwisho wa Shetani:

*Kwa ajili ya kuungua kwa nafsi zenu,  
ulimwengu huu unaimarishwa.*

*Wakati wowote mlipotaka ninyi  
mlifichua kila kitu chini ya shungi.*

*“Moyo wako katika ufinyazi wake  
umetokea kuwa fahari na kivutio cha dunia.  
Hivyo umewafundisha wapumbavu  
wa mbinguni hekima.”*

*“Yeye (Allah) anajua asili ya mwanadamu  
vizuri zaidi kuliko wewe Shetani.*

*Nani ni mashuhuri kama Mwenyezi Mungu  
katika wanadamu wa kawaida, wapumbavu.”*

*“Ambaye kazi yake ilikuwa ni kuswali,  
kusoma na kufanya tawaf, kuzunga Kaaba tu,  
kwa ajili ya husuda zao. Katika aibu daima  
wamefungwa.”*

*“Ingawa wenye busara wote wa Magharibi  
ni mashabiki na wanafunzi wako  
lakini sasa sina imani juu ya busara zao.”*

*“Yule Myahudi mweneza fitina,  
ile nafsi ya Muzdaq.  
Kila gwanda huchanika kutokana  
na lengo lake la uchizi.”*

*“Kunguru huonekana kuelekea  
kunyakuwa uso wa mwewe.  
Haraka iliyoje, ya wakati kubadilisha  
njia ya maumbile”*

*“Akiwa mwenye wahaka alichagua  
sehemu kubwa ya anga.  
Kama wajinga tulihesabu ‘vumbi’  
la mbio za mwanadamu.”*

*“Vitisho vya baadae,  
vikionekana vikubwa mno  
kwa vilima na mabonde  
hutetemeka wacheza kamari  
kwa ukubwa wa ongezeko.”*

*“Bwana wangu!  
ulimwengu ule utatoweka  
Ulimwengu ambao mzingo wake  
ulikuwa mifumo yako ya siasa.”*

Hii ilikuwa ndio hofu ambayo mwanafunzi mmoja aliwasilisha kwa Shetani na jinsi Shetani alivyowajibu wote.

*“Hivyo ndivyo ziliyyo katika miliki yangu  
fahari na vivutio vya dunia, ardhi hii,  
Jua na Mwezi, Anga linang’aa.”*

Shetani anawaambia wawakilishi wake wasiogope kwa vile udhibiti wake bado upo juu ya kila kitu.

*“Kila mtu ataona michezo ya Mashariki na Magharibi  
Wakati nitakapoinyanyua damu ya taifa la Magharibi.”*

Shetani anasema kwamba wakati nitakapounyanyua utamaduni wa Magharibi, matamanio na mapenzi (ya dunia), basi ulimwengu wote utashuhudia michezo yangu ya majanga. Hiki ndicho Iqbal alichokisema zaidi ya nusu ya karne iliyopita, hata kabla ya Pakistan kuundwa, na leo hili limejitokeza kuwa ni kweli, kwani ulimwengu unashuhudia utamaduni wa Magharibi na uvamizi wa umwagaji damu katika mataifa ya Kiislamu.

*“Viongozi wa siasa (dola)  
na mapadri wa Makanisa  
Wote wanaweza kuwa wendawazimu  
kwa mwangi mmoja tu  
wa sauti yangu ya kutisha.”*

Shetani anasema kwamba mwangi wangu mmoja tu wa kishetani unaweza kuwafanya wendawazimu viongozi wote wa kisiasa na mapadri.

*“Mjinga huyu anafikiri huu ni ulimwengu wa kisasa  
Hebu naavunje hivi vikombe vyatdivai vyatutamaduni huu aone.*

*Mikono ya maumbile imezichana kashida,  
mantiki ya Muzdaq haiwezi kuziondoa.”*

Shetani anasema kwamba maovu ambayo nimeyasababisha kati-ka mifumo ya wanadamu haiwezi kuondoka kwa hii mifumo mipya (Ukomunisti, Ujamaa na Demokrasia). Mifumo hii mipya ni kama mantiki ya Muzdaq ambayo haiwezi kufanya chochote (Muzdaq alikuwa khatibu mwenye ufasaha, mwandishi ambaye alileta dini mpya. Alikatwa kichwa kwa amri ya Mfalme Nausherwan). Shetani anasema kwamba hakuna kashida iliyobakia ambayo sikuichana. Kwa hiyo, mifumo hii ya kisiasa tayari imeshawishiwa na uharibifu wangu na hawawezi kunifanya chochote.

*“Vipi watanitishia vijana ujamaa,  
tangu muda mrefu bila kazi,  
vijana wasio na kazi muda mrefu,  
waliochanganyikiwa na wazururaji.  
Tishio pekee nililo nalo ni  
kutoka kwenye umma ule,  
ambao moyo wake bado unashikilia  
vijinga vilivyofichika vya shauku.”*

Shetani anawaambia washauri wake kwamba msishaogope watu hawa ambao wanakuja na kaulimbiu za Ujamaa na Demokrasia, wanatoka kwenye kundi letu tu. Vijana hawa wa mifumo kama hii ambao wanajali kazi zao tu hawawezi kufanya kitu chochote kwetu. Lakini tishio pekee nililonalo ni kutoka kwenye taifa ambalo bado lina haja iliyofichika ya mageuzi ndani ya nyoyo zao.

*“Wachache wao ninaweza kuwaona  
katika umma huu ambao  
alfajiri hutawadha wakitokwa na machozi  
(kwa kumkumbuka Mola wao).”*

Shetani anasema kwamba anahofia mtu mmoja au wawili kama hao ambao huzaliwa katika mataifa. Watu hawa ni wale ambao huanza siku yao kwa utajo wa Mola wao kwa kujilowesha kwa machozi. Hawa ni watu wale ambao wanajali kuhusu mambo ya Allah Aza wa Jallah. Ni nafsi zisizotulia. Shetani anahofia watu kama hawa, watu kama Shahid Arif Husaini, kama Shahid Sadr, kama Imamu Khomein (ra).

*“Je, ninyi wote mnajua yule ambaye  
ameng’arisha kina cha ndani,  
Muzdaqiyat sio tishio, bali ni Uislamu.”*

Shetani anasema kwamba mifumo hii mipya iliyotengenezwa na watu (kiistiali akimkusudia Muzdaq, ambaye alianzisha dini mpya) haina tishio, bali ni Uislamu ambao ndio wenye tishio, na hilo bado ni hai katika kina cha ndani cha umma.

Sasa, Shetani anatoa ushauri wake na sera za kufuatwa.

*“Najua kwamba umma huu sio wafuasi wa Qur’ani,  
na Dini ya waumini ni ubepari (shauku kwa ajili ya utajiri).”*

Shetani anasema kwamba nafahamu vizuri sana kwamba umma huu haujihusishi na Qur’ani. Halikadhalika kwa Ulaya taifa hili pia liko katika kufukuzana kwa ajili ya mapato ya kidunia na ulimbikizaji wa mali.

*“Najua kwamba katika giza la masiku ya Mashariki  
Hakuna walinzi wa Haram ambao wana mikono myeupe.”*

Shetani anasema kwamba naujua ukweli huu kwamba katika giza hili la upotofu ambao tumeutengeneza, hakuna viongozi wa dini

ambao wako kama Musa (as). Viongozi hawa wa dini hawana tabia zile za Nabii Musa (as), sio Musa wa zama zao (ambayo maana yake ni kwamba wao hawako tayari kusimama dhidi ya Firaun wa zama zao).

*“Ninahofia mahitaji ya zama za sasa  
Kama Dini (ya kweli) ya  
Mtume itadhihirishwa.”*

Shetani anasema kwamba jambo kubwa linalonihusu na hofu niliyonayo mimi ni kwa ajili ya dini ya kweli na safi iliyoletwala na Mtume (saww) na katiba iliyowasilishwa na Qur’ani. Hiki ni kitu ambacho nimekikandamiza kwa karne nyingi na nimekizika chini ya matabaka ya vumbi, na wasiwasi wangu mimi ni kwamba dini hii ya kweli kamwe isije ikawa hai tena, na Umma kulazimika kuchukua njia ya kurudi kuelekea kwenye katiba hii ya Kiislamu na mfumo wake.

*“Tahadharini! Mara mia kutokana  
na ile Katiba (ya dini) ya Mtume.  
Ambayo inawalinda wanawake,  
na ambayo inayowafanya wanaume  
kuwa na maamuzi na wakamilifu.”*

Shetani anawaonya wanafunzi wake kwamba lazima wawe na hofu kubwa na wasiwasi kuhusu dini iliyoletwala na Mtukufu Mtume (saww). Dini ile ambayo ni mfumo unaohifadhi heshima na usafi wa wanawake, dini ile ambayo hufanya matayarisho ya kutoka nje na kupambana, na hutoa ujumbe kuonesha njia ya ukamilifu wa mwanaadamu.

“Ujumbe wa kifo kwa kila aina ya utumwa  
Huondoaa ufalme na kuondoa uomba omba.”

“Dini ambayo husafisha mali kutokana na uchafu wote  
Huondosha mali kutoka kwa wadhamini wote matajiri.”

“Ni kipi kinachowenza kuwa mapinduzi makubwa kuliko yale ya  
fikra.

*Ambayo huhubiri kwamba nchi hii ni ya Allah na sio ya wafalme.*”

“*Ingelikuwa bora kama katiba hii (ya kidini) ingebakia imefichika  
mbali na ulimwengu huu.*

*Ni vizuri kwa sasa kwamba waumini wenyewe hawaiamini.*”

Shetani anawashauri wanafunzi wake kwamba dini hii ya kweli ambayo huwasilisha katiba ya Kiislamu, mfumo wa Wilaya, Uislamu wa kisiasa lazima ibakie imefichika kabisa mbali na ulimwengu. Shetani anawaambia wanafunzi wake kwamba lazima washukuru kwamba wafuasi wenyewe wa dini hawaiamini dini yao, kwamba dini hii ina uwezo wa kutawala jamii, na haya ni mafanikio makubwa kwa dini ya Shetani.

“*Ni vizuri kwamba wanajishughulisha na masuala ya metafizikia  
(falsafa ya udhanifu).*

*Na katika kubuni tafsiri zao wenyewe juu ya Kitabu cha Allah.*”

Shetani anawashauri wanafuzi wake kwamba ni bora kuwashughulisha Waislamu katika masuala ya metafizikia ya viumbe, katika masuala ya kiubishani na mahojiano yasiyo na madhumuni kuhusiana na tafsri ya Qur’ani Tukufu.

*“Fanyeni hii kaulimbiu ya “Allahu Akbar” ivunjwe  
kwa mapumbazo ya ulimwengu wa kisasa  
Giza la masiku ya mumini huyu katika Mungu lisione mwanga  
tena.”*

*“Je, mwana wa Mariamu amekufa au amekuwa hai milele  
Iwapo sifa za Mungu ni sehemu ya dhati au ni mbali mbali?”*

*“Je yule ajaye ni Masihi wa Wakirsto,  
au ni mzaliwa upya mwenye sifa za mwanamageuzi?”*

*“Je, maneno ya Allah ni yenye kufa au kuzeeka,  
Ni itikadi ipi itakayoleta ukombozi kwa Ummah?”*

*“Je, haitoshi kwa Waislamu wa zama hizi,  
(kwamba) masanamu haya yametengenezwa  
nje ya majadiliano ya uungu?*

Shetani anaelekeza kwenye majadiliano yasio na msingi ambayo Waislamu wanajiingiza humo, mfano, iwapo Mtume Isa amekufa au yuko katika maisha ya milele, iwapo maneno ya Allah ni yenye kutoweka au kuzeeka? Shetani anasema inatutosha sisi kwamba Waislamu katika zama hizi wenyewe wametengeneza itikadi na masanamu ya mijadala ya Mungu. Shetani amefurahi na anawaambia wanafunzi wake kuwaacha Waislamu wajishughulishe katika aina hiyo ya mijadala na kuwazuiya wasije kwenye siasa, kuwaacha wajishughulishe na masuala ya kiti kati ya kinadharia ambayo huwaweka mbali na katiba halisi ya Uislamu.

*“Muweke mbali na ulimwengu wa ujenzi wa tabia  
Hivyo kuzishinda pauni (kete za bao la chess) zake  
katika maisha yake.”*

*“Ni vizuri kwamba waumini wabakie watumwa  
mpaka Siku ya Mwisho*

*Hivyo wauache ulimwengu huu  
ili wengine wafurahie.”*

Shetani anawashauri wanafunzi wake kuwafanya waumini wasitambue madhumuni halisi ya maisha ambayo ni kuendeleza maadili mema na kujenga tabia katika maadili haya, na kama mwanadamu anashindwa kufanya hivi, basi harakati yake yoyote ya kiungu katika maisha yake itashindwa kwa urahisi sana na Shetani. Anasema kwamba mfanye muumini asitambue jukumu lake katika ulimwengu huu. Kwa hali hiyo atakuwa mtumwa mpaka mwisho wa dunia hii, na wengine wanaweza kwa urahisi kuvuna manufaa ya ulimwengu huu.

*“Mashairi haya ya Usufi ni bora kwake  
yale ambayo huficha kwenye macho yake  
mandhari muhimu za maisha.”*

Shetani anasema kwamba kwetu sisi ni bora kwamba mwanadamu yuko katika kujishughulisha tu na domokaya la aya na matendo ya ibada ya Usufi. Hivi visomo vya mdomo na matendo ya Usufi havitamruhusu kushuhudia ukweli na changamoto za maisha (hususan katika vipengele vya kisiasa ya jamii). Katika maneno mengine Shetani anasema kwamba natufanye ili tuondoe maisha ya kweli kutoka kwenye macho yake na kumfanya atumbukie kwenye ulimwengu wa dhahania.

*“Kila wakati ninakuwa na wasiwasi  
kuhusu kuamka kwa Umma huu,  
Ukweli wa yule ambaye dini yake iko katika  
kuwajibika kwa ajili ya ulimwengu huu.”*

Shetani anamwambia mwanafunzi wake kwamba natetemeka wakati nikiona dalili yoyote ya kuamka katika Umma huu.

*“Mwacheni afurahie dini ya visomo vya mdomo.  
Mfanyeni kuwa dhaifu kwa kuendeleza tabia ya Usufi.”*

Hii ni kanuni ya Shetani kuufanya Umma ujishughulishe katika dini ya visomo vya mdomo na vitu ambavyo havina maana. Shetani anataka aina ya muundo huu wa dini kujitokeza katika Umma ambao uko katika mfano kama ule wa Sufi, ambako watu hupendelea kukaa katika sehemu moja na kufanya visomo vya mdomo (Dhikr au Nyuradi), na Shetani anasema kama wakifanya vitu kama hivyo, basi hili litawafanya kuwa dhaifu sana. Waacheni wafanye Usufi na wasitoke nje kwenye eneo la siasa. Kamwe usimruhusu afahamu asili ya “Wilaya.” Kamwe usimruhusu mumini huyu kuelekea kwenye dini ambayo ngome yake imetengenezwa na Allah kama “Wilaya,” mfanye tu awe katika dini ambayo haina “Wilaya.” Na kama aki-jaribu kuelekea kwenye “Wilaya,” basi iwekee “Wilaya” hiyo mpaka iishie kwenye kusifia tu, usimruhusu kusonga mbele kuelekea kwenye kuikubali “Wilaya” kama mfumo wa utawala. Siku ambayo bendera ya “Wilaya” itakuja mikononi mwa Umma huu, siku hiyo ma-Saamir wote na masanamu yao wataporomoka chini.

Ilikuwa ni bendera hii ya “Wilaya” kwa maadili ambayo kwamba Imamu Khomein (ra) aliuvunja ufalme na udikiteta wa Shah. Ul-imwengu wa leo una wasiwasi tu na mfumo huu. Wanafurahia mi-fumo mingine ya kidunia. Kwa uwazi wanawasifia viongozi fulani wa Waislamu, jumuiya na watawala. Katika macho ya maadui hawa wa Uislamu, jumuiya mbaya mno na mhimili wa uovu ni umma na jumuiya ile ambayo imetegemezwa juu ya mfumo wa “Wilaya.” Hii ni kwa sababu maadui wanatambua kwamba muda bendera hii ya

“Wilaya” itakapokuwa imepandishwa, basi njama zao zote zitakwamishwa na hakuna miujiza ya Saamir au sanamu lolote la Azari litakalokuwa na uwezo dhidi ya hili.

Maadui wamepandikiza wengi wa vibaraka wao katika ulimwengu wa Waislamu, wametengeneza mazingira ya mashaka na hofu, na kwa simu yao moja wapigayo, ulimwengu wote wa Kiislamu hunywea kwenye shinikizo. Lakini dhidi ya adui huyo huyo, waangalie jinsi ya wafuasi wa “Wilaya” walivyosimama imara, madhubuti na wanaongea. Wakati wakimwambia aache mpango wa nyukilia, anajibu kwamba siku ambayo ataacha mpango wake wa nyukilia nasi tutaacha wa kwetu. Wakati wakisema hatutawaruhusu kuendeleza nishati yenu ya nyukilia, anajibu kwamba ni lini tulionba ruhusa ya kulifanya hili? Je, uliwahi kutupa ruhusa kufanya lolote kabla ya hili? Je, ulitupa ruhusa kufanya Mapinduzi ya Kiislamu au tulionba ruhusa kwako? Je, tulionba ruhusa kwa ajili ya kuanzisha mfumo wa “Wilaya” na Wilayatul- Faqih kutoka kwako? Kwa kweli wewe ni katika wale waliokatishwa tamaa na mfumo huu wa “Wilaya.”

Hivyo mfumo ule ambao hauwashindi tu maadui bali pia huwakatisha tamaa ni mfumo wa “Wilaya.” Maadui wametupa macho yao juu ya wale Waislamu ambao hupitisha maisha yao nje ya mfumo huu wa “Wilaya.” Waislamu hawa (Mungu aepushie mbali) wanaweza kuwa sawa na kundi lile ambalo liko katika historia ambao siku zote waliwasaidia maadui, imma kule Siffin au sehemu nyininge. Hili ni kundi lile lile lililokuwa kule Kufa na Bibi Zainab (as) aliwatolea khutba, na kwa kweli kichwa (cha Imamu Husein (as)) vile vile kiliwuta nadhari yao kikiwaambia kwamba huu ni mfumo wa “Wilaya” ambao kwao haupaswi kutendwa katika hali ya uzembe kama huo. Kama mtakuwa wazembe na kujitenga wenye we mbali na mfumo huu wa “Wilaya” basi kamwe hamtakuwa katika amani

na furaha. Matukio yale, Ashura, matukio ya Kufa na Shaam (Damascus) safari ile ya masaibu, kile kichwa katika mkuki, yote haya ni matokeo ya kile walichokifanya kule Siffin na wakauacha mfumo wa “Wilaya” ukiwa umetengwa mbali. Imamu Ali (as) aliwalaani kwamba namna ambavyo mmeniacha mimi mbali Allah Azza wa Jallah vilevile atawaacha mbali.

Huu ulikuwa msafara wa “Wilaya” ambaao ulipita mitaani na soko la Kufa. Ni kitu gani ambacho kile kichwa juu ya mkuki ili-chokuwa inakipigia kelele kuwambia? Kilikuwa kinasema, mimi ni mtoto wa Zahra (as) ambaye alikuwa siku zote akipiga hodi kwenye milango yenu lakini hamkuifungua, na leo mtoto wake amekuja ku-waita akiwa juu ya mkuki. Binti yake (Zainab (as)) anawaiteni akiwa sokoni na anakuambieni kwamba lau kama msingebakia kimya na kukaa kizembe ndani ya nyumba zenu wakati mama yangu alipoku-wa anawaita, kichwa cha kaka yangu kisingekuwa leo juu ya mkuki.

## MLANGO WA PILI

---

### **IMAM KHOMEINI NA MFUMO WA WILAYA**

---

#### **IMAM – MOYO WA TAIFA (UMMAH)**

**H**ali ya Imam au Kiongozi ni sawa na ile hali ya moyo katika mwili ambapo umma unafanana na viungo vya mwili. Kazi ya moyo ni kusukuma damu ndani ya viungo. Kama damu ikiacha kuzunguka kupita ndani ya kiungo au sehemu yoyote, basi inapatwa na kupooza. Ile sehemu au kiungo kinachopooza kinachukuliwa kama kilichokufa na kisichokuwa na faida. Kwa mfano kama mkono wa mtu ukipooza na sasa kama mtu mwingine akimfanyia utani au dhi-haka, yeye atakuwa hawezi kufanya lolote. Yeye anabughudhiwa lakini hawezi hata kuamsha mkono wake. Hawezi hata kukunja kiganja chake kuwa ngumi kwamba useme pengine atawenza kufanya hivyo, hawezi kunyanya mkono wake na hata kama kupooza huko ni kwa kiasi kwamba anawenza kuunyanya, bado hatakuwa na uw-ezo wa kuurushia kwa mtu yoyote. Tunaweza kuona leo kwamba Waislam ulimwenguni ni zaidi ya bilioni moja lakini bado hawawezi kufanya chochote kuhusu Uzayuni. Na wakati wowote unapoona Waislam wakinyanya au kurusha mikono yao; ni juu ya shingo za ndugu zake Waislam wengine tu na sio juu ya maadui.

Uimam ni moja kati ya fadhila kubwa za Allah. juu yetu sisi wafuasi wa Ahlul-Bayt (as) ambayo kwamba wengi walinyimwa na

bado wananyimwa hata mpaka leo hii. Allah aliteua Imam (kiongozi) baada ya Mtukufu Mtume (saww). Alimteua Ali (as) na kizazi chake baada yake kama Maimam (viongozi) wetu na akatuambia tuendelee kushikamana nao ili kuepuka upoozaji. Kama ukibakia kushikamana na Uimam basi hii itakuwa ndio nguvu yako, hadhi yako, uwezo wako na watu watakuogopa, lakini kama ukilemaa kwa kupooza basi hata ukiwa millionea au billionea watu hawatakuogopa.

Kuna zaidi ya Waislam 170 milioni ndani ya Pakistani ambapo magaidi ni watu elfu moja tu lakini hawa mamilioni ya Waislam bado wanawahofia hawa magaidi wachache tu. Kwa nini? Kwa sababu hawa mamilioni wamepooza, wamelemaa. Hawana mahusiano na huyo Kiongozi bali badala yake wanahusiana na watu wa falaki, watabiri kwa viganja, watu wa hekima, watu wa miujiza waliojiten-geneza wenyewe, Abdul Sattar Eidhi (kikundi cha ustawi), Fadhlur Rahman (mwanasiasa mchafu), Sir Sayyid (mhubiri wa kisekyula - kidunia) na wengine wengi. Lakini hawana muungano na Kiongozi Mkuu wa Kweli wa Kiislam Sayyid Ali Khamenei. Umma haupati wokovu kutokana na watu wa hekima kwa sababu hawa watu wa hekima wenyewe wamepooza na wanadhamiria kuwapoozesha wen-gine. Wokovu kwa umma unaweza kupatikana tu kupitia Kiongozi wa Kweli (Rahbar). Unaweza kutimizwa tu kupitia mikono ya kiongozi ambaye amezalisha mashahidi ili kuhuisha Umma, aliyepuliza mzinduko ndani ya vijana, na huyo ni Imam Khomeini (r.a.).

## IMAM KHOMEINI - UKWELI ULIO HAI

Kiongozi Mkuu, Ayatullah Sayyid Ali Khamenei anasema: “Imam Khomeini (r.a.) ni ukweli ulio hai.” Yuko hai vipi? Yuko hai kupitia mawazo yake, uoni wake, malengo na kupitia Askari wake wa Ku-

jitolea (Basij) na wafuasi wake. Wakati watu bado wapo na wanajifunza kutembea katika njia ya Imam Khomeini (r.a.) yeye atabakia kuwa hai. Wakati ambapo njia ya Imam Khomenei inaendelea kuwepo, yeye anakuwa yuhai na hili ndilo linaloupa wokovu Umma ulionyongeka kwa huzuni. Umma unapata kuheshimika kwa kupitia njia hii na hii ndio nukta ambayo tunahitaji kujifunza na kunufaika katika suala la *Wilaya*.

Ni yapi yalikuwa mafanikio makubwa kabisa ya Imam Khomeini (r.a.)? Allah amewazawadia wengi leo hii mapenzi na msukumo wa Imam Khomeini (r.a.), na tunamuomba Allah atujaalie nasi utambuzi wake na maarifa yake. Mshairi wa Kiajemi anasema: “Bila ya mapenzi kwa Khomeini, mapenzi kwa Mahdi ni dhaifu.”

Imam Mahdi (a.t.f.s.) yeye mwenyewe amesema:

مَنْ كَانَ صَائِنًا لِنَفْسِهِ مُطِيبًا لِأَمْرِ رَبِّهِ حَافِظًا لِدِينِهِ

**“Yeyote mionganoni mwa mafaqihin anayeweza kulinda nafsi yake, ambaye anaweza kuihifadhi dini yake, anayepigana na hawaa zake na akawa ni mtiifu kwenye amri za Bwana wake, huyo anapasa kufuatwa na watu.”**

Faqihi yeyote ambaye anazo sifa hizi anakuwa ni mkamilishaji wa hoja juu yako kutoka upande wangu na mimi ni mkamilishaji wa hoja kutoka kwa Allah juu yako. Na vile vile amesema sambamba na haya kwamba yeyote anayemkataa Faqihi huyu amenikataa mimi na anayenikataa mimi amemkana Mwenyezi Mungu.

Mwakilishi wa Imam (a.t.f.s.) sio maasum bali ni mtu mashuhuri, Faqihi ambaye ameielewa dini. Allah anatujariibu na kututahini sisi. Kama Amirul-Mu'minin (a.s.) anamtuma Malik al-Ashtar kwenda mahali fulani na watu wa huko wakasema hawawezi kuelewa na

hawako tayari kumkubali Malik Ashtar, na bado wanadai kuwa ni wapenzi na wafuasi wake Amirul-Mu'minin (a.s.); basi wale ambao hawakuweza kumuelewa na kumtambua Malik Ashtar, hawataweza kamwe kumtambua na kumuelewa Amirul-Mu'minin (a.s.). Kumtambua Malik Ashtar ni uthibitisho kwamba wakati tutakapofika mbele ya Kiongozi wa kweli (a.s.) tutakuwa na uwezo wa kumfahamu na kumtambua yeze pia.

Mtu ambaye hakumuelewa Imam Khomeini (r.a.) hatamuelewa kamwe Imam wa Zama hizi (a.t.f.s.) vilevile. Mtu ambaye hakuweza kumuelewa mfuasi atawezaje kumuelewa huyo Bwana (a.t.f.s.) kwa sababu muelekeo wa wote, mfuasi na Bwana ni mmoja. Amirul-Mu'minin (a.s.) anazungumza na umma na anasema ndani ya *Nahjul-Balaghah* kwamba ninyi mnadai kwamba mmemuelewa na kumtambua Allah lakini hebu niambieni, mmemtambua Jibril au bado? Mtu ambaye ana mapungufu katika kumuelewa Jibril (a.s.) atawezaje kumuelewa Mwenyezi Mungu? Hivyo mtu ambaye hakuweza kumtambua na kumuelewa Imam Khomein (r.a.) na Kiongozi Mkuu anapaswa kuachana na madai kwamba mara atakapodhiihiri Imam (a.t.f.s.) yeze atamuelewa na kumkubali Imam Mahdi (a.t.f.s.). Umma nyingi zenyi kusubiri kama hizo zimekwishapita kabla vilevile. Bani Israili walikuwa wakimsubiri Nabii Musa (a.s.), lakini alipotokeza kila mmoja alimkubali isipokuwa hao Bani Israili. Wayahudi walikuwa wakimsubiri Mtume (saww), lakini alipodhiihiri, washirikina, wanafiki na hata waabudu masanamu walimkubali isipokuwa hao Wayahudi, wao walikataa kumkubali. Umma hizi zilizopita zilifikwa na yote haya ambayo tumesimuliwa na Qur'an na Ahlul-Bayt (a.s.). Hizi ni nyakati za tafakari ambamo tunahitaji kufikiri kwamba kama hatujafanikiwa katika mitihani hii ya leo hii, basi wakati wa kudhihiri kwa Imam al-Hujjat (a.t.f.s.) utakapowadia, kwa vyovoyote vile tutakuja kushindwa.

Itachukua vizazi vichache kuja kumtambua Imam Khomeini. Ayatullah Jawwadi Amuuli (d.a.) anasema kwamba itachukua karne mbili kumuelewa Khomeini. Lakini kuna wale Mashuhuda wa map-induzi na vita vyake vitakatifu vya ulinzi, ambao waliifanya safari hii ndani ya usiku mmoja tu. Na hii ndio sababu inapendekezwa kuyatembelea na kuyazuru makaburi ya mashahidi kama hao kwa sababu makaburi haya yanatufundisha sisi namna ya kufanya safari hii ya kumtambua Kiongozi katika kipindi cha muda mfupi kabisa.

Imam Khomeini (r.a.) alikuwa na mafanikio mengi makubwa. Yeye kwa mara nyingine tena amehuisha Uislam uliokuwa umepotea na kutelekezwa. Aliwasilisha sura halisi, ya kweli na iliyotukuka ya Uislam Halisi mbele za watu. Yule shetani (*Twaghuut*) ambaye Qur'ani inamzungumzia habari zake sisi tulikuwa tumemsahau. Tullichukua tu Tasbihi na tukakaa ndani ya misikiti na sehemu za ibada kwa kuwaonyesha migongo yetu mashetani wa zama zetu. Lakini yeye Imam (r.a.) amewatoa watu kwenye sehemu hizi za upweke za nyuradi na ibada na kwenda kwenye medani ya vita vya makabiliano na ametufundisha namna ya kuangalia macho ya twaghuti wa zama zetu. Amekabiliana na matwaghuti hao na akawashinda. Aliziamsha Umma. Haya yalikuwa ndio mafanikio ya Imam (r.a.). Miaka thelathini nyuma kabla ya hapa, Waislam walikuwa wamekata tamaa na walikuwa wakifikiria tu kujifunza Kiingerea na kuhamia Magharibi kwenda kujaza matumbo yao. Imam (r.a.) alifahamisha kwamba kama Waislam watajenga tabia ya kujiamini wenyewe na kwa kumtegemea Allah swt, Umma unaweza ukafikia hadhi yake ya kweli. Leo tunaweza kushuhudia kwamba ile njia ambayo kwamba Imam (r.a.) amepita ilitwaliwa na watu wengine kwa fahari kabisa. Zile njia ambazo watu wanajaribu kuzitafuta huko Magharibi, yeye Imam alizipata kutoka ndani ya Uislam na akawaambia watu kwamba dini yenu ina vile vito vya thamani na lulu zote ndani yake.

Mafanikio makubwa sana ambayo yalifurahisha nyoyo za Mitume na Maimam (a.s.) yalikuwa ni kule kurudisha upya Mfumo wa Wilaya na Uimam vilivyokuwa vimegeuzwa kuwa ni visomo vyta mdomo, mijadala ya kusisimua, na ambavyo vilikanushwa na baadhi ya watu na kufanywa kama vikatuni na baadhi ya watu. Aliutambulisha mfumo huu na kuutekeleza katika wakati na zama za teknolojia; wakati dunia ilipokuwa inanyanya lile bango la wito wa kwamba dini zimefikia mwisho wao na kwamba sasa eti ni zama za teknolojia.

Yeye aliutekeleza mfumo huu ambao kuitia huo Mwenyezi Mungu aliwainua Mitume na ambao kwa ajili yake Maimam walifika na mabalaa. Yeye Imam (r.a.) aliukuta mfumo huu ukiwa umefichwa chini ya udongo, akautekeleza na hadi leo bendera ya Wilaya inapepea katika ardhi hii (Iran).

Imam (r.a.) alikuwa wakati wote na fahari juu ya wafuasi wake kwa sababu wao ndio walioitikia mwito wa Imam Husein (a.s.) mnamo siku ya Ashura. Katika nyakati za mwisho mwisho ile jioni ya Ashura, wakati kila mmoja alipokuwa ameuliwa, Imam Husein (a.s.) alitoa sauti ya wito: “Kuna ye yote wa kunisaidia mimi?” Hii ina maana kwamba Imam Husein (a.s.) alikuwa anauliza kama kuna mtu ambaye anahiari kuwa mwenye kusaidia kwa kuiendeleza mbele njia hii. Imam (r.a.) alijifaharisha juu ya walini wake wa kujitolea (Basiji) kwa sababu walikuwa kama wale masahaba wa Imam Husein (a.s.) ambao walikuwa waunga mkono wa njia hii na walikuwa hawako tayari kumuacha Imam (r.a) katika dakika za mwisho. Hivyo Imam Khomeini (r.a.) alikuwa na fahari juu ya “askari wake wa kujitolea,” na sio kwa wale waliomfuata na kumchukulia kama *Marja'a* wao katika mambo ya sharia.

Imam Khomeini (r.a.) alikuwa na idadi kubwa ya wafuasi waliomfuata katika mambo ya sharia, lakini kwamwe hakuwasifu.

Kwa kweli katika kisa kimoja cha kweli kilichosimuliwa, "Mfuasi" mmoja wa Imam (r.a.) ambaye alikuwa milionea alikuja kwa Imam (r.a.) kutoa pesa zake za khums. Aliziwasilisha pesa hizo kwa Imam Khomeini (r.a.) na Imam akamwambia aziweke pesa hizo kwenye kona moja. Alikuwa akimsubiri Imam (r.a.) aseme lolote, lakini badala yake Imam alimtazama na kumwambia aondoke kama amekwisha kumaliza kazi yake (kuziweka hizo pesa). "Mfuasi" huyu alikasirika na wakati akiwa anaondoka mahali hapo alilalamika kwa mhasibu. Alisema kwamba kama angezipeleka pesa kiasi hiki kwa marja'a mwingine, yeye angepokea itifaki ya kifahari sana na mtu angemsindikiza hadi kwenye mlango wa gari lake, lakini hapa Imam (r.a.) hakusema hata ile asante. Yule mhasibu akamwambia asubiri na akaingia ndani kwa Imam (r.a.) na kuelezea kauli hizo. Imam (r.a.) akamwambia yule mhasibu amlete mfuasi huyo kwake. Alipoingia ndani aliona kwamba zile pesa bado zilikuwa mahali palepale alipokuwa ameziacha yeye, na Imam (r.a.) akamwambia aokote pesa zake hizo na aondoke hapo mara moja. Yeye alishangaa na akauliza, kulikoni? Imam (r.a.) akamjibu kwamba, kwa kuzikubali pesa zako za khums mimi ninakupendelea wewe. Mimi ninapokea wajibu wako wa kutoa khums yako na kujitwisha mzigo huo mabegani mwangu; na wewe unategemea mimi nikushukuru kwa kusema akhsante?

Huyu alikuwa ni Khomeini (r.a.) ambaye hakumchukulia "mfuasi" kwa thamani hata kama angekuwa mtoaji khums mkubwa, lakini Imam huyohuyo, inapokuja kwa askari wa kujitolea yeye anasema kwamba, niko tayari kubusu mikono ya askari wangu wa kujitolea. Hii ilikuwa ni kwa sababu kwamba hao "askari wa kujitolea" wali-kuwa ndio Umma wenyewe na mfumo wa *Wilaya* ndio mfumo wa Uimamu (Uongozi) na Umma. Imam (r.a.) aliutengeneza Umma huu kwa ajili ya kuchimbua dini iliyopotea kutoka kwenye jalala la

uharibifu na ubadilishwaji na hapo kuuwasilisha kwa ulimwengu na kisha akautekeleza.

Huku ndio kufilisika kulikopindukia kwa Uislam hata leo hii kwamba ule mfumo wa *Wilaya* ambao Imam Khomeini (r.a.) ameuwasilisha bado unatiliwa shaka na watu na wanaauliza Imam ameupata kutoka wapi huu Mfumo wa *Wilaya* ambao una maana ya Utawala wa Kiislam, au Utawala wa Faqih (*Wilayatul-Faqih*).

Imam Khomeini aliuchukua mfumo huu kutoka Ghadir, kuto-ka ndani ya Qur’ani na kutoka kwenye tabia za Ma’sumiin (a.s.). Tangazo la Ghadir lingeweza kufanyika katika hali yenye kufurahisha vilevile, lakini kwa kulifanya tangazo hili katika joto hili kali na hali ya kuchokesha ilikuwa ni kuonyesha umuhimu wake. Na wakati tangazo hili lilipokuwa limekwisha kutangazwa kama ilivyolezwa kabla, likawa ni njia ya kukata tamaa kwa makafiri. Hii ndio desturi kwamba wakati wowote *Wilaya* inapotangazwa, huwa inavunja matumaini ya maadui kwa sababu tangazo hili sio la mtu bali ni la mfumo, na mfumo wa haki huvunja matumaini ya maadui. Hili lilikuwa ndio tatizo kwa wakati ule, ambalo lilimhofisha Mtukufu Mtume (saww) kwamba Umma hautakuwa na uwezo wa kulielewa tangazo hili, na kwamba wataanza kutoa tafsiri mbalimbali za tofauti, za urafiki na kadhalika. Hali hiyo hiyo inajitokeza leo hii vile vile wakati Serikali ya Kiislam au Mfumo wa *Wilaya* unapotekeleza katika Jamhuri ya Kiislam, kuna watu wanaoitafsiri kinyume; wanasema hili ni tangazo tu la Iran au Faqih huyu ni kiongozi wa wafuasi wake tu.

Mtukufu Mtume (saww) aliambiwa pale Ghadir kwamba atoe tangazo hili, na kwamba wakati huyo mrithi wa Mtume atakapoondoka duniani hapa naye atatangaza mrithi wake na hili litakwenda vivyo hivyo mpaka kwa mrithi wa mwisho (a.t.f.s.) atakapoingia ghaibuni, kisha naye atatangaza ni nani anayekuwa baada yake. Hii

ndio hoja tuliyonayo dhidi ya ndugu zetu Sunni kwamba ni vipi Mtukufu Mtume (saww) aweze kuuacha Umma peke yake tu? Tatizo la kuielewa *Wilaya* lilianza tangu siku ile ya kwanza na hata leo hii wale ambao wamekaa kwenye Hauza za Kiislam tangu miongo kadhaa huko nyuma, wakidai kwamba wao ni wafuasi wa *Wilaya* lakini wakati mjadala kuhusu Mfumo wa *Wilaya* na Utawala wa Kiislam vinapozungumzwa mbele zao, wao wanasema mfumo huu umetoka wapi? Wao wakiwa ndani ya Ghadir walilibadilisha tangazo la Mfumo wa *Wilaya* kwenda kwenye urafiki na wakatulia na mabango na miito ya kusifia tu. Shi'ah wa Imam Ali (a.s.) wamejitwalia desturi kama hiyo na wanafurahia katika kuishilizia tangazo hili la mfumo kwenye kupaza sauti na kunyanya mabango yenyе kusifia tu, basi.

Wanapaswa kusoma kwenye *Nahjul-Balaghah*, nawasome ile hotuba ya Imam ar-Ridhaa (a.s.) – ambayo imejadiliwa kabla – na ndani ya miezi miwili, mtetezi wa *Wilaya* alionyesha kwa Madina yote na kwa masahaba wa Mtukufu Mtume (saww) kwamba *Wilaya* na Uimam ni mfumo. Uislam huu uliozikwa, ambao ulizikwa chini ya uzembe, kutojali na fitna ulichimbiliwa na Imam (r.a.) na kutekeleza ndani ya jamii kama Mfumo (yaani Serikali ya Kiislam). Kubwa ya neema zinazotajwa ndani ya Qur'an ni huu Mfumo wa *Wilaya* na yule aliye na bahati ya kuipata hii anakuwa mwenye heshimia, na wale wanaojitenga na *Wilaya* wenyewe wamelemaa. Kama ilivyoolezwa kabla kwamba hata mkono unapendeza sana, mzuri kwa rangi, wenyе pete za kidoleni, lakini kama umetenganishwa na moyo basi hauna faida. Unatakiwa uchukue damu na uhai kutoka kwenye moyo, kadhalika na Umma unapaswa kuchukua uhai kutoka kwa Imam (Kiongozi).

Imam amerejelewa kama moyo. Hisham alikuwa mwanafunzi wa Imam Ja'far as-Sadiq (a.s.). Imesimuliwa kwamba wakati mmoja Hisham aliiingia kwenye mkusanyiko ambamo alikuwepo mpinzani

wa Imam as-Sadiq (a.s.) akitoa hotuba. Alikuwa akikanusha *Wilaya* na Uimam (Uongozi). Hisham akaingia ndani ya mkusanyiko huo na baada ya kupita mionganini mwa watu akafika mbele na akaomba aulize swalii. Mzungumzaji akamruhusu kuuliza. Hisham aka-muuliza, je unalo jicho? Yeye akajibu akasema ndio, halafu Hisham akamuuliza, unalitumia kwa kazi gani, yeye akajibu kwa kuangalilia vitu. Hisham akamuuliza tena, je unayo masikio? Akajibu ndio, naye akamuuliza, unayatumia kufanya nini, akajibu kwa kusikilizia. Hisham akaendelea kumuuliza juu ya kazi ya kila kiungo cha nje cha mwili na mzungumzaji akaendelea kujibu kwa kukubaliana na kazi zake. Kisha kufikia hapa Hisham akamuuliza, je unao moyo? Yeye akajibu ndio. Hisham akauliza, unautumia kwa kazi gani? Sasa hapo akakwama kwa sababu alijua kwamba ulikuwa ni moyo am-bao kwamba kutokana nao huo ndio viungo vingine vyote vinafanya kazi. Hisham akamuuliza kama viungo vya mwili vinaweza kufanya kazi bila ya moyo. Yeye akasema hapana haviwezi. Hisham ndipo akasema, ikiwa macho, masikio, mikono na miguu haviwezi kufanya kazi bila ya moyo, ni vipi Ummah utakavyoweza kuendesheka bila ya Imam. Mzungumzaji alishangazwa sana na akamuuliza Hisham kama endapo ni mwanafunzi wa Imam Ja'far as-Sadiq (a.s.). Hisham akaenda kwa Imam as-Sadiq (a.s.). Imam alikuwa amekwisha kuzi-pata habari za kuhusu majadiliano hayo ambayo Hisham aliyafanya. Imam alipomuona Hisham alifurahi sana na akamtaka Hisham kusimulia kisa chote. Hisham akasema mimi siwezi kufanya hivyo mbele yako kwa sababu mimi ni mtumishi wako mtiifu na huja hapa tu kukusikiliza na kujifunza kutoka kwako na sio kuongea mbele yako. Hivi ndivyo watumishi watiifu wa viongozi walivyo. Wakati Imam (a.s.) alipomuamuru Hisham kusimulia kile kisa na Hisham, ndipo Hisham akasimulia kila kitu kwa Imam as-Sadiq (a.s.). Baada ya hapo Imam as-Sadiq (a.s.) akamuuliza Hisham, umejifunza ku-to-ka wapi haya? Hisham akasema, kutoka kwako Ewe Mkuu wangu!

Wewe ulisema kwamba Imam ndio moyo wa Umma. Imam as-Sadiq (a.s.) alifurahi sana na akamkumbatia Hisham, na kumtia mabegani na kisha akamuombea Hisham.

## **MAFANIKIO MAKUBWA YA IMAM KHOMEINI**

Sasa hapa ndipo ambapo yapasa tuhitaji kufikiri kwamba Hisham alikaa tu mionganoni mwa maadui wa *Wilaya*, akazungumzia na kuthibitisha *Wilaya*; bali hakuitekeleza hiyo *Wilaya*, wala hakufanya vita dhidi ya waovu hao lakini bado Imam anamuombea. Lakini kuhusu mtu yule, ambaye amechimbua ile *Wilaya* iliyokuwa imezikwa, akafanya utafiti juu ya *Wilaya*, akawajulisha watu kuhusu hiyo *Wilaya*, akaanzisha vuguvugu, harakati, akasimamisha bendera ya *Wilaya* ndani ya kifua cha tekinolojia, je! itakuwa vipi hadhi ya mtu kama huyu? Je, Imam wa zama hizi (a.t.f.s.) hatamkumbatia mtu huyu? Yeye (a.t.f.s.) hatawatoa muhanga akina Hisham kwa mama juu ya mtu kama huyu? Haya ndio mafanikio makubwa mno ya Imam Khomeini (r.a) ambayo yalikuwa ndio sababu ya yeye kuan-dika ndani ya wasia wake wa mwisho na pia akiwa akilieleza hili wakati wa uhai wake kwamba:

“Kuweni waunga mkono majasiri (uti wa mgongo) wa Waliul-Faqiih.”

Jifanye kuwa wewe ndio uti wa mgongo au kiongozi, kuwa mfuasi muunga mkono wa kiongozi wa kweli na kama huwi muunga mkono basi historia itajirudia yenyewe. Hawakuwa waunga mkono na uti wa mgongo pale Ghadir, hadi leo hii ardhi ile iko chini ya Salafii na Nasibii. Kama wewe huwi mfuasi wa mfumo huu basi utanyakuliwa kutoka kwako. Hili lilitokea kwa Maimam Maasumin

(a.s.) vilevile kwamba Umma haukuwaunga mkono na hivyo haki za *Wilaya* zikaporwa kutoka mikononi mwao.

Mwenyezi Mungu aepushilie mbali, kama wewe huungi mko-no basi kivuli cha *Wilaya* juu ya ardhi hii kwa mara nyingine tena kitafutika na kufikia mwisho. Na kuna mashetani wanong'onezaji waliopo ambao wangependa kuona mfumo huu ukifikia ukingoni na kwisha kabisa.

Tangazo la Ghadir halikuwa ni kwa ajili ya zama zile tu, bali lilikuwa ni kwa ajili ya zama zote, nyakati zote na kwa ajili ya watu wote wanaoishi kila mahali. Kwa vile nyakati zingine hali zinakuwa zisizofaa, hivyo njia mbadala hutwaliwa. Wakati mazingira yan-apokuwa sio sawa kwa ajili ya mfumo maalum basi hapo mfumo mbadala unapendekezwa. Kama safari za anga hakuna basi kutaku-wepo na garimoshi (treni), kama hakuna garimoshi basi kuna mabasi ya abiria, kama hakuna mabasi kutakuwepo na teksi na kama hakuna teksi hapo basi ikibidi utatembea kwa miguu. Jambo lenyewe ni kwamba unapaswa kusafiri, inakubidi uondoke; haiwezekani kusi-mama na kutoa visingizio. Wakati wa uhai wa Mtukufu Mtume (saww) alipokuwa akienda kwenye jihadi, kila kitu kinachohitajika katika jihadi kilikuwa ni cha mtu binafsi. Leo hii serikali inatoa njenzo zote na kukuomba tu wewe kwenda kupigana. Lakini wakati ule, farasi angekuwa ni wako, upanga ni wako, chakula kitakuwa ni chako mwenyewe, kila kitu kingekuwa ni chako binafsi na utapigana katika njia ya Uislam ukitumia njenzo zako mwenyewe binafsi.

Tumeonyeshwa njia mbadala. Lakini hebu fikiria ile hali ambapo ndege inapatikana na bado mtu anataka kusafiri kwa garimoshi kwa vile tu wahenga wake walisafiri kwa garimoshi? Hao wahenga wako walisafiri kwa garimoshi kwa sababu kwa wakati ule hakukuwa na safari za anga na ni magarimoshi tu yaliyokuwa yanapatikana.

Mwenyezi Mungu ametuonyesha njia ya sawa iliyonyooka na pamoja na njia hiyo ya sawa, Yeye ametuonyesha njia mbadala ambayo inaweza kutwaliwa wakati wa mazingira maalum. Ni kama vile tu tulivyo na njia mbadala katika mikakati ya kivita, usafiri, shughuli za kibiashara na kadhalika. Njia ya kwanza ni Mfumo wa Wilaya, Uongozi na hii ndio namna ya kwanza. Lakini kama serikali ya Kiislam inakuwa haipo, hakuna kiongozi hivyo njia mbadala ni *Marjaa*. Hii ndio njia ya pili, panapokuwa hakuna kiongozi mwanchuoni anaweza kuteuliwa, yule ambaye anatimiza masharti yote ya kuwa *Marjaa* na anaweza kutoa fatwa lakini hawezi kuongoza. Kama hali inakuwa kiasi kwamba hakuna *Marjaa* pia, basi kikundi cha waumini waadilifu kinapaswa kiundwe na kitoe wajibu wao wa kidini, ambapo ina maana kwamba wao watakusanya khums na kuitumia mahali pake stahiki, kuwaangalia Mayatima, kufanya huduma za kijamii na kadhalika. Wajibu wa muumini mwadilifu sio tu kutoa fatwa bali ni kuzitekeleza tu sheria na kuzifanyia kazi kwa vitendo. Kama hakuna muumini mwadilifu basi Aalim ye yeyote achaguliwe kwa ajili ya utekelezaji wa mambo ya kidini.

Hii ina maana kwamba mambo ya kidini yasipuuze katika mazingira yoyote yale bali uzito wa utekelezaji wake huweza tu kupungua. Njia zote hizi haziendi sambamba kwamba unawenza ukajichagulia yoyote unayoitaka. Hizi ni njia mbadala tu ambazo zinawenza kuchaguliwa tu pale ambapo chaguo moja la namna ya kipaumbele cha juu halipo basi kipaumbele kinachofuatia kinawenza kutwaliwa. Ya kwanza katika namna zote hizi ni Imam Ma'sum (a.s.); kama yuko ghaibuni basi Kiongozi Mkuu, kama Kiongozi Mkuu hayupo katika zama fulani basi ni Mwanachuoni Mwadilifu, kama huyo pia hapatikani basi achukuliwe Muumin Mwadilifu, na itakapokuwa hakuna muumini mwadilifu basi achukuliwe muumini wa kawaida, na iwapo atakosekana muumini wa kawaida basi awe muumini akina

sisi. Hoja ni kwamba kwa mazingira yoyote yale mambo ya kidini hayawezi kupuuzwa au kutelekezwa.

Imekuwa ni desturi yetu kwamba tunaafikiana na muumini wa kawaida mwenyewe kwa sababu tu baba yetu pia alikuwa akifanya vivyohivyo. Unaweza kumfuata mtu ambaye sio maasum wakati kuna Maasum anayepatikana? Umma ambao haukuelewa *Wilaya* utafanya hivyo. Watu waliendelea kumfuata Abu Hanifa hata wakati ule ambapo Imam as-Sadiq (a.s.) alikuwepo. Hili lime-tokea katika historia. Umma ulimfuata Saamiri hata wakati Nabii Musa (a.s.) alipokuwepo, na kwa vile Saamiri wala hakuwa njia mbadala, ilikuwa ni njia ovu lakini bado walimfuata tu. Pale ambapo *Wilaya* haikueleweka kwa Umma, wanawafuata kiupofu wale walio wachawi, walaghai na wadanganyivu kama Saamiri. Wanawafuata Anjuman (kikundi kidogo cha kiibada), Wadhamini, Mamwinyi, wamiliki ardhi na yejote yule mwininge lakini hawako tayari kumfuata kiongozi. Hii ilikuwa ndio hofu aliyokuwa nayo Mtukufu Mtume (saww) katika siku ya Ghadir, kwamba *Wilaya* itakuja kuwa ni mijadala ya kufurahisha na Umma utabakia hauna mfumo wa utawala.

Hivyo ni yapi yalikuwa mafanikio makubwa ya Imam Khomeini (r.a.)? Haikuwa kwamba alijifunza jambo kutoka kwenye kitabu fulani cha zamani na akaandika maelezo kwenye kitabu cha kiada na kukiwasilisha kama kitabu kingine kwa jina lake yeye. Hiki ndio kinachotokea, kwamba watu wanasona vitabu kisha wanayanakili yaliyomo humo kwenye vitabu vyao wenyewe vyta kiada, halafu kutoka kwenye kitabu cha kiada hadi kwenye vitabu vingine vilivyochapishwa na kutokana na vitabu hivi zinatengenezwa maktaba. Halafu maktaba hizi zinageuka kuwa makumbusho ya maktaba za zamani ambamo unaruhusiwa kutembelea tu na huruhuswi japo kugusa kitabu chochote humo.

Dini inageuka kuwa makumbusho ambayo yanakusudiwa kwa kuangaliwa na kusikilizwa. Inatubidi tupate dini kutoka kwenye maktaba, vitabu, vifua na akili na kuifanya iwakute watu kihali halisi majumbani. Ni lazima iingie kwenye maisha ya watu na ifike kwenye vitendo vyao. Dini ni jina la vitendo na sio la mijadala ya maneno matupu tu.

Imam Khomeini (r.a.) na wenzake walifanya kazi ya kiasi ambacho hakikufanywa wakati wa zama za Manabii (a.s.). Ilikuwa ni matamanio ya shauku ya mioyo ya Maimam wetu Watukufu (a.s.) kwamba kazi hii (ya kusimamisha dola ya Kiislam yenyen mfumo wa *Wilaya*) ifanyike lakini haikuwezekana kwa sababu Umma haukuwa tayari kwa ajili yake. Leo Allah ameutengeneza Umma huo ambao kwa mikono yao kazi hii imefanyika. Ni ahadi ya Mwenyezi Mungu kwamba kama hamtimizi wajibu wenu, Yeye ataleta Umma ambao utakuwa ni wenye kumpenda Mwenyezi Mungu na yeye Mwenyezi Mungu naye atawapenda pia. Na huu ni wajibu wetu wa kufanya majaribio ya kuwa Umma kama huo ambao unaweza kuleta mabadi-liko na mageuzi ya mfumo wa utawala.

Kila tunapoyatembelea makaburi ya Maimam wetu (a.s.) tunapaswa kujibu maswali mawili; moja ni kuhusu ni nini tulichokifanya mpaka kufikia sasa hivi, na jingine ni tunapanga na kudhamiria kufanya nini kuanzia sasa hivi. Wakati wote tunapokuwa mbele ya Maimam Ma'sum (a.s.) ama Viongozi wetu tunahitaji kujiangalia nafsini mwetu na kujiuliza ni nini tumekifanya hadi leo hii, wapi tumetumia ujana wetu na tutakapotambua kwamba tumeyachezea na kuyapoteza maisha yetu itatupasa kujisikia aibu. Kila nilichofanya hadi leo hakistahili hata kuzungumziwa, lakini leo nimekuja mbele yako ili kwamba uweze kunibadili na kunirekebisha. Ziarat ama kutembelea makaburi haya ya Mawalii kumelengewa kuwa mahali pa kugeukia katika maisha yetu.

Umma hauji kwa Maimam au viongozi wao kwa ajili ya kupoeteza wakati wao tu. Wanakuja kwa mambo mawili muhimu; moja ni kuwasilisha taarifa ya mishughuliko iliyopita, na la pili ni kuahidi juu ya shughuli na amali za baadaye. Taarifa zetu za yaliyopita sio nzuri sana lakini angalau itatubidi kuahidi kwamba kuanzia hapo tutafanya amali na mambo ambayo baadaye yataweza kufidia ile taarifa yetu mbaya ya yaliyotupitia.

Inatubidi kutoa ahadi kwa Maimam wetu (a.s.) na vilevile kwa mwakilishi wa Imam wa zama hizi (a.t.f.s.) kwamba tutaishi na tut-akufa katika njia ya *Wilaya*. Njia ambayo mmeionyesha ninyi (a.s.) na njia ambayo ameitekeleza Imam Khomeini ndiyo hiyo njia tutakayokanyaga sisi juu yake. Kama Khomeini anaweza kubadilisha mustakabali wa umma kwa nini sisi tusibadili wa kwetu? Kamwe tusiitekeze Ghadir kwa sababu kila pale ambapo watu waliacha Ghadir waligeuka kuwa watazamaji waliobweteka kimya, walijitenga na *Wilaya* na matokeo yake nyumba ya Zahra (a.s.) ikachomwa moto. Nyumba ya Fatima Zahra (s.a.) sio nyumba nyepesi iliyojengwa tu kwa magogo ya mitende; Nyumba yake yeye ni hii dini; nchi ya Zahra (s.a.) ni Uislam ambao leo hii unaungua moto. Leo hii Palestina inaungua moto, Lebanoni inaungua moto, Afghanistan, Kashmir zote zinaungua moto, na zote hizi ni nyumba za Zahra (a.s.), lakini kwa nini zinaungua? Kuna wahalifu ambao wameziwasha moto kwa sababu wengine wengi wamekubali kukaa kimya na kubweteka.

Wakati Imam Musa al-Kadhim (a.s.) alipoulizwa kuhusu ukomo wa mipaka ya Bustani ya Fadak; yeye (a.s.) akasema kwamba dunia yote hii, na hususan nchi za Kiislam zinakuja chini ya Fadak. Kama tutaendelea kubakia kimya leo hii, na tuseitekeleze wajibu wetu, basi nyumba ya Zahra (s.a.) itachomwa tena; Palestina, Lebanoni, Iraqi, Kashmir zitaungua tena. Leo hii Imam wa zama hizi (a.t.f.s.) anabisha hodi milangoni kwetu. Kulikuwa na siku ambapo Bi. Fatima

Zahra (s.a.) alikuwa akibisha hodi kwenye milango lakini hakuna hata mmoja aliyeufungua mlango, lakini mara tu ghafla wakaja kuuchoma moto mlango wake. Nyumba ya Zahra (s.a.) ndio Mfumo wa *Wilaya* ambao wengi wanajitahidi kabisa kujaribu kuuchoma moto.

## **MAAGIZO YA WALIU AL-FAQIIH NA KUMFUTA MARJAA MWINGINE**

Kuna swali linaloulizwa mara kwa mara la iwapo kwamba tunaruhusiwa kumfuata Marja'a mwagine katika mambo ya sharia badala ya Wilii al-Faqiih (Mlezi), au wakati akiwepo Wilii al-Faqiih tunaweza kumfuata Marja'a mwagine? Hebu ngoja nijaribu kilitatua suala hili kutoka kwenye misingi yake.

Mfumo halisi hasa ambao Mwenyezi Mungu ameusimamisha ni Mfumo wa *Wilaya*. Bila kujali zama za Utume, Uimam au kipindi cha ghaiba, katika kila zama kunakuwa na mfumo mmoja tu wa utawala uliowekwa na Mwenyezi Mungu na huo ni Mfumo wa *Wilaya*. Mfumo wa Kidini hauwezi kusitishwa kamwe katika zama yoyote ile, iwe ni kutokana na kufariki kwa Mtukufu Mtume (saww) au kwa ghaiba ya Imam wa Mwisho (a.t.f.s.). Haiwezekani kusitisha mfumo wa kidini na ile mipaka iliyowekwa na Mwenyezi Mungu. Huu Mfumo wa *Wilaya* ndio ulio safi halisi ambao watu wanapaswa kuuelekea, kuutwaa na kuishi maisha yao chini yake. Ambapo kwa upande mwagine ile hali ambayo tunakabiliana nayo leo hii ni ile ambayo kwamba, kuliko kuukubali mfumo huu, kuishi maisha yetu chini yake na kuutekeleza, sisi tuko tayari kukubali na kuijiveka sawa kwenye mfumo mwagine wowote ule unaolazimishwa juu yetu. Kwa kweli hasa, sisi tunajaribu pia kuifanya dini iwe yenye kunyambulika na kurekebishiwa kwa kufikia kiasi kwamba tunaihalalisha

hii mifumo inayobambikwa, eti iwe yenyé sura ya Kiislam! Juhudi tunazoziveka katika kujizoeza na kijiweka sawa na mifumo iliyopo sasa, ni nusu yake tu ambayo ingehitajika na kutosha kutekeleza ule mfumo halisi wa Mwenyezi Mungu.

Kwa mfano huko Iraqi sasa hivi, kiwango cha maisha yanayopotea na mauwaji ya halaiki yanayotokea huko yote ni kwa ajili ya kuafikiana na mfumo uliopo sasa. Hata nusu ya maisha haya mengi haitapotea iwapo wataamua kuvunja huu mfumo uliopo na kugeukia kwenye utekelezaji wa mfumo halisi wa utawala. Imam Khomeini (r.a.) alikuwa na utaratibu huo huo, wakati Shah alipowasilisha njia kadhaa za maafikiano kwa Imam Khomeini (r.a.) na akamtaka atoe madai yake na yeye Shah alikuwa tayari kuyatekeleza madai yake hayo na kufanya marekebisho na maafikiano katika mfumo uliopo, Imam (r.a.) alisema jambo moja tu, kwamba dai langu moja na hilo pekee ni kwamba inakubidi wewe uondoke hapa nchini. Kama Imam Khomeini (r.a.) angeafikiana na Shah wakati ule, hali ya Iran leo hii ingekuwa mbaya zaidi kuliko ile ya Iraq. Mfumo uliopo sasa kwa kiasi chochote utakavyofanya kazi haufai maafikiano wala marekebisho. Tunajaribu kuleta mnyumbuliko (flexibility) katika dini ili irekebishike na kuafikiana na mfumo uliopo sasa. Mfumo halisi hasi ni Mfumo wa *Wilaya* na Uimam. Kama mfumo huu haupo basi vilevile kwa hali na mazingira yoyote yale sisi tusijiweke sawa kwenye mfumo mwingine wowote wa utawala. Hata unapoziangalia sheria zote za kifqhi za Mujtahid wote huwa zinaelekeza kwenye mfumo wa *Wilaya*. Hakuna ubishani wowote hata kidogo, hivi ni vita vyatya kisaikolija tu ambavyo sisi hatupaswi kushindwa navyo, kama mtu ye yeyote anakuja na kusema kwamba utawala wa Kiislam, *Wilayatul-Faqih* ni jambo lenye utata, usisalimu amri na kuweka silaha zako chini. Mwanadamu anapaswa kuwa imara na aliyedhamiria angalau kwa

kiasi fulani kwamba anaweza kuchanganua na kuhakikisha utata wenyewe.

Tunaweza kuona dhahiri kwamba kuna fatwa kadhaa zinazohusiana na Mtawala wa Kisharia. Sheria zinazungumzia kuhusu wajibu wa Mtawala wa Kisharia katika mas'ala mengi, na katika sura za utakaso wa kiibada, Swala, Saumu, Hajj, na Zakat na kila ndani ya kila sura kwenye sehemu nyingi sheria hizo zinategemea kwa Mtawala wa Kisharia. Kama tukiwa mahali au nchi ambayo haina Mtawala wa Kisharia, ina maana kwamba hakuna serikali ya Kiislam inayotekelizwa hapo, na hakuna *Wilayatul-Faqiih* ingawa inaweza ikawa ni jamii ya Kiislam, hivyo katika hali kama hii mfumo mbadala ni ule wa Marjaa. Kwa hiyo katika zama na nyakati ambapo kuli-kuwa hakuna mfumo wa *Wilaya* uliokuwa unatekelezwa mahali pote, hapo mfumo huu wa Marjaa ulianzishwa ambamo tulirhusiwa kuwafuata wanachuoni hawa ambao walikidhi masharti fulani ya kidini ya kuwa wamethibitishwa kuweza kufuatwa.

Lakini wakati ule mfumo halisi wa *Wilaya* unapokuwepo, hapo huu mfumo mbadala hautumiki kwa maana ya moja kwa moja. Ni kama vile anapokuwepo Imam Maasum (a.s.) basi mfumo wa *Wilayatul-Faqiih* unakuwa haupo. *Wilayatul-Faqiih* ni mfumo mbadala wakati wa kipindi cha ghaibu, mpaka atakapodhihiri huyo Maasum (a.t.f.s.) anayesubiriwa. Kila mmoja, wakiwemo Mafaqiih, Marjaa, Wanachuoni na watu wa kawaida watakuwa wanamfuata yeye (a.t.f.s.) peke yake tu. Lakini kipindi Imam Maasum (a.t.f.s.) akiwa hayupo, basi wakati huu wa Ghaibu *Wilaya* inakuwa ni ya Faqiih, nayo hiyo pia kwa mipaka iliyoainishwa. Wakati kunapokuwepo na *Wilaya* ya Faqiih kila mmoja itambidi amkubali na kumfuata yeye hususan katika masuala ya kijamii. Lakini katika mambo binafsi na mas'ala ya ibada imeruhusiwa na Imam Khomeini (r.a.) na Kiongozi Mkuu mwenyewe kwamba unaruhusiwa kumfuata Mujtahid yoyote

mwenye elimu pana ya sheria za kidini. Imeanishwa wazi kwamba ufuasi lazima ufanyike kwa kumfuata Mujtahid ambaye anayo elimu pana ya kutosha juu ya vipengele vyote vya sheria ya kidini na sio yule Mujtahid mwenye taasisi ya utangazaji yenyne nguvu ya kueneza na kukuza jina lake. Na hili ndio linalotokea leo hii, kuna baadhi ya Mujtahid wazuri kweli lakini hakuna anayewafuata kwa sababu wao hawatangazwi na kuinuliwa. Marjaa hapaswi kujiwasilisha mwenyewe kwa watu; ni watu ambao wanalazimika kumtafuta *Marjaa* wa kumfuata katika mambo ya sharia. Wafuasi wanapaswa kumwendea Marjaa na wala sio Marjaa awafuate wafuasi au watu wake wa karibu waende kumtangaza Marjaa huyo kwa ajili ya kuwashawishi watu hao kumfuata.

Hivyo katika masuala yako binafsi na ya kiibada unaweza ukamfuata Marjaa yoyote yule, lakini katika mas'ala ya kijamii na ya kisiasa, katika yale masuala yanayohusiana na jamii kwa maana pana zaidi, utamfuata Wilii al-Faqiih. Katika mas'ala haya hata Marjaa analazimika kumfuata Walii al-Faqiih. Hivyo katika hili, kama Walii al-Faqiih akitoa amri ambayo sio fatwa yake kama Marjaa, ni lazima kwa mtu kutii amri hiyo. Kwa mfano, kama Walii al-Faqiih akitangaza Jihadi inakuwa ni wajibu juu ya kila mtu, hata kwa Marjaa. Na hili linakubaliwa na wanachuoni wote na Mafaqih, na katika utaratibu pia wanachuoni na Mafaqih wanatoa maoni yao katika mambo ya kibinafsi lakini katika mas'ala ya kijamii wanatutaka tumrejee Walii al-Faqiih. Huu ni mfumo kamili ambamo hata Marjaanakuja chini ya Walii al-Faqiih. Hata katika uhai wa Imam Khomeini (r.a.) kulikuwa na wengi wa wafuasi wake ambao walikuwa wakimfuata yeye kama Marjaa na pia wengine wakiwafuata Marjaa wengine, lakini hii ilikuwa ni kwa sababu Imam Khomeini (r.a.) alikuwa ametoa ruhusa ya kumfuata yoyote kama Marjaa katika mas'ala ya Fiqhi.

## MLANGO WA TATU

### **ATHARI YA MIFUMO YA UTAWALA ISIYO YA KI-MUNGU JUU YA JAMII**

### **MFUMO WA KIISLAM NA MIFUMO MINGINEYO YA KIJAMII**

Hapa ndipo ambapo dini inatenganishwa na siasa. Mfumo wa kijamii ambao unazaliwa kutoka kwenye tumbo la siasa unalenga tu kupata ukamilifu katika vile vikwazo (parameters) vya maisha vinavyohusiana na mahitaji ya kimwili ya mwanadamu ya siku hadi siku. Kama vile kuna mfumo katika jamii ambao unasimamia msongamano wa magari katika mitaa ili kuepuka vurugu kwenye barabara za mji. Jambo la kutafakari hapa ni kwamba hata maono yasiyo ya kidini, mawazo na mashule yanaamini katika mfumo wa kijamii kwa ajili ya wanadamu, lakini hilo ni kwa ajili tu ya kutimiza mahitaji ya kimwili ya mwanadamu ya kila siku, kuepuka vurugu, mapigano, wasiwasi na kuwazuia binadamu kutumia mabavu katika kuchukua haki za kila mmoja wao na mwингine.

Lakini ule mfumo ambao Allah ameuanzisha kwa ajili ya mwanadamu sio wa kudhibiti tu maisha yake ya kila siku bali ni wa kuhakikisha kwamba mwanadamu anapata kuelimika kiroho na ana-pata ukamilifu wake kwa msaada wa mfumo huu. Kwa hiyo mfumo aliouanzisha Mwenyezi Mungu na kuwafanya wanadamu wautenge-mee juu yake, na mfumo ambao upo katika mwendano na mahitaji

ya msingi ya mwanadamu na uhai wake. Si mfumo ambao umelengea tu katika mahitaji ya muhimu ya maisha, kutimiza matamanio ya mwanadamu, kuzuia vurugu na kutoa ulinzi kwenye hatari. Lengo kuu na la msingi la mfumo wa kijamii ni kutengeneza mazingira kwa ajili ya ukuaji na ukamilifu wa mwanadamu katika muundo wake wa kiroho. Mfumo huu wa kijamii au kiutawala katika Uislam una-julikana kama mfumo wa Uimamu na Umma (Uongozi na Umma), au unaojulikana pia kama Mfumo wa *Wilaya*. Huu ni mfumo uli-otengenezwa kwa ajili ya maendeleo ya kijamii ya wanadamu, sio kwa ajili ya mtu mmoja tu, bali katika muundo wa mjumuiko wa kuipeleka jamii katika ukamilifu wake.

Hapa ndipo ambapo tofauti kati ya Mfumo wa *Wilaya* na mifumo mingine ya kijamii inayopingana nao inapodhihirika wazi kabisa. Tofauti kati ya mifumo yote mingine kwa ajili ya jamii kama ikilanganishwa na Mfumo wa *Wilaya* inakuwa katika misingi yake mikuu. Wasomi wanairejea hii tofauti ya msingi kama tofauti katika kiini. Hii ina maana kwamba tofauti iko kwenye chimbuko na sio katika sifa. Ni makosa kusema kwamba kimsingi mifumo yote ni sawa, lakin tofauti zipo tu katika utekelezaji au katika sifa zake. Chimbuko la mfumo wa kijamii wa kidini na ule mfumo usio wa kidini wa utawala wa kijamii ni tofauti. Tofauti yenye ni kufikia kiwango cha tofauti kati ya wanadamu na viumbe visiviyokuwa wanadamu, kati ya mwanadamu na mti. Kufanana na hili, Mfumo wa *Wilaya* na mfumo wa demokrasia iko tofauti kabisa; Mfumo wa *Wilaya* na mfumo wa kidikteta iko tofauti kabisa pia.

Mahitaji hasa ya mfumo, uwe wa *Wilaya* au mwengine wa kuten-genezwa na binadamu yanaweza kutambulika pale tu mwanadamu atakapoelewa chimbuko au uhalisia wa nafsi yake. Wakati mwanadamu atakapoeleweka kwa maana yake halisi, hapo ndipo tutakapotambua iwapo kama tunahitaji Mfumo wa *Wilaya* ama mifumo

mingine ya kuongoza jamii yetu. Qur'ani pia inazungumzia jambo hilihili katika muktadha pamoja na simulizi ya kisa.

## **QURAN TUKUFU - CHANZO CHA MUONGOZO**

Qur'ani Tukufu ina mkusanyiko wa visa vilivyosimuliwa kwa Mitume, Umma na jamii mbalimbali. Kwa kusema kweli visa vyote hivi vina seti ya mkusanyiko wa masomo ya mwongozo na elimu kwa ajili ya wanadamu. Lengo letu linapaswa liwe ni kuyapata masomo hayo ya mwongozo kuititia visa hivi. Lengo hili linaweza kuthibitishwa kwa ule ukweli kwamba Qur'ani yenyewe inasema kuwa Yenyewe ni Kitabu cha Mwongozo.

هُدَى لِلْمُتَّقِينَ

“.....ni uwongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu.” (2:2)

Na mahali pengine inasema:

شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنْزِلَ فِيهِ الْقُرْءَانُ هُدًى لِلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنْ  
الْهُدَى وَالْفُرْقَانِ

“Ni mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa katika (mwezi) huo Qur'ani, kuwa mwongozo kwa watu na upambanuzi.....” (2:185)

Hivi ndivyo ambavyo Qur'ani imejitambulisha yenyewe kama Kitabu chenye mwongozo makhsusi kwa wachamungu na mwongozo wa jumla kwa wanadamu wote. Kama Qur'ani Tukufu ni kitabu cha mwongozo kwa mwanadamu; basi kila kile kilichomo ndani yake ni kwa ajili ya mwongozo tu na sio kwa lengo jingine lolote. Tumeshughulika na Qur'ani kwa namna ya kuikosea adabu kabisa kwa kiasi kwamba Qur'ani yenyewe itakuja kulalamika kuhusu hili. Siku hizi kuna wale makafiri ambao wanainajisi Qur'ani kwa kuitupa kwenye mabomba ya maji machafu mabafuni, bali zaidi ya hao, Qur'ani italalamika dhidi yetu sisi kwa unyanyasaji tuliofanyakia Kitabu hiki Kitukufu. Hii ni kwa sababu wale makafiri ambao waliinajisi Qur'ani walikuwa wajinga, hawakuja chochote kuhusu umuhimu na hadhi ya Kitabu hiki. Bali sisi ndio warithi wa Kitabu hiki. Tumeifunika Qur'ani katika majalada mazuri ya nguo na hatuifungui na kuisoma. Hili ndio tusi kubwa kwa Qur'ani kwamba wafuasi wake hawaifungui, hawana habari nayo, hawaisomi na baya zaidi ni kwamba kuna wengi ambao hawajui hata jinsi ya kuisoma. Imo katika hadith pia kwamba fedheha kubwa ya mwanachuoni sio kwamba apigwe mawe, atukanwe na ashutumiwe bali fedheha iliyo kubwa sana na matatizo kwa mwanachuoni ni kwamba yeze yumo katika jamii na hakuna hata mtu mmoja anayefaidika kutokana na elimu yake. Hivyo kilele cha matatizo ya Amirul-Mu'minin (a.s.) ilikuwa kwamba alikuwa akiwakaribisha watu kuja kumuuliza maswali lakini wao walikuwa wakimpuzzia, hawakuongeza elimu yao kupitia kwake, hawakujishughulisha na kuondoa ujinga wao kupitia yeze. Walikuwa na kila aina nyingine ya shughuli pamoja naye mbali na uchukuaji wa elimu kutoka kwake, na hii ilikuwa ni dharau kubwa kwenye shaksia yake.

Hali kadhalika, Qur'ani ni Kitabu cha mwongozo na chenyewe kina uongofu ndani yake. Hiki sio kitabu cha “*Istikhara*.” Kwa vile

mada iliyoko kwenye mjadala sio Qur'ani Tukufu, hivyo mimi natoa baadhi ya viashirio muhimu kuhusu hili, lakini kuwa na uhakika kuhusu yale tunayoyachukulia na kufikiri juu ya Qur'ani, si chochote kinginecho zaidi ya kuwa ni Kitabu cha mwongozo tu. Sio kitabu cha kutafutia thawabu kwa visomo vya sauti tu. Allah hakuishusha Qur'ani kwetu sisi ili kwa ajili ya kujikusanya thawabu nyingi kiasi iwezekanavyo. Haikuwa kana kwamba Mwenyezi Mungu alimpa Jibril Qur'ani kumletea Mtukufu Mtume (saww), ili kwamba Yeye awaelekeza zaidi watu kwenye thawabu zitokanazo na visomo vyao. Tunaandaa sherehe za usomaji wa Qur'ani kwa ajili ya kutafuta thawabu. Mfano wa kwenye hili ni wakati tunapotaka kugawa au kukanibisha watu kwa ajili ya kupata chakula tunaandaa Majlisi, au mpango wa kimuujiza wa usomaji wa Qur'ani kuufanya iwe ni njia ya kugawa chakula. Kana kwamba Mwenyezi Mungu anataka kugawa thawabu na hivyo aliumba Qur'ani ili watu waisome na kupata thawabu. Lengo la kuambatanisha thawabu na Qur'ani linahusiana na lengo la uumbaji, ambapo Allah anatutaka sisi tupate mwongozo, tupate utakatifu na kuwa na nidhamu. Qur'ani Tukufu ndio njia ya kuyafikia mambo haya muhimu kwa ajili ya maisha yetu na hivyo kuna thawabu zinazoambatana na usomaji wake, ili kwamba kama sio dhahiri kabisa kwa ajili ya mwongozo, basi angalau kwa ajili ya kupata thawabu tutakuwa tunaisogelea karibu hiyo Qur'ani.

Kuna matendo kadhaa wa kadha yafanywayo kwa lengo la kuwawutia wengine kwenye malengo ya hali ya juu nyuma ya hayo matendo ya utangulizi. Tukirejea kwenye mfano huo huo wa ugawaji wa chakula kwenye Majlisi, mara nyingi tunapokuwa hatuna uhakika na mahudhurio mazuri kwenye Majlisi, basi tunatangaza rasmi kwamba baada ya Majlisi kutakuwa na chakula kitakachoandaliwa. Hili linatuhakikishia ukusanyikaji wa hadhara kubwa ya watu ambao hata kama watakuja kwa ajili ya chakula, bado watasikiliza hotuba

ambayo itakuwa ni njia ya mwongozo kwao. Allah aliweka mwongozo kwa ajili ya mwanadamu na sambamba na hili Yeye amesema kwamba kujihusisha kwenu na chanzo hiki cha uongofu kunakuwa na uhakika. Lakini mtazamo wetu kwenye Qur’ani ni kuifungua tu na kuisoma kwa ajili ya thawabu bali sio pamoja na lengo la kupata mwongozo kutoka humo. Kitabu cha Mwongozo bila kukielewa hakina maana, lakini kitabu cha thawabu ima ukielewa au usikielewe bado utapata thawabu. Hivyo ni juu yetu sisi kuamua ni jinsi gani tunataka kushughulika na Qur’ani, kama kitabu cha mwongozo au kitabu cha thawabu. Endapo ni kama kitabu cha mwongozo, basi tunahitaji kutafakari juu ya aya zake na hivi visa vyake ili kuielewa. Qur’ani ina kila kitu ambacho kinahusiana na maisha yetu ndani yake, lakini tunatoa umuhimu zaidi kwenye Qur’ani baada tu ya kifo. Kama mtu hataweza kupata chochote kutoka kwenye Qur’ani wakati wa uhai wake, kwa kweli kabisa hatakuja kupata chochote kutoka kwenye kitabu hiki baada ya kufariki kwake pia. Tumechagua Sura chache kama vile Yasiin na Rahmaan ambazo zina thawabu nyingi zaidi; tunazisoma siku zote kwa ajili ya kupata hizo thawabu zake tu.

## WANA WA ISRAILI NA MFUMO WA FIRAUN

Tukirejea kwenye mada yetu, Qur’ani Tukufu imechukua njia nyingi tofauti za kuwasilisha masomo ya uongofu ndani yake. Mionganii mwa hizi, njia moja ni kupitia usimuliaji wa visa vya watu mbalimbali, Manabii, zama na Umma. Moja ya visa ambavyo Qur’ani inavisimulia ni kuhusu kisa cha mwongozo wa Nabii Musa (a.s.) kwa Umma wake. Mwenyezi Mungu alimnyanyua Nabii Musa (a.s.) kwa ajili ya kuwaongoza Bani Israil kwa vile wao Bani Israil walikuwa wanaishi maisha yao chini ya mfumo wa utawala ambao ulikuwa

haufai, wa hatari, wa kiharibifu na wa kidhalimu unaokataza maendeleo ya maadili ya kibinadamu na kuzuia ukamilifu. Haikuwa tu kwamba mfumo huo ulizuia ukuaji wa mwanadamu huyu wa minofu kuwa mwanadamu kwa asili yake (yaani kupata ukamilifu), bali badala yake ulikuwa ukimshusha hadhi mwanadamu na kumfikisha kwenye hali duni ya chini kabisa, kama ile ya wanyama. Qur'ani Tukufu imeuita mfumo huu kama Mfumo wa Bani Israil. Walikuwa wakiendesha maisha yao chini ya mfumo huu wa Kifirauni.

Kuanzia mwanzo kabisa wa Qur'ani katika Surat al-Baqarah, kisa cha Bani Israil kinaanzia hapo. Wao walikumbushwa na kuambiwa:

يَبْنِي إِسْرَائِيلَ أَذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ .....

**Enyi wana wa Israil! Kumbukeni neema yangu niliyowaneemesha:  
.....” (2:40)**

Na halafu Qur'ani inaendelea kusema:

وَأَنِّي فَضَّلْتُكُمْ عَلَى الْعَالَمِينَ

**“..... na hakika nimewafadhilisha kuliko viumbe wengine.” (2:122)**

Halafu mionganoni mwa neema ambazo Qur'ani imezihesabu, ya kwanza ambayo wao walikumbushwa ni:

وَإِذْ تَحْيِنَّكُمْ مِنْ ءالِ فِرْعَوْنَ

**“Na tulipowaokoa kwa watu wa Firaun. ....” (2:49)**

Hii ina maana kwamba tuliwatoeni kutoka kwenye ukatili na matatizo mliyokuwa mkikabiliana nayo katika mfumo wa utawala wa Kifirauni. Hili linazingatiwa na Qur’ani kama neema kubwa kabisa waliyopewa Bani Israil.

Bani Israil walikuwa wakiishi maisha yao chini ya mfumo wa Kifirauni huko Misri, ambako watu wa Misri walikuwa wamegawanyika katika koo kuu mbili. Moja ikiitwa “Sibti” na nyagine ikiitwa “Qibti.” Wa-Qibti walitokana na kabile la Firauni, ambapo Wa-Sibti walikuwa wa kizazi cha Nabii Ya’qub (a.s.) na Yusuf (a.s.), yaani kutoka kwenye familia ya Manabii, au kwa istilahi ya kileo, wote walikuwa ni “Masayyid.” Nabii Ya’qub alikuwa na watoto kumi na mbili, wote ni ndugu zake Nabii Yusuf (a.s.). Walikwenda nchini Misri na kuanzia huko kizazi chao kikaanza kujulikana kwa jina la “Sibti.” Tunahitaji kumakinika na kutafakari juu ya nukta moja muhimu hapa. Hawa wote walikuwa wanatokana na kizazi cha Manabii maarufu sana kama Ibrahim, Isma’il, Is’haaq na Yaq’ub. Wahenga wao walikuwa ni hawa Manabii mashuhuri kabisa na kwa hiyo wao walikuwa ndio Masayyid wa zama zile. Bani Israil waligawanyika katika makabila kumi na mbili na kila kabile lilikuwa na mamia ya maelfu ya watu, lakini kwa bahati mbaya Masayyid hawa walishi maisha yao chini ya mfumo wa Kifirauni. Qur’ani inasema kwamba huo Mfumo wa Kifirauni ulikuwa ndio mfumo mbaya kabisa juu ya ardhi kwa ajili ya mwanadamu tangu mwanzo wa dunia. Kulikuwa na maovu makuu mawili katika mfumo huu, moja ambalo limeelezwa na Qur’ani kama:

يُسْوِمُونَكُمْ سُوءَ الْعَذَابِ

“.....wanawapeni adhabu mbaya.” (2:49)

Hii ina maana kwamba umma mzima ulikuwa unaburuzwa kuelekea kwenye adhabu kali. Wakati mwagine, serikali au mfumo ambamo mwanadamu anaishi maisha yake, mfumo huo unaiburuza jamii, ummah na nchi nzima kwenye maangamizi (yaani adhabu). Tunaweza tukaiita mifumo hiyo kama Mifumo ya Jahannam au mifumo ya kidhalimu. Sasa inatubidi tuchukue mwongozo kutoka kwenye maelezo ya Qur'ani Tukufu.

## **UHUSIANO WA KIHENGA HAUKUHAKIKISHII ULINZI**

Katika jamii yetu leo hii, baadhi ya watu wanajiita wenyewe kama ni Waislam, Shi'ah, Masayyid, Ja'fariy, Kadhimiy, Hashmiy na wafuasi wa Dini ya Kiislam. Sote tunayo hii hadhi ya kihenga kama vile tu kwa Bani Israil kwa uhusiano wetu kupanda hadi kwa watu mashuhuri, lakini inatubidi kuona kwa maana halisi ya kiutendaji ya ile aina ya mfumo inayotawala maisha yetu. Hili ni muhimu sana katika mwanga wa Qur'ani kama ilivyotajwa kabla. Ili kuifanya nukta hii ieletekele vizuri, ngoja nichukue baadhi ya mifano hapa. Kama kwa mfano Sayyid mmoja mashuhuri na mwenye uchamungu na kuheshimika amekaa juu ya farasi, ambaye sio wa kufugwa na anamwendesha kuelekea kwenye bonde zito, kwa sababu tu yeye ni Sayyid ajali hii kwa kawaida itaepukika? Tusije tukadhani kwamba ajali huwa haziwatokei Masayyid na Mashah. Ajali huwa zinawatokea Masayyid na Mashah na watu wa ngazi za juu pia. Mtu anaweza kuwa anatokea kwenye familia nzuri, familia yenyeheshima lakini kwa wakati huu hilo gari analoendesha linashuka kuelekea kwenye bonde zito. Uhusiano wake na familia nzuri hautamlinda na mwisho mbaya ambao karibu atakutana nao ndani ya gari hii. Kadhalika wakati mwagine wanadamu wanakuwa na uhusiano mzuri

sana, yeye ni Mwislam, pengine ni bingwa wa Qur'an pia na mfuasi wa Maimam Maasum. Mahusiano yote haya na sifa ni mazuri katika maana halisi, lakini ule mfumo alioukubali kwa kuendeshea maisha yake unaweza bado ukawa unamchukua na kumwelekezea kwenye bonde la Jahannam sawasawa na ile gari.

Tunahitaji kufikiri kwa makini kabisa ni mwelekeo gani mfumo wetu wa utawala unakotuelekezea? Huu Mfumo ambamo sisi tunaendeshea maisha yetu, je ni wapi unakotupeleka sisi, familia zetu, watoto wetu na jamii yote nzima? Inaweza kuwa ni sawa na ile “**wanawapeni adhabu mbaya**” ambayo ina maana kwamba wote wamekaa ndani ya gari ambalo linaonekana kuwa zuri sana lakini linawapeleka kuelekea Jahannam. Hivyo ni muhimu juu yetu sote kufikiria na kuona ni mfumo gani unaotuendesha sisi, tuko kwenye mikono ya nani na inatuchukua kuelekea wapi.

Jukumu la serikali sio tu kuandaa chakula kwa ajili yetu sisi, kuanzisha mfumo wa utaratibu wa magari barabarani, kujenga mashule na vyuo vikuu tu, na wajibu wetu sisi pia sio wenye kuishia kwenye kupiga kura kuchagua serikali. Dini ina mawazo tofauti juu ya mfumo wa serikali. Serikali ni kama garimoshi ambalo wote tumepanda humo na tunakwenda safari fulani. Hivyo kabla ya kupanda garimoshi hili ni bora kwanza tutathmini ni wapi lina-kotupeleka sisi, ni kuelekea kwenye wokovu au kuelekea kwenye maangamizi? Badala ya kupata masomo kutoka kwenye visa hivi vinavyosimuliwa na Qur'an Tukufu ambavyo ni kwa ajili ya mwongozo wetu, sisi tumevitumia hivi kwa ajili ya utamaduni wa usomaji usio na mazingatio. Soma aya hizi na kisha utafakari:

يَبْنَىٰ إِسْرَائِيلَ أَذْكُرُوا بِعَمَّتِي الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ .....

**“Enyi wana wa Israil! Kumbukeni neema yangu niliyowaneemesha:  
.....” (2:40)**

**وَإِذْ نَجَّيْنَاكُم مِّنْ ءالِ فِرْعَوْنَ**

**“wanawapeni adhabu mbaya” (2:49)**

Aya hizi sio kwa ajili ya kupatia thawabu; badala yake ni kwa ajili ya kufungua macho. Aya hizi zinatutaka sisi kwanza na muhimu kabisa tuone jinsi Bani Israil licha ya kuwa wanatokana na kizazi cha Manabii, walikuwa wanaishi katika mfumo ambao ulikuwa unawaelekeza Jahannam. Na kwa bahati mbaya kabisa, sisi tunazisoma tu aya hizi kwa ajili ya thawabu na wala hatuufikirii ule ujumbe ul-iowekwa ndani ya aya hizi.

## **DU’A YA ARAFAH NA MFUMO WA WILAYA**

Huu ndio ulikuwa ni ujinga wetu juu ya Qur’ani, sasa tukija kwa Maimam Maasum ambao kwao sisi tunadai kuwa na mapenzi ya hali ya juu, tuna utambuzi kiasi gani kuwahusu wao? Mapenzi yetu kwao ni yasiyopimika, bali maarifa yetu kuhusu wao ni machache sana, kwa kweli haitakuwa ni kutia chumvi hata kusema kwamba hakuna utambuzi kabisa. Kama tukichukua nukta hiihii ya mjadala kuhusu huo mfumo wa utawala, tunaweza kuthibitisha zaidi hitimisho letu kutoka kwenye aya ya Qur’ani chini ya mwanga wa Du’a ya Arafa. Hii Du’a ya Arafah ni maombi ambayo yanakusanya mambo mengi ya msingi katika muundo wa du’a na maombi. Maimam wetu Watukufu (a.s.) wamefanya mpango madhubuti sana kwa ajili

ya kutoa na kuhifadhi mafundisho yao kwa ajili ya vizazi vijavyo. Wamewasilisha mafundisho yao katika miundo mitatu tofauti; mengine katika muundo wa hadith na riwaya, mengine katika muundo wa Du'a na maombi ya minong'ono (Munajaat). Na yaliyobakia katika muundo wa Ziyarat. Hali yetu ni ya kutisha sana kiasi kwamba kwanza kabisa hatuzigusi hizo hadith, tunasoma du'a wakati mwingine pale mtu anapokuwa anaumwa au kuna mabalaa fulani makubwa, na kuhusu Ziyarat tumeweka nyakati maalum kama vile wakati wa Ashura ambapo hapo tunaziangalia Ziyarat hizi. Kwa kweli haya ni mambo ambayo yanapaswa kuwa ni sehemu ya mai-sha yetu kuanzia asubuhi hadi jioni, lakini kwa bahati mbaya haya yamegeuka pia kuwa kama visomo vya kitamaduni tu. Du'a hizi sio nyuradi za Masufi. Kulingana na Allamah Iqbal, ile dini iliyotufikia sisi ilikuwa tofauti. Tumeibadilisha dini hiyo na kuwa Dini ya baraza la Sufi. Katika mabaraza ya Sufi hakuna chochote isipokuwa vipindi vya nyuradi zisizo na maana, ambako Masufi, na wale wenye raghba na hisia kali wanakaa pamoja katika vikundi na kufanya visomo vyao, na baadaye visomo hivi vinapata kasi ya nguvu na kugeuka kuwa namna fulani ya mtingishiko wa kimwili.

Isije kuwa kwamba tunatengeneza Shule za Kidini (Madrassa) na kuanza kufanya visomo vya mdomo vya du'a hizi, tunaandaa Majlisi za maombolezo na humo pia tunaishia na visomo visivyo na mazingatio, tunaandaa mikusanyiko binafsi vilevile kwa ajili ya visomo kama hivyo. Du'a hizi sio kwa ajili ya visomo vya kupatia thawabu kama hivyo tu, bali kwa kweli du'a hizi zina mukhtasari wa mafunzo ya vitendo kwa ajili ya maisha yetu. Du'a hizi zimebarikiwa kuwa na kiwango cha utambuzi juu ya Allah ambacho kimekuja tu kupitia wahyi kwa hawa watu Maasum. Na watu hawa nao wakaandaa mpangilio kama huo kwa ajili yetu wa kuhamishia ufahamu huo katika muundo wa du'a na Ziyarat zilizorahisishwa vizuri kabisa.

Du'a ya Arafah ni moja ya du'a zenyé thamani sana, muhimu na yenye maana sana ambayo tunaisoma mara moja tu kwa mwaka (mnamo Siku ya Ashura – mwezi 9, Dhil-Hajj). Kwa kweli wengi wetu wala hatujui ama hatujasikia lolote kuhusu du'a hii pia. Du'a hii ambayo imo ndani ya Mafatih imekuja kutoka kwa Mkuu wa Mashahidi Imam Husein bin Ali (a.s.). Hii ni namna ya kito cha thamani kabisa ambacho hakuna maneno yanayoweza kupatikana kuweza kuelezea umashuhuri wake mkubwa. Ndani ya Du'a hii, baada ya kumdhukuru Mwenyezi Mungu na kuzihesabu fadhila Zake, Imam Husein (a.s.) anaonyesha shukurani zake juu ya neema na fadhila ambazo Allah amemjaalia yeye binafsi. Yeye (a.s.) alizigawanya fadhila hizi katika mafungu namna tatu. Fungu la kwanza ni zile fadhila ambazo alizipokea kabla ya kuzaliwa kwake, la pili ni zile fadhila ambazo ni za wakati wa kuzaliwa kwake na la tatu ni zile alizojaaliwa baada ya kuzaliwa kwake.

Ni dhahiri kwamba tutakuwa ni wenye hamu sana kutaka kujua ni fadhila zipi zote hizo ambazo alizawadiwa yeye katika awamu hizi tatu za mazazi yake, na Mungu akipenda, kama utafanya uchunguzi wa du'a hii basi utazikuta. Nia yangu sio kufanya sherehe na mael-ezo juu ya du'a nzima hapa. Ninataka tu kupata usikivu wenu kueleke kwenye fadhila moja ambayo inahusiana na somo la mjadala wetu. Yeye anasema: "Ewe Allah, mimi ninakushukuru kwa mpango uliyofanya kwa ajili ya kuzaliwa kwangu." Huu ulikuwa ni mpango gani? Yeye anasema "mpango mmoja ulikuwa ni kwamba Wewe umenileta mimi hapa duniani kuititia utakasifu wa wazazi wangu Maasumin, na mpango mwingine ulikuwa kwamba ulichelewesha kuzaliwa kwangu mpaka pale ardhi nitakayozaliwa mimi ilipokuwa imetakaswa kutohana na kufuru na ushirikina, pale ambapo serikali ya Kiislam ilipokuwa haijaundwa na mfumo Wako Mtukufu hau-jatawala mahali pa kuzaliwa kwangu. Wakati ardhi Yako, yaani Ma-

dina, ilipotakaswa kutokana na ukafiri na mfumo wa Kiislam wa serikali uliposhika nafasi, hadi wakati huo ulikuwa hujaruhusu kuzaliwa kwa Husein kutokea katika ardhi ile.

Mkuu wa Mashahidi anauchukulia uanzishwaji wa mfumo wa utawala wa Kiislam kama ni fadhila kwa ajili ya kuzaliwa kwake na anamshukuru Mola Wake kwa zawadi hii kubwa. Inatubidi tutambue hapa kwamba ye ye huyu ni Maasum, ambaye ameepukana na aina zote za uchafu. Maasum ni Maasum tu bila kujali mazingira ambamo amezaliwa na anamoishi. Licha ya kuwa Maasum, anakichukulia kitendo cha kuzaliwa kwake kwenye ardhi ya utawala wa Kiislam kama ni zawadi kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Tutakuwa tunatambua kuhusu ukweli huu wa kihistoria kwamba Imam Husein (a.s.) alizaliwa katika mji wa Madina na mazazi yake yalitokea katika wakati ule ambapo Mtukufu Mtume (saww) alikuwa ameanzisha na kutekeleza mfumo wa utawala wa Kiislam ndani ya Madina. Tunapaswa kujiuliza swali hili la ni kwa nini Mtukufu Mtume (saww) na Imam Ali (a.s.) walihama kutoka Makka. Kwani Makka ilikuwa ni Mji Mtukufu ambao ulikuwa na Masjidul-Haram, msikiti ulio mtukufu kuliko misikiti yote, ulikuwa na ile Ka'ba Tukufu, lakini mbona bado Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipokea maagizo ya kimungu ya kuhama kutoka Makka na kwenda Madina? Majibu ya hili ni kwamba, ingawa Makka kwa hakika ilikuwa na makumbusho yaliyotakasika na matukufu kama vile Ka'aba Tukufu, lakini mfumo uliokuwa ukitawala mji ule ulikuwa ni mfumo wa ukafiri na ibada ya masanamu. Ulikuwa ni mfumo wa Abu Jahal na Abu Lahabi. Hili linathibitisha hoja yetu kwamba, hata kama ni ardhi tukufu yenye maeneo matakatifu, lakini kama haina mfumo wa haki wa serikali ya kimungu, basi itawaelekeza watu wanaoishi humo kwenda Jahan-nam. Hivyo Mtukufu Mtume (saww) alipata amri ya kuhama humo pamoja na wafuasi wake na familia yake na kuelekea Madina. Ali-

hama kwa sababu mfumo huu ulikuwa haustahili kuishi ndani yake na yeze alitaka kuubadilisha mfumo huo. Asingeweza kuubadili mfumo huo akiwa bado anaishi Makka, kwa hiyo alikwenda Madina ambako ilikuwa ni rahisi zaidi kuanzisha serikali ya Kiislam, ambapo alifanya hivyo na kisha hatimaye akaubadilisha ule mfumo wa Makka pia. Sasa, Makka haikubakia tena kuwa hekalu la masanamu, iligeuka kuwa Qibla cha ibada kwa ajili ya Waislam wote.

Hivyo katika kuhitimisha nukta hii, umuhimu wa kuishi maisha katika serikali ya Kiislam umesisitizwa kwa uwazi na dhahiri kabisa katika mafundisho ya ndani ya Qur'ani na yale ya Maasumin (a.s.).

## SIFA YA KWANZA YA MFUMO WA KIFIRAUNI

Qur'ani Tukufu iliuwasilisha ukweli halisi wa mfumo wa Kifiraun. Hatuwezi kukanusha kwamba Firaun alikuwa na mfumo wa utawala ulioundwa vizuri ambao ulikuwa ukitoa mahitaji muhimu ya maisha kwa watu. Walikuwa wakipata chakula, maji, wakishughulika ndani ya soko, kulikuwa na mfumo wa uhamasishaji kwa njia ya farasi, ngamia na merikebu, watu walikuwa wakipata kazi, walikuwa wakipata pesa, na walikuwa wakioana wakiwa bado ni watoto. Mambo yote haya yalikuwa yakinkeza katika mfumo wa Kifirauni, lakini pale Qur'ani ilipotoa picha ya mfumo huu wa kifirauni ilisema:

وَإِذْ نَجَّيْنَاكُم مِّنْ ءالِ فِرْعَوْنَ يَسُوْمُونَكُمْ سُوءَ الْعَذَابِ

“Na tulipowaokoa kwa watu wa Firaun waliowapa adhabu mbaya;  
.....” (2:49).

Hii maana yake ni kwamba, kumbukeni ule mfumo ambamo mlikuwa mkiishi maisha yenu, na kumbukeni kwamba tulikupeni uhuru na ukombozi kutoka kwenye mfumo ule ambao ulikuwa ukielekezeni Jahannam. Hii Qur’ani Tukufu ni Kitabu ambacho ki-meelezea tukio hili kwetu sisi ili tupate kufikiri na kutafakari kwa makini zaidi juu ya mfumo ambamo sisi tunayapitisha maisha yetu, kuchunguza na kuona ni wapi mfumo huu unakotupeleka. Qur’ani inatutahadharisha sisi tuchunguze na kuona ni treni gani uliyopanda au ni mashua gani unasafiri nayo. Pengine mashua hii inakukokota kukuingiza kwenye tufani. Huu mfumo wa serikali ambao unatutawala sisi na maisha yetu unaweza ukawa unatupeleka kwenye moto wa Jahannam. Wakati mwagine watu wanaosafiri katika mashua wanaweza wakawa ni watu wa dini na wachamungu hasa, lakini mashua yenyewe inasafiri kuelekea kwenye dhoruba. Sasa wote hao wataishia ndani ya dhoruba hii licha ya uchamungu wao na ibada zao. Bila kujali kwamba wewe ni mwema au muovu, kama mfumo wenyewe unaelekea kwenye maangamizi, hatima yako itakuwa sawa na hiyo ya mfumo wenyewe.

Ni wapi inakoelekea mifumo hii ya kidunia? Hii ni ile mifumo ya ki-Yazid na kwa nini Imam Husein (a.s.) akaanzisha vuguvugu la kuung’oa mfumo huu? Hii ilikuwa ni kwa sababu kwamba watu waliokuwa wanaishi chini ya mfumo huu wa utawala wa Yaziid walikuwa ni watu wa dini, walikuwa wakiswali, wakifunga na kwenda Hijja, lakini mfumo huu ulikuwa ukielekea Jahannam. Swala na Hijja zao zisingeweza kuwaokoa kutokana na mfumo huu ambao ulikuwa unawapeleka kuelekea kwenye maangamizi. Kulikuwa na haja kubwa ya kuuvunja mfumo huu wa kiliberali usio na fungamano maalum, ili kuwa huru kutokana na mfumo huo na kuwafanya watu watambue kuhusu mambo maovu ya mfumo huu. Hii ndio sababu ya kwa nini alianzisha vuguvugu lake hilo, akatoa kafara la watoto

wake, familia na masahaba zake. Aliwachukua wanawake pamoja naye ili aweze kuuambia ulimwengu kwamba huu sio mfumo ambao tutakubali kuishi maisha yetu yote. Hii ilikuwa ndio sifa ya kwanza ya mfumo wa Kifiraun ambamo umma mzima unachukuliwa kuelekea kwenye maangamizi ya milele (Jahannam).

## SIFA YA PILI YA MFUMO WA KIFIRAUN

Sifa ya pili ya Mfumo wa Kifiraun kama ilivyoelezwa na Qur'an Tukufu ni:

**يُذَكِّرُونَ أَبْنَاءَكُمْ وَيَسْتَحْيِونَ نِسَاءَكُمْ**

**“.... wakiwachinja watoto wenu wa kiume na kuwaacha hai wa kike;  
.....” (2:49).**

Hii ina maana kwamba ye ye ali kuwa akiwauwa watoto wenu na kuwaacha hai wanawake zenu. Kwa nini aliwaacha hai wanawake zenu? Ilikuwa ni kwa sababu ya kuwaacha uchi na kuwavunjia adabu zao. Kama leo hii utataka kujua uko chini ya mfumo gani wa utawala unamoendeshea maisha yako, utazikuta sadifa na mifanano mingi ya mfumo wa Kifiraun katika mfumo wako mwenyewe wa utawala uliopo sasa. Qur'an Tukufu yenye inazo istilahi zake na ina njia ya kiungwana sana ya kuwasilishia mambo fulani. Firauni ali kuwa akitoa umuhimu zaidi kwa wanawake na umuhimu kidogo tu kwa wanaume; hii ni kwa sababu alitaka sana kuwavua nguo wanawake. Kwa kupitia wanawake, ye ye ali kuwa akiiharibu na kufisadi jamii kwa miili ya wazi ya wanawake. Hata leo hii jambo hili linajitokeza katika mfumo wenu. Haya mashindano ya mbio ndefu (marathon)

huko Lahore yalikuwa ni kwa munasaba gani? Hebu jaribu kuielewa nchi yako na fikiria tu kwamba mfumo huu unatuswaga kuelekea wapi. Kama ingekuwa sasa ni wakati wa Firauni yangetokea mambo haya haya yanayotokea leo hii, au kwa maneno mengine, kama Firauni angekuwepo leo hii, basi angefanya mambo haya haya yanayofanyika sasa katika jamii yetu. Leo hii wanatengeneza taassis chungu nzima za kuwaunga mkono na kuwasaidia wanawake, tasnia ya habari hasa inafanya kazi kubwa ya kuwasaidia wanawake, na kauli nyingi na maelezo, ngonjera zinatolewa kuwapendelea (na kuwapa kichwa cha kighiliba) wanawake. Wanachotaka ni kuwavua nguo wanawake na kuwafanya watembee uchi mitaani katika mbio za marathoni. Waliwalika wanawake waovu wasio na staha kutoka kote ulimwenguni na wakawafanya wakimbie katika mbio za Marathoni. Nchi hii (Pakistan) ina wanawake wasafi wenye staha zao ambao walijiweka wenyewe katika utakaso. Ili kuuharibu na kuu-dunisha utawa wao serikali hii inatengeneza mazingira ya uharibifu. Wote mmeyaona haya kwa macho yenu wenyewe, kwamba kutoka duniani kote, wanawake wameshiriki katika mbio hizi (za Lahore) katika hali ya nusu uchi na mitandao ya televisheni ikazitangaza mbio hizi pamoja na kauli ya kujiridhisha kwamba nchi inasonga mbele kuelekea kwenye maendeleo na kwamba nchi sasa imepiga hatua.

Hebu shuhudia ile picha ambayo Qur’ani inapamba kwa ajili ya mbio ndefu (marathoni) hizi. Hiyo ni ile picha ya mfumo wa Firauni, ambaye aliwaweka wanawake wa Bani Israili hai kwa ajili ya kuwafanya wenye tabia mbaya, hivyo kueneza uharibifu na utembea uchi katika jamii. Qur’ani imesema huu ni mfumo wa Kifirauni ambao unawauwa watoto wenu na kuwavua nguo wanawake zenu, na Sisi tulikutoeni kwenye mfumo huu – vipi?

## MUSA (A.S.) – MWOKOZI DHIDI YA MFUMO WA FIRAUNI

Mwenyezi Mungu alimtuma Nabii Musa (a.s.) kwa ajili ya ukombozi wa Umma huu kutokana na mfumo wa Kifirauni. Ni jambo linalojionyesha wazi kwamba isipokuwa pale tu ambapo Umma hauwezi kuwaunga mkono na kuwasaidi viongozi na waelekezaji kama Nabii Musa (a.s.), hapo wokovu utakuwa hauwezekani. Wanawake hawa walitoka Ulaya wakaja Lahore, wakakimbia uchi mitaani, na wanawake zetu watawa, wenye staha na shungi zao wakawa wanawaangalia. Walifanya hivyo kwa makusudi kabisa ili kuwadhalilisha na kuwanyanyasa wanawake zetu wenye staha. Kama wanawake hawa waovu, wasio na staha (wanaokuja kutoka Magharibi) wanaweza kwa uzuri kabisa kutambua na kutekeleza jukumu lao kwenye uovu, basi ni jukumu la wanawake zetu wenye staha, ama kuondoka ndani ya nchi hii, au kama wakitaka kubakia kukaa humu, basi wawajibike katika kuiokoa nchi hii kutokana na uharibifu huu. Wajibu na majukumu ya wanawake zetu waungwana wenye staha sio tu kuhudhuria kwenye Majlisi za maombolezo ya kidini kwa ajili ya kupata thawabu tu au kusoma Qur’ani kwa lengo hilohilo. Matendo haya hayatuondolei wajibu wetu. Wajibu na majukumu ya wanawake hawa wasafi ni kumuunga mkono na kumsaidia Nabii Musa (a.s.). Musa yupi? Yule ambaye amekuja kubomoa mfumo huu wa uharibifu na kuubadilisha na mfumo wa utawala wa kimungu.

Nabii Musa (a.s.) vilevile mwanzoni aliwataka wanawake waon-doke nchini Misri kwa sababu mfumo wa kifirauni hautufai kue-ndeshea maisha yetu ndani yake hapa. Wanawake hao walionyesha kuhiali kwao na wakatoka pamoja na wanaume wao ili kumfuata Nabii Musa (a.s.). Firauni akawafukuzia mpaka ufukweni, ambako

yeye alikufa maji katika mkabiliano huu. Qur’ani inaliwasilisha hili pia kama fadhila na neema kwa Bani Israili.

## KWA NINI TUJISHUGHULISHE NA MIFUMO YA TAWALA ZETU?

Qur’ani inasema kwamba, tulimwangamiza Firauni na tukakuokoeni kutoka kwenye ule mfumo dhalimu ambapo ilikuwa ni neema kwenu. Baadaye nitazungumzia kuhusu zile athari ambazo mifumo hii ya kidhalimu huwa inaziacha juu ya jamii mbalimbali. Hata ingawa mkiokolewa kutokana na mifumo hii miovu, lakini wakati wowote mtakaotumia kwenye mfumo huu utaacha athari haribifu ya hali ya juu kabisa katika tabia na mienendo yetu. Sisi hatujihusishi na mambo kama hayo. Wakati wote sisi tunasema – inatuhusu nini sisi habari ya mfumo wa utawala, majukumu yetu ni kupata namna ya kuishi kwetu, kuwaangalia watoto wetu, kwenda kwenye Huseiniyah kwa ajili ya Maombolezo, kufanya baadhi ya ibada za wajibu, kwa nini tuwe na wasiwasi au kushughulishwa na mfumo kama ni mbaya au mzuri? Ndio, kwa kweli tunaweza tukawa hatushughuliki juu ya mfumo wao wa kiovu juu yetu, lakini wao wanajali kuhusu sisi. Chukua na kuyaamini maneno yangu kwa uhakika kwamba wale ambao hatujali juu yao, wao kwa hakika wana namna ya ku-jali kuhusu sisi. Leo hii, hatujishughulishi kuhusu Marekani, lakini yenye Marekani inashughulika sana kuhusu sisi.

Kiongozi Mkuu, Ayatullah Khamenei (r.a.) anasema kwamba hawa watu wa Magharibi wanatushauri sisi (viongozi wa dini) kwamba tujitenge na siasa. Wanasema kwamba hawa viongozi wa kidini wanahusika nini na siasa. Yeye anasema kwamba ushauri wao na hoja yao havina mashiko kwa kiasi chochote kile, bali kwa muda

mfupi tu, hebu na tuyapokee na kuyakubali yale wanayoyasema. Hebu na tujitenge na siasa, vyema, sisi hatutaingilia masuala ya siasa. Lakini basi, nanyi pia ni lazima muahidi na kutuhakikishia sisi kwamba hamtashughulika na Dini wala kuingilia kwa lolote lile. Na ninyi pia m jitenge kutoka kwenye Dini. Mnatutaka wana-chuoni wa kidini tujitenge na siasa na tubakie kukaa kwenye Mad-rassa, lakini ninyi hamtaki kuacha kuingilia kwenu kwenye masuala ya Dini. Kama utenganishaji ni lazima ufanyike, basi ni sisi sote, pamoja nanyi wanasiasa, tupaswe kujitenga. Kama ikiwabidi wana-chuoni wa kidini kujitenga na siasa basi ninyi wanasiasa lazima pia m jitenge na dini na muache kuingilia masuala ya kidini!

## **WANAWAKE NA MATUKIO YA KISASA**

Leo sisi Waislam na hususan ninyi wanawake mnapaswa kutambua kuhusu matukio ya kisasa ya ulimwengu wa Kiislam. Isije ikawa kwamba mnajishughulisha zaidi sana na mambo ya jikonii na shughuli nyingine za nyumbani kiasi kwamba muwe hamna habari kuhusu ni nini kinachotokea karibu yako, katika mji wako mwenyewe, ndani ya nchi yako na usitambue kuhusu ni mfumo gani ambamo wewe unaishi. Wakati mwingine tunasema kwamba kiwango cha kielimu cha wanawake wetu kiko chini sana, na kwa hivyo wanachuoni wanapaswa kuwapa mazungumzo rahisi ya kimsingi tu. Mtazamo huu ni matusi kwa wanawake. Hawa wanawake nao ni binadamu vilevile na wana majukumu ya kufanya katika ubinadamu wa ulimwengu huu, wao pia wanapaswa kutoa tabia na inawabidi pia kuishi kul-ingana na zama. Wao wanahitaji kuhisi na kuelewa wajibu wao wa kijamii na kidini mkabala na majukumu yao ya nyumbani. Hawa wanawake ambao walikwenda Karbala na wakatoa ujumbe wa Karbala baadaye pia wao walikuwa na majumba na majiko. Na wao

pia wangeweza kutoa visingizio na kufanya kazi za jikoni, kusafisha nyumba na mambo mengineyo kama hayo maishani mwao mwote, lakini waliamua kwenda bega kwa bega na wanaume huko Karbala. Dini haijawazuia wanawake mahali popote. Kwa kweli wanawake wanalo jukumu makhsusi kabisa ambalo linaweza kutekelezwa na wao tu basi. Hili ni jambo ambalo viongozi wengi na mashuhadaa wa Karbala walikuwa ni matokeo ya juhudzi za wanawake nyuma yao. Kama mke wa Zuhair ibn Qain asingekuwa naye katika safari yake, mambo yangekuwa tofauti upande wake. Yeye alikuwa ni mfuasi wa Khalifa wa tatu na hakuwa ni mfuasi wa Abu Abdillah (a.s.). Ali-kuwa ni mke wake ndiye aliyembadilisha mawazo yake. Baada ya kugeuzwa huku aliingia kwenye orodha ya majina ya mashuhadaa wa Karbala na hivyo pia mionganoni mwa viongozi. Hii ndio jitihada kubwa ya mwanamke huyu ambaye alimfanya mwenza wake wa maisha kufikia daraja hiyo Tukufu na yote haya ni kwa sababu yeye alitambua na kuhisi wajibu wake.

Usikae bila kujihusisha. Inakubidi utambue kuhusu ulimwengu unamoishi na yanayotea karibu yako. Usidhani au kusema kwamba huna lolote la kuhusika nalo kuhusu mfumo wa serikali na ukataka kuishi maisha ya kawaida. Unaweza ukawa huna habari yoyote na mfumo huu, lakini kwa hakika mfumo huu unahuksika vikubwa sana kuhusu wewe. Kama tukisema kwamba hatuhusiki lolote na joto la kiangazi au baridi ya kipupwe, basi pia hilo joto na baridi vina husika na wewe, vitakusonga na hivyo itakubidi uchukue hatua za kujikinga navyo. Kama virusi fulani au maradhi yakienea na mtu akakufahamisha kuhusu hilo, hivi utasema huna habari na mambo kama hayo? Wewe huna cha kufanya na virusi hivyo, lakini vye-nyewe kwa hakika vina cha kufanya kwako wewe. Kirusi huyu ni hatari kwa mwili wako; hivyo kama wewe hutapambana naye kirusi huyu basi utakuwa mateka wake, na atakuathiri. Hatuna haki sisi za kuishi katika aina zote za mifumo. Je, wewe utakunywa aina zote

za maji? Utakunywa maji kutoka kwenye kidimbwi kilichotuama? Endapo mtu atasema haya ni maisha yangu binafsi na ninaweza kunywa aina yoyote ya maji ninayotaka, basi huyo atakuwa anakosea.

Kiakili na hata kidini huna haki ya kunywa maji yasiyo halisi na machafu; ni lazima unywe maji halisi safi na salama. Ikiwa Shariah inaweza kuweka kanuni kuhusiana na maji kwa kiwango hata cha maji yanayotumika kufulia nguo, vipi basi itawezekana kwamba Uislam huo huo usijishughulishe kuhusu usafi wa mfumo wa kijamii unaotutawala sisi? Ujishughulishe sana kuhusu ufuaji wa nguo zetu lakini sio kuhusu maisha yetu, utu wetu, au mambo yetu ya kiroho, au watoto na vizazi vyetu? Ingawa akili Shariah vyote vinakataza kunywa maji machafu, lakini kuna watu ambao bado wanayanywa maji hayo.

## **UDIKTEA CHINI YA KIVULI CHA DEMOKRASIA**

Hatuna haki ya kuishi chini ya mfumo wa aina yoyote, ama kwa Shariah au kwa akili zetu na hususan kuishi chini ya mfumo wa Kifirauni. Hii mifumo ya kiserikali ambayo imenyanyua mabango na miito ya demokrasia yote ni wawakilishi wa Shetani. Kama Allama Iqbal anavyosimulia katika moja ya mashairi yake, “Baraza la Ushauri la Shetani,” ambalo lilitajwa hapo kabla, kwamba Shetani alitiisha mkutano wa mwaka, ambamo wawakilishi wake wote waliifika. Shetani akazichambua kazi zao za mwaka mzima uliopita na akarasimu mpango wa mwaka unaofuatia katika kuwapotosha watu. Iqbal anasema, wakati Shetani alipoulima kuhusu hali ilivyo katika dunia kutoka kwa wafuasi wake, wao walimjibu kwamba mipango yetu ya kishetani inashindwa katika maeneo mengi kutoptana na

sababu fulani fulani. Mmoja wa wafuasi wake alijitokeza mbele na akasema kwamba moja ya hatari kubwa sana kwa Shetani ni kutoka kwenye mfumo wa utawala wa kidemokrasia ambao unaenea kote duniani na demokrasia pia ni mfumo mzuri sana. Shetani akasema kwamba hakuna chochote cha kutilia hofu kuhusu hilo, kwa sababu demokrasia hiihii ndio udikteta wenyewe. Huu ni mfumo ule ule wa Kifirauni, mfumo ule ule wa kiburi na matumizi mabaya ya madaraka tangu zamani na nimeubadilisha mwonekano wake tu. Kwanza ulikuwa ni ubepari, udikteta, ukabaila na sasa pia bado ni ule ule lakini nimebadili vazi lake kuwa demokrasia.

## ATHARI ZA MFUMO WA KIFIRAUNI

Sisi tunadhani kwamba mfumo wa kidemokrasia ambamo ndimo tunamoishi ndio bora kabisa, lakini kihalisia ni udikteta uleule ambao umefichikana katika demokrasia. Ngoja nilielezee hili pia kutoka kwenye Qur'ani. Mwenyezi Mungu anamuamrisha Nabii Musa (a.s.) ndani ya Qur'ani kwenda kwa Bani Israili na akawape ukombozi kutoka kwenye mfumo wa Kifirauni, kwa sababu Umma umekuwa hauna maana, umeharibiwa na mfumo huu na imani zao zimepotoshwa. Hii ndio nukta ya kufanya umakinifu, ambamo tutaona sasa kwamba ni athari angamizi za namna gani ambazo mfumo wa Kifirauni unaziacha juu ya itikadi za kidini za Umma. Walishuhudia miujiza kadhaa ya Nabii Musa (a.s.). Alikuwa na muujiza wa fimbo yake na mkono wake uliokuwa na nuru ulikuwa ni muujiza pia. Kulikuwepo na miujiza mingi kama hiyo ambayo alipewa Nabii Musa (a.s.) ambapo kati ya hiyo, kumi na mbili yake imeorodheshwa ndani ya Qur'ani. Muujiza mkubwa kabisa wa Musa (a.s.) ulikuwa ni ile fimbo yake ya mti ambayo kwayo aliigawanya bahari, aliwashinda wachawi, alimwangamiza Firauni na

akawakomboa Bani Israili. Miujiza yote hii ilishuhudiwa na Bani Israil kwa macho yao wenyewe, bali tazama basi ajabu ya yaliyokuja kutokea baadaye.

Baada ya miujiza yote hii na hatimaye wakavuka kwenye ile bähari na wakaondoka Misri, wakaelekea Palestina na maeneo fulani ya Jordan. Walipofika kwenye ukanda huu wa ardhi ya Jordan, waliona jamii fulani ikijishughulisha na ibada ya masanamu ya miungu iliyotengenezwa kwa mikono ya mwanadamu. Sasa, kwa kusisitiza juu ya jambo hili la kwamba Bani Israil waliona miujiza ya Musa (a.s.), wameyasikia malinganio ya Musa na wakashuhudia mwisho wa Firauni kupitia mikononi mwake Musa, bado walimda Musa (a.s.) jambo ambalo liliduwaza. Kama ilivyotajwa ndani ya Aya ya Qur'ani, walidai kutoka kwa Musa (a.s.)

**قَالُوا يَمْوَسَى أَجْعَلَ لَنَا إِلَهًا كَمَا لَهُمْ إِلَهٌ يَرَوُونَ**

“..... Ewe Musa, tufanyie mungu kama wao walivyo na mungu wao.”  
(7:138).

Hii inaonyesha ni kiasi gani walivyoshuka katika fikra na iti-kadi zao. Hii inathibitisha kwamba masomo yale ya Upweke wa Mungu (Tawhiid) aliyokuwa akiwapa Nabii Musa wao walikuwa hawakuyaelewa kamwe. Lakini swali hapa ni kwa nini? Sababu ili-kuwa kwamba, ule muda mrefu, kwa kweli ni vizazi kadhaa, ambao wameutumia katika ule mfumo wa Kifirauni ulikuwa umedhoofisha kiwango chao cha kufikiri kwa kiasi kwamba hata kufikia hapo hawakuweza kutofautisha kati ya ibada ya sanamu na ya Mungu Mmoja. Hivyo walimda Musa (a.s.) awatengenezee sanamu kama hilo. Waliifanya kuwa ni desturi yao sasa kudai mungu wa sanamu kila

walipomuona mtu yejote akiabudu mungu badala ya yule Mungu wa Musa (a.s.).

Halafu Musa (a.s.) akawachukua kuelekea kwenye nchi ya Qanaani. Baada ya kufika huko Musa (a.s.) akawaambia kwamba Mwenezezi Mungu amenitaka niweke kambi kwa muda wa siku thelathini juu ya Mlima Tur ili nikapokee Taurati. Siku hizi thelathini baadaye zikaongezwa siku kumi zaidi na zikawa siku arobaini ambazo Nabii Musa (a.s.) alikuwa mbali na Umma wake. Kabla ya kuondoka alimfanya Haruni kuwa mwandamizi na mwakilishi wake. Kuna jambo moja la kutafakari hapa, kwamba Musa (a.s.) alijitenga na Umma wake kwa muda wa mwezi mmoja na kisha siku kumi tu, lakini bado hakuuacha Umma wake wenyewe tu, alimfanya Haruni kuwa mwakilishi wake na kiongozi wa Umma. Sasa inawezekana vipi kwamba yule Hojja wa Mwenezezi Mungu (a.t/f/s/) yuko ghaibu kwa takriban miaka 1300 na hakuuacha mwakilishi katika Umma huu?

Wakati Nabii Musa (a.s.) aliporejea baada ya siku arobaini, aliona mandhari ya kutisha. Mandhari hii ilikuwa kwamba ule Ummah umemuacha na kumtenga Harun na ulikuwa ukimfuata Saamiri. Swalii hapa ni vipi Saamiri alifanikiwa katika kuuchukua Ummah huu kutoka kwa Harun. Hapa ndipo tena tunapoweza kuona tabia ya wanawake.

## SAAMIRI NA SANAMU LAKE LA NDAMA

Wanawake wanaweza wakachukua nafasi muhimu kote katika upande wa mazuri na ule wa kinyume chake. Wanaweza wakasaidia katika kuuangusha mfumo wa Kifirauni na pia katika kuimarissha kazi ya kiovu ya Saamiri. Huyu Saamiri aliwaendea wanawake na akawaomba wamletee mali zao zote hususan mapambo yao, ili

kwamba aweze kuwatengenezea mungu wa kumwabudia. Aliwaambia kwamba mungu atakayewatengenezea atawatimizia matakwa na tamaa zao za kidunia, kama wakiongea naye, yeye huyo atawajibu, - mnawenza mkamgusa na kumhisi mungu huyo, na juu ya yote hayo, mnawenza pia mkambusu mungu huyo. Sasa, hiki kisehemu cha kubusu kina umuhimu hata kwetu sisi pia, mpaka tubusu vitu vitukufu na vilivyonkaswa vinginevyo hatujihisi kwamba tumetimiza wajibu wetu. Saamiri alicheza mchezo wa hila; aliwasilisha yale mambo yote ambayo Musa (a.s.) asingeweza kuyawasilisha/ Mungu wa Musa (a.s.) alikuwa hagusiki, watu hawawezi kumbusu Mungu huyo na hawakuweza kumuona ama kumsikia Mungu aliyejulishwa na Musa (a.s.). Hivyo Saamiri alitumia kuwashawishi wanawake kukusanya mapambo yao ambayo walikuja nayo kutoka Misri. Aya ya Qur'ani inasema kwamba wanawake hawa walitoa vito vyao vya thamani vyote, hata kutoka kwenye mikono na mabega yao na kumpa Saamiri. Sasa Saamiri akawasha jiko (tanuri), akayeyusha vito vyote na akatengeneza ndama kutokana na dhahabu na fedha hizo. Hili lilikuwa ni sanamu la mfano wa umbo la ndama aliyetengenezwa kwa dhahabu na fedha.

Saamiri alikuwa ni mtu mwenye akili na mhandisi. Alikuwa ni mtu wa kiroho na kidini. Alikuwa anaitambua hiyo teknolojia vinginevyo asingefanikiwa kutengeneza ndama kwa kuyeyusha mapambo. Hakutengeneza ndama wa metali tu, bali pia aliingiza ndani yake athari ya kiasi kwamba ndama huyo alikuwa anasogea pia. Baadaye wakati Nabii Musa (a.s.) alipokuja kumuuliza ni vipi alifanikiwa kumfanya ndama yule azungumze, yeye alijibu kwamba yeye alikuwa ameona mabaki ya mjumbe. Mabaki ya mjumbe ina maana kwamba ama alichukua kitu kutoka kwa Jibril au alichukua mchanga kidogo kutoka chini ya nyayo za Musa (a.s.) na akautumia kwa ndama huyo kumfanya azungumze. Hii inathibitisha kwamba kiwango chake cha elimu kilikuwa cha juu sana kiasi kwamba ama

alijua athari za mchanga chini ya nyayo za Musa au alichukua kitu kutoka kwa Jibril na akamfanya ndama huyo kuwa mashughuli. Umma wote mzima kwa mbinu hii ya Saamiri ulidanganyika, ukamuacha Haruni na ukaanza kumfuata Saamiri.

## MUSA NA HARUNI (A.S.)

Sasa, wakati Musa (a.s.) aliporejea, alikasirika sana juu ya hali hii. Mara akaidondosha ile Taurati kutoka mikononi mwake na aka-muuliza Haruni kuhusu hali ile. Haruni akajibu kwamba yeze alijitahidi sana kuwalingania haki, akawazuia na kujaribu kuwahakikishia kuhusu upotovu huu, lakini wao hawakuwa tayari kumsikiliza yeze. Qur’ani inaelezea ule ukali ambao Musa alimfanya Harun (a.s.). Alimshika Haruni kwenye ndevu na nywele zake za kwenye paji la uso na kisha akamburuza kwa hasira. Musa kukerwa na Haruni ni kwamba yeze kama Nabii amemfanya Haruni kama mwakilishi wake, alimpa uongozi wa Umma na kwa hiyo wajibu wake ulikuwa ni kulinda dini ya Umma huo, na isingetokea hivyo ila ni kwa sababu ya uvivu na uzembe wake Haruni ndipo jamii yake ikam-fuata Saamiri. Hili wakati wote hutokea kama hapa, ambapo wakati Musa (a.s.) alipokwenda ghaibu ya siku thelathini, Saamiri alitoka nje ya jumuiya. Hivyo jiandae kukubali ukweli huu kwamba wakati Maasum anapoingia kwenye ghaibu kwa muda wa miaka 1300, ni Saamiri wangapi wangeweza kutoka nje ya jumuiya katika kila kizazi na kila zama?

Huu ni ukweli uliothibitika kwamba kutokana na sheria na malengo ya kimungu, yule Hoja ya Allah (Hujjatullah) anapoingia kwenye ghaibu kwa kipindi cha muda fulani. Basi jumuiya hiyo na dini yao vinakuwa vinakabiliwa na tishio kubwa la kutokana na ma-Saamirii. Tusiwe wepesi sana na tusio na fikra kwamba kila

yejote anayekuja na ndama anayezungumza na kufanya namna ya jambo, sisi tuanze kumwabudu ndama huyo na kuwa watumwa wake. Kwanza mwangalie yule aliyeleta sanamu hilo kwetu sisi, na kisha angalia ni nani ambaye ni mwakilishi wa Hujjatullah ambaye amemuacha mionganoni mwetu wakati wa ghaibu yake hii. Nukta hii inahitaji kufafanuliwa tena kwamba Musa (a.s.) aliondoka kwenda ghaibu kwa muda wa siku thelathini tu na akaacha mwakilishi wake mionganoni mwa watu, na wakati aliporejea hakuuliza Umma mara moja juu ya vitendo vyao viovu, kwanza alitaka taarifa kutoka kwa Haruni endapo kama hali hii ya Umma ilikuwa ni matokeo ya uvivu wake ama laa. Musa (a.s.) alikuwa na wasiwasi kwamba huenda Haruni alihusika na akakaa kimya nyumbani kwake, au kwa lugha ya kisasa alikaa kimya ndani ya Madrassa yake (shule ya kidini) ama alijishughulisha na kazi zake za kila siku na akauchacha Umma ukacheza mikononi mwa Saamiri, na akamwachia Saamiri kuu-peleka Umma kwenye mwelekeo wowote alioutaka yeche.

Somo linalopatikana kutoka kwenye masimulizi haya ya Qur’ani yako wazi kabisa kwamba, wakati huyo Hujjatullah atakapodhibiri atawauliza kwanza wawakilishi wake. Kwa hakika atawauliza kwamba: “Mimi niliwaachieni Umma huu, na je sio ninyi amba ml-ijihuisha na mambo yenu binafsi, mambo ya kifamilia, au mkashuhulika sana katika hotuba na mihadhara yenu, na matokeo yake mkauachia Umma ukatekwa na Saamiri?” Pale Haruni alipokuwa na majibu yenye mantiki ya kuaminika kwenye maswali ya Nabii Musa (a.s.), ndipo tu Musa alipomwacha Haruni (a.s.) na akamuuliza Saamiri na kisha Umma wake.

## WAJIBU WA MSINGI WA WANAWAKE WAKATI WA GHAIBU

Madhumuni na lengo la kujadili kadhia hii yalikuwa yanafaa kwa wajibu wa Umma na hususan wanawake, kwa vile sanamu hili litengenezwa kwa pamoja na ushirikiano wa wanawake. Wanawake lazima wawe makini sana juu ya jambo hili kwamba wakati wa kipindi cha ghaibu, wajibu wa wanawake sio kumsaidia, kumuunga mkono na kushirikiana na Saamiri. Hatuna budi kuwa na tahadhari na Saamiri wa zama zetu hizi, kwa vile kipaji cha Saamiri ni kututumia sisi tu katika kutengeneza masanamu ambayo yanasisimama dhidi ya Mungu wa Nabii Musa (a.s.), kwa namna ileile Saamiri alivyowatumia wanawake katika kutengeneza yule ndama. Halikadhalika leo hii ndama kama hao wanatengenezwa kwa msaada wa Umma. Lakini, masanamu ya ndama wa leo hii ni ya kisasa zaidi. Haya ni masanamu ya uoni – mtazamo, mawazo, misingi na dhana, zinazoishia kwenye kuwepo kwa madhehebu nyingi zinazochipuka kutoka kwenye kundi moja hilo hilo la kidini. Yote haya ni masanamu ya Saamiri, na jukumu letu ni kutafuta kwanza ni nani Haruni wa zama zetu, na ni Mungu na madhehebu gani anayotutaka sisi tufuate.

Moja ya athari za hatari sana ambazo mfumo wa Kifirauni unaizacha juu ya Umma ni ile ya kwamba Umma wenyewe unakuwa dhaifu sana katika imani zao, itikadi na elimu ya kweli. Matokeo ya udhaifu huu ni kwamba unakuwa hauwezi kutofautisha kati ya mungu wa sanamu na Mungu wa Milele. Hii ndio sababu Imam Hussein (a.s.) anaonyesha shukurani kwa Allah kwa kule kwanza kusimamishwa kwa mfumo wa utawala wa Kiislam mionganii mwa jamii ambamo yeye alikuja kuzaliwa baadaye. Hili lilikuwa ni kutuuliza sisi kuhusu ni aina gani ya mfumo wa utawala tunaopendelea kuishi ndani yake. Ufuasi kwa Husein hauna maana ya kufanya vitendo

kulingana na matakwa yetu katika jina la Husein (a.s.), bali badala yake ufuasi kwa Husein ni mkusanyiko wa vitendo vile ambavyo Imam Husein (a.s.) alivikamilisha. Hivyo ndio vitendo ambavyo hatuna budi kuhitajika kuvitenda na kuvihifadhi.

## **TATIZO KUBWA LA UMMA UNAOWASADIA MA-SAAMIRI**

Juu ya msingi wa itikadi na fikra, Umma huwa unakuwa dhaifu pale unapoishi katika mfumo wa Kifirauni. Hapo ndipo Saamiri anapo-chukua fursa ya madhaifu haya ya Umma. Kutokana na urahisi huu wa Umma, Saamiri hutumia nafasi hii, anaubadilisha mwelekeo na kuwaweka nyuma ya sanamu la ndama au mahali pengine popote. Leo hii pia hali ni hiyohiyo, ni mfumo uleule wa Kifirauni. Katika nchi yetu (Pakistan), tangu mwanzo wa kuwepo kwake ilikuwa na mfumo wa Kifirauni. Lakini ndani ya mfumo huu wa Kifirauni, mara nyingi katika umbo la ndama wa Saamiri, tumeona masanamu ya demokrasia, masanamu ya udikteta, masanamu ya nguvu za kijeshi na yote haya, wakati fulani yaligeuza mfumo mzima kuwa mfumo wa kijeshi wa Kifirauni. Na wakati wote tunafikiri na kusema, tu-nahusika nini sisi na mfumo huu! Rais awe ama ni wa mrengo wa kushoto au wa kulia, awe mwanaume au mwanamke, hili au lile, naaingie mtu yejote kwenye madaraka, sisi linatuhusu nini hilo? Rais naawe mtu yejote yule sisi hatuna wasiwasi, madhali tu yeje awe hatuzuii sisi kufanya Maombolezo ya Imam Husain (as), madhali hatuzuii sisi kuendelea na kuomboleza. Naatawale na kutuongiza mtu yoyote yule sisi hatujali wala kuhofia, ambacho tutajali tu na kuhofu ni kwamba serikali hiyo isituzuie kufanya Majilisi na maombolezo yetu. Lakini ukweli halisi hauko kama hivyo! Wewe unaweza usiwe na wasiwasi nao, lakini wao ni dhahiri kabisa wana

wasiwasi na wanajishughulisha na wewe. Na kujishughulisha kwao na sisi ni kwamba watatudhoofisha sana sisi kiakili kiasi kwamba hatutakuwa na uwezo wa kutofautisha kati ya Saamiri na Haruni. Huyo Haruni wa zama zetu atakuwa anatuita sisi kuelekea kwake nasi tutakuwa tunajishughulisha zaidi sana na kuwaunga mkono ma-Saamiri. Soma Qur’ani Tukufu na uone, hiki ndio hasa kile Bani Israil walichokuwa wamefanya huko nyuma kwamba pia wanawake wao wa kidini walishirikiana na Saamiri katika kutengeneza sanamu la ndama. Leo hali kadhalika hali ni ileile, katika jina la uhuru wa wanawake na haki za wanawake, mbio ndefu (za marathoni) zinaandalowiwa. Wanatengeneza masanamu kwa ajili ya wanawake na wanayatumia masanamu haya katika kuwakengeusha watu mbali na dini.

## **WILAYA – MFUMO HALISI NA WA KWELI WA UTAWALA**

Kama tulivyoeleza katika sehemu ya mwanzoni ya kitabu hiki kwamba Uimamu (Uongozi) sio itikadi tu au wazo au dhana ya kisomi au kirai au mwito au kiasi tu cha ufahamu wa akilli. Imam Ali (a.s.) anasema kwamba:

فَرَضَ اللَّهُ ..... الْإِمَامَةَ نِظَامًا لِلأُمَّةِ

**“Uimam ndio mfumo wa kimungu  
wa utawala kwa ajili ya Umma.”**

Hii ina maana kwamba inatubidi tuishi maisha yetu chini ya mfumo wa Uimam na Wilaya. Wilaya ni ule mfumo ambao unaweza kuongoza Umma kuelekea kwenye uongofu; unaweza ukauchukua

Umma kuelekea kwenye upandaji au ukuaji kimungu na unaweza ukawa chanzo cha utukufu kwa Ubinadamu. *Wilaya* ni ule mfumo ambao unaweza kulinda na kuhifadhi heshima ya binadamu. Ndio mfumo pekee unaoweza kutetea na kulinda dini yetu na kutuokoa kutokana na fedheha kubwa. Na hii ndio sababu ambayo kwamba makafiri walikuwa wamekata tamaa na wakawa na wasiwasi ile siku ya Ghadir. Walipoteza matumaini kwa sababu kama Mfumo huu wa Utawala utaendelea hata baada ya Mtukufu Mtume (saww) pia, basi Umma utapata wokovu na hawa matwaghuut (mashetani) hawata-fanikiwa katika mamlaka na utawala juu ya Umma. Ili kuitengua hatari hii mara tu baada ya kifo cha Mtukufu Mtume (saww) wali-fanya kazi ya kuubadili mfumo huu. Waliugeuza mfumo wa *Wilaya* na kuwa Ukhilifa, kisha Ukhilifa nao ukageuka kuwa Ufalme ambao baadaye uligeuka kuwa Uyaziid, na Umma ulikuwa tayari kuishi chini ya mifumo hii ya utawala. Matokeo yake damu Tukufu na tohara ya Imam Husein ibn Ali (a.s.) ilimwagwa ili kuuzindua Umma na kuukumbusha kwamba huu mfumo wa utawala mnamoi-shi chini yake maisha yenu unakuongozeni ninyi na Uislam kwenye maangamizi.

Leo hii vilevile hali ni ileile ambamo sisi pia tupo tayari kuishi maisha yetu chini ya mfumo wowote wa utawala. Katika nchi hii (Pakistan), mfumo unabadilika kila baada ya miaka minne. Wakati mwingine tunaliona sanamu la ndama wa demokrasia, wakati mwingine la udikteta na tuko tayari kuupokea mfumo wowote kama huo ambao unakuja kutawala juu yetu. Mfumo pekee ambao hatuko tayari kuukubali au angalau kupiga hatua kuuelekea uliko ni mfumo wa Uimam. Yeyote anayepigia kura ndama wa sanamu la demokrasia anafanana na wanawake wa Bani Israili waliota mapambo yao kwa Saamiri ili kutengenezwe sanamu la ndama. Masanamu ya ndama wa Saamiri huwa wanatengenezwa tu kwa ushirikiano wa Umma.

Nchi inaweza kuokolewa tu kwa utekelezwaji wa Uislam Halisi, yaani kufuata Mfumo wa *Wilaya* na Uimam. Kufanya hivyo, kwanza inatubidi kuuwasilisha mfumo huu wa *Wilayaat* kwa watu. Leo hii kuna hao Ma-Saamiri wengi kama hao ambao hawazungumzii kamwe dhidi ya mifumo ya udikteta, Uyaziid na Ufirauni, lakini in-apokuja kwenye *Wilaya* hufungua midomo yao haraka haraka. Wao wakati wote watazungumza tu dhidi ya serikali ambayo ina mfumo wa *Wilaya* ndani yake. Wakati wowote unapowaona watu kama hao wanaofungua vinywa vyao dhidi ya mfumo huu wa *Wilaya* (yaani, Jamhuri ya Kiislam ya Iran), basi chukulia kwa uhakika kabisa kwamba hao ndio ma-Saamirii wa zama zako na kisha uwatambue kutokea hapa penyewe.

Kama ukitaka kujua kuhusu Uimam basi usiende kuwauliza wale ambao wala hawajui kama Uimamu katika Kiarabu inaadikwa kwa ‘Alif’ au kwa ‘Ain.’ Dini yetu imeingia kwenye hali na mazingira ya kushangaza sana, ambamo tabaka la wenye elimu linakaa na kusikilizishwa dini kutoka kwa watu wasio na ujuzi waliokaa juu ya mimbari. Watu wenye akili timamu wanasiliza mazungumzo ya kidini kutoka kwa watu wasio na maana kabisa. Tunao wazungumzaji mabingwa, kote kwa wanaume na kwa wanawake, wale ambao wana-jua mbinu za uongeaji tu, hawa wameiharibu dini yetu. Mabingwa hawa wa uongeaji wanakuja kutuingiza sisi katika mambo yenye mishkili, wanachukua ada zao na kwenda zao nyumbani, ambapo wanatuacha tunagombana wenyewe kwa wenyewe kuhusu masuala haya yenye utata.

## UIMAM KWA MTAZAMO WA ALLAMA IQBAL

Kama unataka kuulizia kuhusu Uimam, basi muulize Allama Iqbal. Kwa mujibu wake yecheza anasema:

*“Umeniuliza juu ya uhakika wa Uimam,  
Haki ikufanye mwenza wa siri zake kama mimi.”*

Hii ina maana kwamba kama umedhamiria hasa kuhusu kuelewa mfumo wa *Wilaya*, basi kwanza inakubidi uwe mwenza wa siri zake. Mpaka uwe umejihususha na upande wa ndani wa Uimam, vinginevyo huwezi kuuelewa mfumo wa *Wilaya*. Hutaweza kutofautisha kati ya Ndama na Mungu wa kweli, kati ya Musa na Saamiri mpaka uwe mwenza wa siri za Uimam. Kisha Iqbal anaendelea kusema:

*“Yeye ndiye Imam wa zama kwa hakika,  
Mtu anayekuzuia kutokana na ulimwengu wa kimaada,  
Anakuonyesha uso wa mpenzi wako katika kioo cha mauti.  
Hivyo kuyafanya maisha yenu kuwa magumu zaidi na ya dhiki.”*

Sasa tazama ndani kabisa ya vifungu hivi na ujiulize wewe mwenyewe ni kwa nini sisi tunaamini Maimam. Tunaamini kwa ajili ya uboreshaji wa maisha yetu, kutimiza tamaa zetu za kidunia kupitia kwao wao? Allama Iqbal anasema kwamba huyo ni Imam wako wa zama, yule mtu anayefanya maisha yako kuwa magumu zaidi na yenye dhiki hasa. Halafu anaendelea kusema:

*“Imam wa mtu huyo ni Fitna,  
Yule anayefukuzia watu kuwaabudu mabeberu.”*

Hii ina maana kwamba mtu ambaye uongozi wake unalifanya taifa linyenyeknee kwenye udikteta, ubeberu, ufalme, demokrasia na utawala, huyo ni mtu fitna juu ya Umma huo. Mpaka pale tu tutakapoufunza ulimwengu juu ya Uimam na tukaanza kutekeleza Wilaya, vinginevyo dunia haiwezi kwa yenyewe tu ikaelekea kwenye mfumo wa Wilaya. Ninyi wanawake inakubidini mchukue masomo na mpate kuona ni wanawake wangapi walichangia kwenye mafanikio ya Nabii Musa (a.s.). Akina mama jaribuni kuwa kama mama yake Nabii Musa, dada yake na mke wake Musa (a.s.), hapo tu ndipo Musa atakapopata nguvu ya kuuangusha chini ule mfumo wa Kifirauni na kuanza kutekeleza mfumo wa Wilaya mionganoni mwa watu.

## **WAJIBU WA WANAWAKE KWENYE MFUMO WA WILAYA**

Tena ukumbuke jambo lile lile nililosema mapema, kwamba athari za kuishi muda mrefu chini ya mfumo wa Kifirauni zinadumu muda mrefu. Athari hizi ni udhaifu katika imani, maadili, akili, uwezo wa kihisia na mtindo wa maisha. Na kwa matokeo yake Umma huo ulimsumbuwa sana Nabii Musa (a.s.) baadaye. Walikuja kuwa wenye mawazo finyu na hawakuweza kuelewa kile ambacho Musa (a.s.) alikuwa akijaribu kuwalingania, yote haya yalikuwa ni katika jumla ya athari za kule kuukubali mfumo wa Kifirauni kwa ajili ya kupitishia muda wa maisha yenu. Qur'ani Tukufu inaelezea namna ny- ingine moja zaidi ya udhalimu ambao Firauni aliufanya juu ya taifa lake, na huo ni uitwao "*Istkhafful Kaum*," alilifanya taifa lake kuwa duni mno. Umma uligeuka kuwa duni na dhalili sana, ukiwa tayari kukubali aina zote za fedheha, vitendo vibovu na kukandamizika sana katika muundo wa fikira zao.

Leo hii utauona mfumo wa Kifirauni umetufanya sisi nasi jambو kama lile lile. Wale wanawake ambao wajibu wao ni kuwasili-sha *Wilaya* kwenye ulimwengu wamejiingiza kwenye masimulizi ya Mkatakuni (kisa cha kubuni kinachosimuliwa katika mwezi Mtukufu wa Rajab, wakati wa hafla za “Qunda Nazr,” tafrija za chakula kwa jina la Imam as-Sadiq (a.s) ). Hili ndio tatizo ambalo mfumo wa Kifirauni unatujengea katika jamii. Wanawake zetu wanatarajiwa kuwa watetezi wa *Wilaya* kama Bibi Zainab (a.s.), ambao inawabidi watoke kuuendea ulimwengu na kuzungumza juu ya *Wilaya*, Uimam, kuwasihи water wasikubali kuishi chini ya huu mfumo wa ki-Yaziid na kuwalingania kwenye mfumo wa Uimam. Lakini wakati dini in-apokuwa imedhibitiwa na kumilikiwa na mfumo wa Kifirauni, basi dini hii inabadilika na kuwa dini ya visomo vikavu vya mdomo na madua, ambamo water hupitisha maisha yao katika kuvuta na kuhes-abu punje za Tasbihi tu.

Chini ya mfumo huu wa Firauni, wakati wanapotekeleza dini, huwa wanaishia katika kuunda miundo yao binafsi ya dini na kuanza kuviabudu vitu hivyo usiku na mchana. Endapo kama tutajiingiza kwenye mambo kama hayo, basi atakuwa ni nani atakayejitokeza na kuelezea na kufundisha walimwengu Uimam na *Wilaya* ni kuhusu nini hasa? Ni nani atakayeandaa yale mazingira muhimu kwa ajili ya kudhihiri kwa Imam (a.t.f.s.)? Ulimwengu ni lazima kwanza uji-andae katika kuupokea mfumo wa *Wilaya* ndipo tu kudhihiri kwake kutakapotokea. Hii ni kwa sababu, hapo wakati atakapodhihiri yeye (a.t.f.s.) hatakekeleza demokrasia au udikteta, yeye atatekeleza huo Mfumo wa *Wilaya*. Lakini ni vipi atatekeleza mfumo huu wa *Wilaya* kama water hawako tayari kuukubali mfumo huo wa *Wilaya*? Kama tumo kwenye kushughulishwa na simulizi zile za visa vya Mkatakuni, basi ni lini mtakapomtarajia yeye (a.t.f.s.) kudhihiri na kutekeleza *Wilaya*?

## MLANGO WA NNE

### KUUHIFADHI MFUMO WA WILAYA

#### KUTOKA NJE YA NJIA SAHIHI YA DINI

**M**oja ya msisitizo wa kitabia wa Maimam Maasumin ni kwamba wakati wote walikuwa wakiwashawishi watu kuelekea kwenye kupata umaizi na utambuzi wa kina juu ya dini. Wamehimiza sana juu ya kipengele hiki na wao wenyewe wamechukua hatua za kivitendo na wamefanya mipango kwa ajili ya hilo.

Baadhi ya waheshimiwa Maimam Maasum (a.s.) mionganoni mwa Maasumiin wametoa nyenzo kwa watu ili wasiingie katika ugumu katika kuielewa dini, kwa hiyo hizi nafsi takatifu zenyewe zilitoa fursa kwa watu kwa ajili ya kujitokeza kuja kuielewa na kuitambua dini. Mfano mkubwa kabisa wa hili ni maisha ya Imam al-Baqir (a.s.) na Imam as-Sadiq (a.s.) na kisha tena baada ya wao Maimam wengine (a.s.) pia walifanya vivyo hivyo kwa kiwango kidogo kutokana na mazingira (hasa ya kisiasa). Utoaji fursa walizokuwa nazo Maimam ulichukua hatua kila ilipowezekana kuondoa matatizo na matukio yaliyowapata Umma wa Waislam kutokana na kutoutambua Uislam na kukosa ufahamu wa dini. Jambo kama hili linaonekana pia ndani ya *Nahjul-Balaghah* kwenye sehemu mbalimbali ambamo tunaweza kuona kwamba jambo moja ambalo lilimhuzunisha sana Amirul-Mu'minin Ali (a.s.) lilikuwa kutokufahamu kwa watu na kuwa na uelewa mbaya wa dini ambapo pia hususan katika zama zile ambamo mlikuwa na wale waliokuwa wakati wote waki-

jaribu kuipotosha dini wakiwakilisha kinyume chake chini juu, juu chini. Kulikuwa na mwanya wa miaka 25 hadi 30 hivi baina ya kifo cha Mtukufu Mtume (saww) na ile serikali ya Amirul-Mu'minin Ali (a.s.), na ilikuwa ni katika kipindi hiki ambamo uharibifu ultokea katika dini ya kweli halisi ya Nabii Muhammad (saww). Ile dini Safi ikawa chafu, yenyewe mapungufu na iliopotolewa; na juu ya hili Amirul-Mu'minin (a.s.) anasema ndani ya *Nahjul-Balaghah*:

### لِبْسُ الْاسْلَامِ لِبْسُ الْفَرْوَ مَقْلُوبًا

**“Nguo ya Uislam imevaliwa juu chini.”**

Hii ina maana kwamba, leo hii kama nimekamata hatamu za serikali na mambo ya watu mikononi mwangu; na ninapoona hali ya dini mionganoni mwa watu ninahisi kwamba watu wamevaa vazi la Uislam chini juu, na juu chini, yaani wameuchukulia ndivyo sivyo. Wanajifanya kuwa ni wachamungu na wanayo dini pamoja nao lakini wameivaa ndivyo sivyo. Hivyo siwezi hata kuwaita wasio na dini wala siwezi kuthibitisha au kuridhia udini au uchamungu wao. Hili lilikuwa ndio tatizo kubwa mno hasa lililowakumba Maimam Watukufu (a.s.) kwamba watu walikuwa na uhusiano na dini lakini uchamungu wao haukuwa wa kiwango cha kuweza kuwa wachamungu hasa. Na sababu ya hili ilikuwa ni yale matatizo ya watu hawa yaliyowakabili katika kuitambua dini ambako kuna maana ya maandalizi, mipango na umuhimu ambavyo vilitarajiwa kutolewa wakati wa kuieleta dini havikutolewa kamwe; waliichukulia dini kwa wepesi kabisa na kwa kiwango cha juu juu tu. Hivyo wapinzani wakaja na kwa urahisi kabisa wakageuza mwelekeo wa dini yenyewe na wa watu pia hawakuweza hata kuhisi wala kutambua kuhusu hilo!

Wakati wote huwa nikitoa mfano wa treni kwenye muktadha huu. Katika mfumo wa reli kuna mtu ambaye jukumu lake ni kubadilisha zile njia. Magari moshi yanatembea juu ya njia za reli ambazo zinakwenda pande mbali mbali tofauti. Katika kituo fulani cha reli au njia panda magari moshi mengi kutoka pande tofauti huja na kuondoka kuelekea upande mwengine kabisa. Idara ya reli imeajiri mtu maalum ambaye kazi yake ni kubadilisha njia au mikondo. Kazi hii ya kubadili njia na mikondo hutokea kwa ulaini sana kiasi kwamba watu waliokaa mle ndani ya garimoshi huwa wala hawatambui kwamba mwelekeo wao umebadilishwa kwa sababu yule anayebadilisha hiyo mikondo hafanyi hivi kutoka ndani ya treni; anafanya hivyo akiwa yuko nje. Treni inayotembea katika njia iliyonyooka inabadili mkondo wake kwa mshughuliko wa kawaida wa mtarimbo; kwa kuu-sogea kidogo mtarimbo huo kwenda kushoto au kwenda kulia, treni inayoelekea Mashariki sasa inakwenda kuelekea Magharibi na ile inayoelekea Kaskazini sasa inakwenda kuelekea Kusini. Ungeweza kusafiri ndani ya treni na usingeweza hata kuhi ni wakati gani mtarimbo huo ulibadili mkondo huo. Huyo anayebadili mikondo hiyo ameajiriwa na anapata mshahara ili kubadili mikondo hiyo. Ingawa hili ni muhimu kwa ajili ya treni kwa sababu inabidi iende upande tofauti, lakini jambo kama hilo limefanywa upande wa dini vilevile. Hii ina maana kwamba dini ilikuwa na njia iliyonyooka, *Siraat al-Mustaqiim*, lakini wabadili njia fulani wamebadilisha. Wanalfanya hilo kimya kimya kweli kweli kwamba hata wale waliokaa ndani ya treni hiyo ya dini, wenyewe uhusiano na shule za Kidini, wanaohusiana na vituo vya kidini na itikadi wala hawasikii chochote kuhusu hili kwamba njia yao ya dini imebadilika. Wamekaa kimya kwa kuridhi-ka kwamba kuanzia pale walipoanza kushughulika juu ya dini itaendelea katika njia hiyo hiyo kuelekea kwenye hatima yake. Kadha hii inatokea katika msingi wa kila siku na ilitokea wakati wa Maasumin (a.s.) vilevile. Hivyo kulikuwa na watu wakati ule pia ambao kimya

kimya bila kujitambua walibadilisha mikondo, na njia na wakaipelika jamii, makabila na Umma kwenye mielekeo mingine. Hii ndio sababu ambayo kwamba Mtukufu Mtume (saww) ameainisha na kuonyesha alama dhahiri zenyé kuonesha Njia iliyyonyooka ya haki, lakini watu waliachä njia hii. Kama unataka kuzielewa zama hizi za sasa, basi jaribu kuielewa historia na ili kuielewa historia; tafakari juu ya zama hizi zinazoendelea sasa.

Tukio la Ghadir lilikuwa ni ishara iliyoonyeshwa wazi na Mtukufu Mtume (saww) lakini ingawaje kwenye mwanga mkali wa mchana, alama za njia hii iliyotangazwa na Mtukufu Mtume (saww) ilibadilishwa na Umma ukawekwa kwenye mkondo mwingine tofauti. Umma ulikuwa hata haukutambua kwamba tumepotoshwa kutoka kwenye njia hiyo. Watu waliachä njia ya *Wilaya* na wakashika njia nyingine. Hata leo hii, kama ukiiiona njia ya *Wilaya*, mfumo wa *Wilaya* uko wazi na unaonekana dhahiri kabisa kufanana sawa kama ulivyoonekana wazi mnamo siku ya Ghadir. Amirul-Mu'minin Ali (a.s.) aliteuliwa na kutangazwa kama yeye ndio njia sahihi ya dini, kadhalika leo hii pia njia ya *Wilaya* ndio njia sahihi na ya haki.

Sasa hivi, Ummah wote wa Kiislam, na hususan Shi'ah umepelekwa kwenye njia nyingine kabisa na wengi wao wameng'olewa kwenye njia sahihi na treni inakwenda kwenye uelekeo mwingine. Mkondo wa dini upo bali wanaongozea kwenye uelekeo mwingine tofauti, na watu wanafurahia kwamba hiyo inaelekea moja kwa moja kwenda Peponi; hawana hata fununu kwamba mtarimbo umebadilishwa.

Msiba kama huo huo umetokea kwa Shi'ah pia katika zama hizi za sasa wakati ule Mfumo wa *Wilaya* uliposimamishwa (katika Jamhuri ya Kiislam ya Iran baada ya Mapinduzi ya Kiislam). Ukweli wa tangazo la Mtukufu Mtume (saww) uliwasilishwa, ukatekelezwa na matakwa ya Maimam (a.s.) yakatimizwa. Yalikuwa ni matakwa

yenye shauku kubwa ya Maimam kwamba siku moja Mfumo wa *Wilaya* uwe umesimamishwa juu ya ardhi, lakini tunaona baadhi ya watu walichukua fursa ya washika mitarimbo wote na kwa msukumo mmoja tu wao wamegeuza njia ya jamii kadhaa, Umma kadhaa, makabila, nchi kadhaa na makundi na sharika mbalimbali za watu. Tunafurahi kwamba tuna uhusiano na Uimam lakini Umma bila ya *Wilaya* unabeba dhana na njozi tu za Uimam; uimam usio na Mfumo wa *Wilaya* (Utawala wa Kiislam).

Msiba huu umekuwa ukitokea wakati wote katika dini na kile ambacho Maimam wote (a.s.) walichokifanya kuhusiana na hili kinapatikana kwa maelezo ya kina bali kwa bahati mbaya sana sisi tumeng'ang'ania kwenye mas'ala ya imani tu kuhusu Maimam. Mpaka sasa hivi tumesimama katika kidati cha awali cha Ngazi ya Uimam na kwa kusema kweli wala hatujafikia ile hatua ya Imani juu ya Maimam vilevile. Tumefikia katika hatua ya kwamba Imani juu ya Maimam maana yake ni mapenzi juu ya Maimam na kuwakumbuka kwao, lakini hatujasonga mbele kuelekea kwenye hatua inayofuatia ya kuwatambua, na kutokana na kukosekana mazingatio, maisha ya Maimam (a.s.) yamefichikana kwetu sisi na hususani mtindo wao wa maisha wa upinzani na makabiliano.

Kama tukiangalia na kutazama huku na huko tunajikuta kwamba ni nadra kujua chochote kuhusu Imam yoyote yule baada ya wale Maimam watatu wa kwanza. Tunajua kiasi gani kuhusu Imam Haadi (a.s.). Hata kama ukiwaliza Wanachuoni au ukitembelea kwenye Maktaba, ni kiasi gani utakachokuta kilichoandikwa kuhusu Imam Haadi (a.s.)? Je, kuna utafiti wowote uliofanywa juu ya hili? Kwa jumla tutakuta kwa shida sana kurasa kumi na tano tu zilizoandikwa kuhusu Imam Haadi (a.s.), na katika kila zama, kila anayeandika kumhusu ye ye takriban anarudia kurasa hizo hizo kumi na tano tu. Kiasi cha matukio, kiasi cha miujiza, kiasi cha

mahojiano na yote hayo kwa pamoja yamekusanywa katika kurasa 15 na hayo ndio yanakamilisha umri wote wa maisha yake Imam Haadi (a.s.). Msiba kama huohuo ndio uliopo kwa Maimam wen-gine vilevile, kama mfano ni kiasi gani tunachokijua kuhusu Imam Jawad (a.s.)? Tunazungumzia tu kuhusu taarifa; hatuzungumzii kuhusu ni utambuzi gani tulionao kuhusu mwelekeo wao wa fikra na njia yao. Pakistani yalifanyika maombolezo yaliyoandaliliwa katika kadhia ya maadhimisho ya Shahada ya Imam Haadi (a.s.) na kila mzungumzaji aliyesimama alikuja kuzungumzia ubora wa Imam Ali (a.s.) na mashairi ya maombolezo ya Imam Husein (a.s.). Ilipokuwa inakaribia zamu ya mhutubu wa mwisho, mtu mmoja akasema kwamba angalau zungumzieni chochote kuhusu Imam Haadi. Wakamuomba yule mzungumzaji wa mwisho kufanya hivyo. Khatibu huyu akamuuliza mwanachuoni aliyekaa karibu naye kwamba: “Unaweza kunipatia tarehe ya kuzaliwa na ya ku-uliwa shahidi kwake Haadi (a.s.) halafu mimi mwenyewe nitaten-geneza kisa na historia ya maisha yake kutokana na tarehe hizo?” Huu ndio msiba ambamo Imam ametelekezwa na kusahaulika na hii ndio dhulma kwa Uimam ambao kwamba bado haujatambulika kwa sababu hatujasonga mbele zaidi ya itikadi juu ya Uimam na wala hatukusudii kufanya ama dalili zozote za kusonga mbele zi-nazoonekana.

Kazi ambayo Maimam Watukufu (a.s.) waliyoiwasilisha wakati wa zama zao imeelezwa kwa kina; mipangilio yao, tabia na hatua zao ni kubwa mno na licha ya wao kutokuwa na nguvu za kisiasa za kutawala, wao bado walifanya Uongozi (Uimam). Na kama tutaiele-wa ile siri ya ni vipi waliweza kufanya hivyo, basi mengi ya matatizo yetu yatafumbuka. Kwa mwanga wa mafundisho haya tunaweza ku-tatua matatizo yetu yote bila kujali ni kwa kipimo gani maisha yetu yanahuksika kwayo.

Jambo moja ambalo limekuwa la kawaida katika maisha ya Maimam (a.s.), kuanzia Amirul-Mu'minin Ali (a.s.) hadi kwa Imam al-Hujjah (a.s.) limekuwa ni uhifadhi wa msimamo wa kweli na halisi wa dini. Hii ni kwa sababu kioja hiki cha kubadili mikondo kilianza toka mwanzo kabisa katika ile siku ya kufariki kwa Bwana Mtume (saww) na dini ikapatwa na misukosuko mikubwa mara tu baada ya kuondoka duniani kwa Mtukufu Mtume (saww). Inakubidi utoe umuhimu wa hali ya juu kabisa kwenye suala hili kwamba kitendo hiki cha kubadilisha mikondo kilianza tangu wakati alipofariki Bwana Mtume (saww) na kinaendelea hadi leo hii, na kwa kweli kinaongezeka siku hadi siku.

Utakapotembelea Quba la Imam ar-Ridha (a.s.) utaona watumishi wanaofagia sakafu; mionganoni mwa watumishi hawa baadhi yao wanalipwa na baadhi yao wanafagia kwa msingi wa kujitolea. Kadhalika katika kitendo hiki cha kubadili mikondo vilevile kuna njia mbili ambapo ina maana kwamba kuna watu wanaolipwa ambao wanalipwa rasmi mishahara ili kubadili mikondo na kuwafanya watu watoke kwenye njia sahihi ya dini ambapo wengine wanafanya jambo hilohilo kwa kujitolea wakitoa huduma zao kwa kuli-chukulia kama ni tendo jema. Wanafikiri kwamba, kama tukiweza kuikiuka dini japo kidogo, tukafanya upotoshaji ndani yake, tukabuni fitna kiasi ndani yake na hata kama tukiweza kuwatoa watu kumi nje ya njia hiyo yatakuwa ni mafanikio makubwa kwetu sisi. Kitendo hiki kinaendelea tena kwa nguvu ya hali ya juu kabisa. Hatujawahi kamwe kufikiria kuhusu nukta hii, hatukufanya tahad-hari kwenye kitendo hiki ambacho kinaendelea kwa wingi katika zama hizi, kinaendelea wazi wazi kweupe, kwa namna zote, kuanzia kwenye mimbari, kutoka misikitini, kutoka kwenye madrassa za Kiislam, kutoka kwenye mihrabu, kutoka kwenye vitabu lakini hatuna hisia juu ya hili.

Kwa vile kitendo hiki kilitokea wakati wa Maimam watukufu pia, hivyo walikichukulia kama ni wajibu na kwamba Mwenyezi Mungu pia aliwapa wajibu huu wa kulibadilisha hili. Walikichukulia hiki kama ni wajibu wa kusahihisha huku kubadilika kwa mikondo kunakofanywa na serikali potofu na watu wachache waliopotolewa. Kama ilivyosemwa kabla, huku kubadili mikondo sio mabadiliko makubwa; mtekenyo kidogo wa mtarimbo na mkondo nao pia hu-sogea kwa sentimita chache, lakini huo hubadilisha mwelekeo wa treni na watu waliokaa ndani yake. Ili kuhakikisha kwamba hakuna uharibifu japo kidogo unaotokea, akili na uamsho vinahitajika. Hii ni kwa sababu watu wanaokaa ndani ya treni kwa kawaida huwa wanalala kinyume na mabasi na ndege ambamo kwa kawaida wanaku-wa wako macho kutokana na mirusho na hofu. Lakini ndani ya treni watu wanalala bila ya hofu na wanafurahia ule myumbo wa sampuli ya kwenye susu la kitoto wa treni, na jinsi njia za reli zinavyoende-lea kubadilishwa, na mwelekeo wa treni pia unabadilika lakini wao wanalala tu. Hali ya wafuasi wa dini inakuwa kama hivyo tu; wanabembea, wanasikiliza nyimbo za kubembeleza na kuingia kwenye usingizi mzito. Hawana hisia na mazingatio juu ya mwelekeo iwapo kama wanakwenda kwenye njia sahihi au kama imebadilishwa hapo katikati. Hivyo kama Maimam watukufu wasingetoa uthibitisho wa mwamko wao na wasingewasilisha haki za Uimamu basi leo hii ngozi yoyote ya dini halisi yenyе japo ufinyu inayoonekana sasa pia isingekuwepo. Hivyo mionganoni mwa juhudzi za Maimam (a.s.) juhudzi majawapo ilikuwa uhifadhi wa dini halisi. Kila serikali, watu binafsi, makundi, mashule, madhehebu, watu mashuhuri na vitengo wote kila mmoja anakwenda na mwelekeo wake kwenye njia tofauti lakini ndani ya yote haya, wajibu mkubwa kabisa ni kuihifadhi njia sahihi na sio kuiruhusu ipotee. Wakati watu wengine wanapokuwa wanajishughulisha na mambo mengine kwa jina la dini; kama vile inapokuwa ni zama ya fatwa, zama ya vita Tukufu (Jihadi), zama za

kukusanya ngawira za vita, zama za maslahi binafsi na wakati kila mmoja anapokuwa ameshughulishwa na mambo haya, hapo una-hitaji mtu ambaye wajibu wake ni kuihifadhi ile njia sahahi ya dini ili kwamba kutokana na kutojali na ile mishughuliko ya wengine, mkondo au njia halisi ya dini isije ikabadilika.

Kadhia hii ya Karbala ilitokea kwa ajili ya lengo hili tu. Wakati wa zama za Karbala mkondo ulibadilika sana kiasi kwamba treni la dini lilifika mbali sana juu ya mkondo potofu kwamba ilikuwa haiwezekani kulirudisha kwenye mkondo wake kwa kitendo cha kawaida tu. Hivyo mhanga mkubwa huu ultolewa kusudi dini iweze kurudishwa kwenye mkondo wake, na kwa mara nyingine tena watu walipata ile njia ya sawa na ile dini halisi hasa. Jambo hili liko katika maisha ya kila Maasumin na kwa uwazi wa dhahiri kabisa. Ni lazima izingatiwe pia kwamba matatizo na mambo yaliendelea kuongezeka katika zama za kila Imam aliyetokeza. Matatizo ambayo Amirul-Mu'minin (a.s.) aliyapitisha kwa Imam Hasan (a.s.) na mgogoro na mambo mapya yaliyojitekeza katika zama zake yote yalihamishiwa kwa Imam Husein (a.s.). Kwa njia hii, kila Imam aliyetokeza alirithi yale matatizo ya Imam aliyetangulia ambayo ina maana kwamba ukubwa wa matatizo uliendelea kuongezeka polepole. Hii ni kwa sababu zile athari za migogoro katika zama za Imam aliyetangulia zilikuwepo katika zama za Imam mpya na migogoro mipyä iliambatana na athari za migogoro ya nyuma hivyo kuzidisha uzito wa mambo ya kila Imam. Hivyo changamoto juu yao ilikuwa ni kukabiliana na mambo haya mazito na kuulinda Umma kutokana na migogoro hii na upotovu, na kwa hali hiyo kuhifadhi ile njia ya sawa. Kama njia iliyonyooka ikihi-fadhiwa, basi siku moja mtu atakuja kutembea juu ya njia hiyo. Sio lazima kwamba leo hii kama njia hiyo pia nayo ipo, na watu wa kupita juu ya njia hiyo wawepo pia. Wakati mwininge watu

hawako tayari kutembea juu ya njia fulani lakini ni lazima kuirithi kwamba huenda huko baadaye kinaweza kuja kizazi ambacho kitaitambua njia iliyonyooka na kutembea juu yake. Hili ni jukumu na wajibu kule kuihifadhi njia iliyonyooka.

## **JITIHADA ZA KUUNG'OA MFUMO WA WILAYA KATIKA ZAMA ZETU**

Matatizo yaliyoko ndani ya Jamhuri ya Kiislam ya Iran baada ya Mapinduzi ya Kiislam yenye ni somo tosha; tena yote haya yanahusika kwenye ukweli kwamba Mapinduzi ya Kiislam yalilenga na kuweka juhud katika kutekeleza Mfumo wa *Wilaya*. Ni lazima idhiihiriwe wazi kwetu sisi kuhusu njama na mipango ya maadui wa Mapinduzi na dini, zile mamlaka zenyet kiburi zilizonayo juu ya Iran; na wanashughulika kivitendo juu ya mipango hii. Kama una-vyoweza kuona baadhi ya mambo kwa uwazi kabisa, kuna uingiaji mkubwa wa bajeti ya kimarekani kwa ajili ya kueneza uharibifu wa tamaduni mionganoni mwa watu, na hilo nalo hususan ni kwa vijana. Mamilioni ya dola za kimarekani yanasantazwa ili kuwavuruga vijana wa Iran na kuwachochea dhidi ya Mfumo wa *Wilaya*, kuwaingiza wanawake wa Kiirani kwenye utovu wa staha na upujufu, kuwafanya vijana wa Iran kuwa waathirika wa madawa ya kulevyta, kueneza maelezo ya matusi ya kingono na lugha chafu; yote haya yanafanya na bajeti ya baraza la Congress la Marekani mahususi na iliyotamkwa wazi hadharani kwa ajili ya oparesheni za siri siri ndani ya Iran. Mbali na hii, bajeti isiyotamkwa hadharani ni kubwa zaidi kuliko ile iliyotamkwa katika kueneza mmomonyoko wa maadili ndani ya Iran.

## UVAMIZI WA TASNIA YA HABARI KWENYE UTAMADUNI

Wingi wa vituo vya TV vinalenga katika kuiharibu jamii hii. Wanazindua chaneli za Kifursi makhususia kwa ajili ya jamii ya Kiiran. Unaweza kujua kwamba Al-Jaziira inaanzisha chaneli ya TV ya Kifursi; hawahisi haja ya kuwa na chaneli ya Urdu lakini tayari wamekwisha kuanzisha chaneli ya Kifursi. Chaneli nyingine moja zaidi ya Kiarabu ijulikanayo kwa jina la al-Arabia imeanzisha chaneli yake yenyewe. BBC ina vipindi vitatu tu vya Urdu kila siku ambayo ina maana katika jumla masaa mawili ya matangazo hewani ya Kiurdu ambapo kwa Kifursi zaidi ya masaa nane ya programu zinarushwa hewani ingawa idadi ya wanaozungumza Kifursi duniani ni ndogo sana kuliko ya wanaoongea Urdu. Hata ukiangalia wa-Hindu wenye idadi ya watu bilioni moja duniani kote, bado ni aghlabu kuwepo matangazo ya kihindu ya BBC. Kadhalika uharibifu na upotoshaji vinatokea katika maeneo mengine vilevile.

## KUTANGULIZA DUNIA (*MATERIALISM*)

Msiba mmoja mwingine zaidi ambao umejitokeza ndani ya Iran na ambao umeenezwa kwa makusudi hasa ni kuhusu wale wana mapinduzi na watu wa dini ambao walitegemewa kutoa huduma kwenye mapinduzi hayo lakini wamegeuka wapenda dunia. Wao sasa wameelemea katika ulimbikizaji wa mali, faida za kidunia na rasilimali, majumba yenye mashamba na vyeo. Hizi ndio hasara ambazo zinaingizwa kwenye harakati baada ya kufanikiwa kwake na kuanzishwa kwake. Hii ndio sababu Imam Khomeini (r.a.) anasema kwamba kuleta mapinduzi ni rahisi bali kuyalinda ndio kazi kubwa

na ngumu sana. Wale wanaoyahami mapinduzi wanapaswa kuwa na nguvu sana, na ujasiri na usafi kuliko wale wanaoleta mapinduzi yenewe. Hii ni kwa sababu wale wanaoyalinda na kuyatetea mapinduzi wanakutana na yale matatizo pia ambayo wanamapinduzi waliyapitia walipokuwa wakileta mapinduzi na vilevile watakutana na matatizo mengine mengi zaidi. Hii ndio sababu ambayo kwamba wachache leo hii wanashughulika katika kuleta mabadiliko na ni wachache hawa tu wanaolinda mabadiliko hayo vilevile; walio wengi wanafuata tu. Hii idadi ndogo, taifa moja tu la Iran, inashughulika na linabeba mzigo juu ya mabega yao kwa ajili ya kukabiliana na ulimwengu wote mzima, kwa ndani na nje ya nchi. Lolote linalotokea huko nje unakuwa unalijua kwa kiasi fulani kwa sababu unasikiliza vyombo vya habari, lakini hiyo sio picha kamili, hawaelezi kila kitu. Lakini ngoja nikuwasilishie mtazamo wa juu juu wa kile kinachotokea ndani nawe hutaamini kiwango cha jinsi mambo yanavyofanywa kupotosha mapinduzi hayo na kuyatoa kwenye mkondo wake wa sawa.

## VYAMA VYA SIASA NA WATU

Kuna vyama vya siasa rasmi vilivyoundwa kutoka kwenye bajeti hiyo hiyo ambayo Congress ya Marekani imetoea kwa ajili ya kuedesha harakati za kichinichini ndani ya Iran. Kutoka kwenye bajeti hiyo hiyo, Vikundi vya kisiasa vinaundwa, wanasiasa, watu ovyo wasioaminika, watu wenyе kutaka majina ambaо hawana usuli (background) wa ama kisiasa au kielimu. Watu wasio na msingi kama hao walifanywa kama watu maarufu ili waweze kutekeleza majukumu fulani. Utakuwa unasikiliza habari hizi kila siku nyingine kwamba wagombea kwa ajili ya uchaguzi wamekataliwa na vyombo vya habari vinaieneza hiyo kwamba hakuna demokrasia ndani ya

Iran. Kukataa huku ni majibu na kunaashiria kwamba wagombea hawa ni mapandikizi yaliyowekwa. Hatua moja nyingine kubwa inayohusiana na hili ambayo ilichukuliwa ndani ya Iran kuyatengua mkondoni Mapinduzi ya Kiislam, na hatua hii ikawa yenyeshari sana katika miaka kumi iliyopita ilikuwa ni uundwaji wa vyama vyaya siasa ndani ya Iran na kuviunga mkono na kuvisaidia kiendelevu. Ulimwengu wa habari unapiga kelele kwamba hakuna haki za binadamu nchini Iran, hakuna uhuru; makelele yote haya ni kwa ajili ya wale walitengenezwa na wao tu na walio na baraka zao. Wakati watu na vikundi kama hivyo wanapodhibitiwa, wanapiga mayowe kwamba hakuna uhuru na haturuhusiwi kufanya kitu chochote. Hili ni jambo moja kubwa lililofanyika.

## MAGAZETI PINZANI NA MFUMO

Jambo jingine la pili kubwa ambalo limefanywa ni la harakati za magazeti. Magazeti machache kama hayo ambayo hakuna mtu anayeyanunua. Wakala hawa wa magazeti wanawantu makaratasimmatupu ya uchapishaji vilevile kutoka kwenye masoko binafsi kwa bei kubwa zaidi na wanayafanya yachapishwe katika ubora wa hali ya juu. Magazeti ya rangi yenyeshari ubora wa hali ya juu kama hiyo hayawezikuonekana katika maeneo haya ya dunia popote pale. Wale wanaojitokeza na magazeti haya wala sio waandishi wa habari, ni watu wa kawaida tu; karani fulani, daktari fulani, mhandisi fulani na watomakanao na taaluma nyingezo. Utakuwa umepata kusikia habari hizi kwamba katika siku moja tu magazeti ishirini na tano yalifungiwa nchini Iran.

## MAHDADIYAT (UFUASI WA MAHDI A.S.)

Jambo la tatu ambalo linafanyika kwa wingi sana ni kueneza, kuimarisha na kuunga mkono madhehebu mbalimbali na mitazamo tofauti tofauti kadhaa kwa jina la dini. Ngoja nikupe kadhia moja ya mfano iliyotokea mwaka wa jana. Kulikuwa na Kadhm Syed mmoja ambaye kwa sasa hivi yuko jela, alikuwa ni mwanachuoni, alikuwa amevaa kilemba na joho, ndevu za kupendeza na uso mzuri akiwa katika vazi la kimwanachuoni na pia ni msemaji mkubwa. Huyu alikuwa ni msemaji aliyekuwa akilingania itikadi maalum na dini mionganoni mwa watu kwa jina la Mahdiyat. Utaweza kuona iwapo faida kama hizo zinavunwa kutoka kwa Wasemaji wazuri na wakubwa kama hao katika nchi iliyodhibitiwa na kusimamiwa kama Iran, kisha uone ni kazi gani itakayochukuliwa kutoka kwa wasemaji wakubwa kama hawa nchini Pakistani au India. Alianzisha itikadi kwa jina la Mahdiyat. Kwanza alianza kuwaomba watu kuomba kwa ajili ya Imam wa zama hizi (a.t.f.s.), kumpenda yeye (a.t.f.s.); kukusanyika kwa ajili ya kumkumbuka kila Alhamisi usiku. Alianza pole pole kisha baadaye akachukua hatua kubwa zaidi. Watu hawa huwa hawazungumzi kuhusu ajenda zao katika ile siku ya kwanza. Wale ambao huongea kuhusu jambo la mwisho katika siku ya kwanza hawana elimu. Huna budi kungojea wakati unaostahili ili kuongea. Kama vile mtu unapokwenda kutafuta ndoa kwenye familia ya msichana, huanzi na majadiliano juu ya Mahari. Kwanza pata makubaliano ya uchumba yafanyike, hakikisha kama wapo tayari kumuvoza binti yao. Hawa waliitumia taratibu hii ya kuzungumza kuhusu jambo la mwisho katika ile siku ya mwisho na kidogo kidogo wakaleta mkengeuko wa kiiitikadi.

Mtu huyu yuko gerezani sasa hivi, na George W. Bush kwa mara kadhaa amelitumia jina lake kwenye hotuba zake akimzungumzia

kama ni mwanafikra mkubwa na Ayatullah. Bwana huyu amekiri kosa lake na video yake inapatikana pia katika mtandao. Amejifunza Uislam japo kidogo kwa miaka miwili tu na wala hawezি kuongea Kiarabu barabara. Jina lake ni Mohammed Ali Kazmi Burjerdi na amejifanya mwenye kuwa maarufu kama Ayatullah ul-Udhma Burjedi. Alidanganya na akasema, mimi ni mjukuu wa Marjaa mkubwa Ayatullah Burjedi ambaye kaburi lake lipo kwenye Quba la Bibi Maasumah (a.s.) huko Qum. Amekiri upangaji wa mipango yake ambamo kwanza aliwavutia watu kwake yeye mwenyewe kwa kutumia jina la Ayatullah Burjedi na kwamba watu watakapokuwa na mwelekeo kwake, mpango wake ulikuwa ni kuwakusanya watu takriban milioni kumi katika uwanja mkuu wa Tehran katika mwezi wa Shaaban chini ya jina la Imam wa zama hizi (a.t.f.s.) na kuanza maasi kutokea hapo dhidi ya serikali kwa kusema kwamba Imam (a.t.f.s.) amedhihiri na kwamba sasa serikali hii haina haki ya kuwepo. Jambo moja jingine la ziada ambalo alilifanya kama wote tunavyofahamu kwamba Imam Mahdi (a.t.f.s.) atakuja kudhihiri kutokea kwenye Ka'aba Tukufu iliyoko Makka, lakini kwa vile Ka'aba hiyo iko chini ya udhibiti wa Saudia na haiko huru kwa hiyo yeye akasema kudhihiri huko hakutafanyika Ka'aba hiyo. Yeye alisema kwamba Imam Mahdi (a.t.f.s.) amemwagiza yeye kujenga Ka'aba mpya kwa ajili yake. Huko Karaj, mji wa jirani na Tehrani kwenye milima, alijenga Kaaba na msikiti na akasema kwamba Imam (a.t.f.s.) amesema kwamba atadhihiri kutokea hapa. Huu ulikuwa ni mpango wake na mipango mingi kama hiyo ya madhehebu za kiitikadi potovu zinatengenezwa kwa uvezeshwaji na Marekani.

## SUFIYA

Sasa hivi kama utafika Qum, kuna barabara karibu na hiyo Quba ambayo jina lake la sasa ni “Barabara ya Ayatullah Marashi” na jina la zamani ni Eram Road. Kuna maktaba mashuhuri ya Ayatullah Marashi vilevile kwenye barabara hiyo, na majengo machache kutoka kwenye maktaba hii unaweza kuona kiwanja cha wazi. Kiwanja hiki katika miaka miwili kabla kilikuja kugeuka kuwa chaka la Masufi, ma-Qalandar na Watawa. Waliwakusanya watawa wote, wenye busara na Masufi kutoka kote nchini na wakawapa silaha za majambia, panga na wakaupa changamoto mfumo wa utawala. Msukosuko ulifanyika lakini kwa namna fulani watu na polisi walividhibiti watu hawa. Kikundi hiki kilikuwa kinaitwa kwa jina la Sufiya na tukio hili liliuja kwenye vyombo vyaya habari vyote. Hii ni mifano ya kuweza kuelewa ni aina gani ya majoribio yanayofanywa ili kuitengua ile njia ya kimapinduzi ya Uislam halisi na wa kweli.

## ANJUMAN AL-HUJJATIYAH

Mbali na hili harakati moja zaidi ambayo ilianza kabla ya Mapinduzi ya Kiislam na ambayo ilipungua nguvu wakati wa ujio wa mapinduzi, sasa inaanza kupata kasi tena na kuwa na nguvu zaidi. Kulikuwa na taasisi moja huko Iran kwa jina la *Anjuman al-Hujjatiyah* ambayo iliundwa na mtu Mtukufu kabisa katika Iran. Hakuwa mwachuono bali alikuwa msemaji, mkumbushaji (dhakir) na kaburi lake liko Tehran. Alionyesha mwonekano wa nje wa kiuchamungu sana na akajithibitishia shaksia ya utukufu. Alichukua fursa ya haiba yake ya uchamungu na utukufu katika kukusanya watu karibu naye. Hujjatiyah inatokana na neno Hujjah ambalo linamaanisha Imam wa zama hizi (a.t.f.s.). Kwa vile Imam Mahdi (a.t.f.s.) ni Hujjah ya Al-

lah, hivyo alikifanya kikundi hiki kwa jina la Hujjatiyah ambalo lina maana ya wafuasi wa Imam Mahd (a.t.f.s.), na kuitia kundi hili akaunda namna ya fikra fulani maalum kabisa.

Alianza kutangaza mawazo yake kabla ya mapinduzi, lakini wakati mapinduzi yalipotokea mawazo haya yalifisia bali sasa tena yanaanza kupata mashiko ndani ya Iran. Mawazo ya *Anjuman al-Hujjatiyah* ni ya hatari sana na yanababisha matatizo mengi katika baadhi ya nchi, hususan India na Pakistan. Ndani ya nchi ya Pakistan sasa hii imeanzishwa na imechangamka. Sasa hivi usiulize ni nani anayeunga mkono hili ndani ya Pakistan. Kila tunapokuja kujua kitu kipyaa ama cha kipekee tunakuwa kama waandishi wa habari na moja kwa moja tunauliza ni nani anaunga mkono hili? Hebu fikiria, hata kama ukiwajua wanaunga mkono hilo, halafu ndio wewe utafanya nini? Kwanza ni muhimu sana kuzielewa dalili za fikra hii; inaweza ikafanywa na baadhi ya watu, pengine na Majini fulani, baadhi ya wanachuoni, wajinga fulani, msikiti fulani, Madrassa fulani zinaweza kuwa nyuma ya hili na inaweza ikawa ndani ya eneo lolote maalum. Lakini kwanza hebu tuelewe alama tambulishi za fikra hii hatari ili wakati wowote unapokutana na alama hizo uwe huna budi kutambua kwamba hii ni *Anjuman al-Hujjatiyah*.

Fikra na mawazo yaliyokuweko kwenye kundi hili ni kwamba kusiwe na mageuzi yoyote ya kijamii yatakayofanyika wakati wa Ghaibu kubwa (Ghaibat al-Qubra). Msilete mabadiliko yoyote kwa sababu mabadiliko ya kijamii yatachelewesha wakati wa kudhihiri kwa Imam (a.t.f.s.). Hii ni kwa sababu sharti la kudhihiri kwake ni kuenea kwa dhlulma na uonevu duniani kote. Kutokea hapa zinazuka aina mbili za itikadi. Moja ni kali sana na hiyo nyingine imepoa kidogo. Hiyo aina kali sana ya fikra hii ni kwamba sio kwamba tukae kimya tukisubiri udhihiri wake bila ya kufanya mageuzi yoyote ya kijamii bali badala yake inatubidi kusaidia na kuunga mkono katika

kueneza dhulma, utovu wa heshima na adabu na tunapaswa kuizamisha dunia yote kwenye maovu ili kwamba ile hali ya sharti la kudhi-hiri itimizwe kikamilifu. Fikra na mawazo yao kuhusu wana-mapinduzi ilikuwa kwamba kwa vile hawa watu wa mapinduzi wanazuia dhulma, basi kwa hakika wanazuia kudhihiri kwa Imam (a.t.f.s.). Uadui wao juu ya Imam Khomein (r.a.) ulikuwa katika msingi huohuo wa kwamba Imam (r.a.) amechelewesha kudhihiri kwa kufanya kazi hii ya kimageuzi chini ya jina la Mapinduzi ya Kiislam.

Hivyo kuna sura mbili za fikra ya Hujjatiyah; moja ni kwamba tusifanye kazi yoyote ya kimageuzi kwa vile yote haya ni katika wajibu na majukumu ya Imam (a.t.f.s.) na yatatokea tu katika wakati huo na inakatazwa kufanya mambo kama hayo kabla ya kudhihiri kwake. Na ile sura ya pili ni lilikuwa ni daraja kuhusu hili ambamo wao wanataka kufanya mambo maovu ambayo yatasogeza karibu kudhihiri kwa Imam (a.t.s.f.). Jukumu lako wewe ni kuswali na kuomba du'a kwa ajili ya Imam (a.t.f.s.), kuelezea sifa zake bainifu na tabia na kisha ukae kimya na ungojee tu ni lini kudhihiri huko kutakapotokea.

Dalili nyingine ilikuwa ni fikra yao kwamba Dini haihusiki chochote na Siasa. Hizi ndio kanuni ambazo kwazo hizo kundi hili la Hujjatiyah hukamatika. Wao wanasema kwamba Dini imetakasika na siasa ni mchezo mchafu hivyo viwili hivyo havina uhusiano kabisa. Kuhusisha dini na siasa, kwa muono wao, ni uzushi (biddah) na ni jambo lisilo sahihi. Kisha wanasema kwamba hakuna uhusiano kati ya madhehebu mbalimbali za Kiislam na ulimwengu wa Kiislam, na pia hairuhusiwi kuunganisha madhehebu mbalimbali au Ummoja wa Kiislam unakatazwa kabisa. Na tunapaswa kulaani dhidi ya hilo, tukashifu na kuzishutumu madhehebu nyinginezo za Kiislam kwa kiasi inavyowezekana na kwa uwazi kabisa ili umbali baina ya madhehebu upate kuongezeka zaidi. Haya ndio mawazo

yao ambayo yanaenezwa huko Iran tena na hata sasa katika Hauza. Kama inavyosemekana katika miaka michache iliyopita, yameanza huko Pakistan vilevile na unaweza ukayatambua kwa alama na kawnuni zilizotangulia kutajwa. Yamekuwa yakienea nchini India pia kwa zaidi ya miongo miwili sasa.

## UTAWA BANDIA

Upenyezaji mwagine unaofanyika ndani ya Iran ni uundwaji wa itikadi nyingine moja potovu kama hiyo ambayo ni utawa (irfan), utawa wa bandia haswa. Marjaa na Imam wa Ijumaa wameonyesha unyeti wa hisia kwenye msiba huu tangu miaka michache iliyopita, na wamekuwa wakiwajulisha vijana na watu wa kawaida kwamba huu ni mtego waliowekewa kwa jina la utawa bandia. Vijana wadogo wa kiume na wasichana wanatekwa nyara kwa njia ya hilo jina la utawa, na aina ya mafunzo kama hayo inatolewa kwao ambayo haina uhusiano wowote na dini, na matokeo yake ni mmomonyoko wa maadili. Tukio moja la mfano kama huo lilitokea mjini Qum ambamo mtu mzima mmojaa alijitangaza yeye mwenyewe kama mtawa mtukufu. Baadaye aina ya uchafu na upotofu aliokuwa amejiingiza nao kwa vijana hawahawa ukaja ukafichuka!

## MWENENDO MBAYA KATIKA MAOMBOLEZO

Kama hivi, katika kila sehemu ya dini mikengeuko kama hiyo inafanyika, kwa mfano katika taratibu za maombolezo na mahuzuniko kwa ajili ya marehem hasa katika mwezi wa Muharram, huko Iran miaka miwili iliyopita, wahadhirii (watunzi wa marsia za maombole-

zo) walibuni mtindo mpya ambao kwa hakika sio usomaji wa marsia bali ni muziki wa kisasa ambao uliwasilishwa kwa watu katika jina la Maimam (a.s.), dansi, mitikisiko, hafla za shamrashamra zilikuwa zikifanyika rasmi kwenye matukio ya sherehe za maadhimisho ya kuzaliwa kwa Maimam (a.s.).

## **MAHDI WENGI WA BANDIA**

Halafu jambo jingine ambalo limekuwa la kawaida sana lilikuwa ni kujitangaza kwa Mahdi wa bandia wengi tu, na kuna mamia ya wasingiziaji kama hao walioko kwenye selo za mahabusu sasa hivi. Kwa kweli, hata mwanamke mmoja alidai kuwa yeye ni Mahdi ingawa kila mtu anatambua kwamba Imam Mahdi (a.t.f.s.) ni mwanaume; kwa vile tu wanawake wanataka kuwa bega kwa bega na wanaume yeye alijitokeza mbele kwa kiasi kama hicho. Mzaha mwingine ulio-jitokeza mjini Qum ulikuwa wa mtu mmoja aliyeeneza taarifa kwamba Imam Mahdi (a.t.f.s.) amefariki dunia na kwamba amemteua yeye kuwa mwakilishi wake kwa ajili ya kusimamia mambo yote. Alifunga sura au mlango mzima wa mambo yanayomhusu Mahdi na huko kudhihiri kwenyewe. Maongezi kama hayo yanaendelea hapa ndani ya Iran na kuungwa mkono kwa nguvu sana na baadhi fulani ya vikundi vyta kidini, vyama, vikundi vyta kisiasa, channeli za radio/TV, magazeti na majarida. Upotofu kama huu unasimamiwa na kufadhiliwa kifedha na mabepari na vikundi vyta matajiri.

Kwa upande mmoja wana uvamizi wa kitamaduni wa kichochezi kwa magazeti na majarida mbalimbali, halafu kwa upande mwingine wana uundaji wa vikundi vyta kidini na itikadi zilizopotolewa. Kwa nini yanafanyika yote haya? Hii inafanyika ili kwamba miongoni mwa yote haya, ile njia ya mapinduzi, Uislam Halisi na Mfumo wa *Wilaya* vipate kupotea. Hii ni mbinu ambayo kwayo unafanya

makelele mengi sana, unatengeneza madhehebu mengi sana, kuno-nyesha njia nyingi za upinzani kiasi kwamba watu wanakuja ku-changanikiwa wasijue ni njia ipi iliyo ya sawa?

Unauna mkanganyiko huohuo katika dini yako vilevile. Viana wanakuja na kusema kwamba wanachuoni fulani wanasema hivi na baadhi yao wengine wanasema vingine kabisa na tunakuwa hatuwezi kuelewa ni nani yu sahihi na nani yu mwenye makosa. Wamezitengeneza sauti hizi zinazotofautiana na kupingana kwa ajili ya kupata haya matokeo ya kisaikolojia tu. Wakati baadhi wakisema jambo hivi, wengine wanasema jambo jingine kabisa halafu miongoni mwa ikhtilafu zote hizi za maoni, vijana wanashindwa kuigundua njia ya sahihi. Sio muhimu kwamba makundi tofauti yote haya na madhehebu yanaundwa kwa lengo la kumiliki madhehebu mengine; haya yameundwa hasa kwa ajili ya kusababisha kelele ili kwamba sambamba na sauti ya haki, sauti za bandia zianzishwe ili kusababisha mchanganyiko katika akili za watu na wasiweze kuelewa njia ya kweli ni ipi mojawapo? Ni sawasawa na vile wanavyofanya hasa wanasiasa; siku moja mwanasiasa mmoja atasema jambo, siku nyingine mwanasiasa mwingine atasema kitu tofauti kabisa. Siku moja, Qadir Khan atatoa kauli na siku ya pili Jenerali mmoja atasema jambo tofauti, na Umma wote unapata kuchanganyikiwa kuhusu nguvu za Atomic za Pakistan. Wakati sauti bandia chache kama hizo zikiamshwa, zile sauti za kweli huwa zinazimishwa. Watunga sera wa Bani Umayyah na Bani Abbas waliifanya kazi hii ya kukandamiza sauti na mawazo ya Maimam Watukufu (a.s.) kwa mafanikio makubwa. Hii ina maana ili kuukandamiza Uislam wa Mtume, Uislamu halisi, waliendeleza katika kila zama za Maimam sauti kama hizo, ili kusababisha vurugu, na kuunda madhehebu na makundi ambayo kwayo sauti za Maimam zikomeshwe na kukan-damizwa.

## KUUHIFADHI MFUMO WA *WILAYA*

Wakati mambo kama hayo yakinuka kila mahali kila mtu ameshika lake inakuwa ni muhimu kwamba kundi moja lipaswe kusimama na kujaribu kuilinda ile njia ya haki, ikihakikishwa kwamba ule mwelekeo sahihi wa fikra usije ukasombwa katika hali hii ya vurugu, machafuko na ya hofu kubwa. Isije ikatokea kwamba mambo haya yakachanganyika na ule mwelekeo halisi wa dini ukapotea mionganoni mwa hii mielekeo mingineyo. Kama kuna mstari umechorwa juu ya karatasi na endapo mtu akaja akachora mistari mingi mingine karibu na huu mstari wa kwanza kabisa, sasa huo mstari wa kwanza una-potea, itakuwa ni vigumu kabisa kutambua ni mstari upi uliochorwa mwanzoni, na itakuwa ni kitendawili hasa.

Hii ni kazi ya kisaikolojia na inapofanywa katika itikadi, mawazo, na mitazamo, basi hubadilika na kuwa kitendawili; maana ya kitendawili ni jambo ambalo linasababisha mkanganyo na jambo ambamo mwanadamu anakosa kuipata njia iliyonyooka. Kazi hii inaendelea kwa shari sana dhidi ya Mfumo wa *Wilaya* na mapinduzi ya Kiislam kote duniani, na hususan ndani ya India na Pakistani. Vitendawili vinafanywa kuhusiana na mapinduzi; aina mbalimbali za sauti zinainuliwa, minong'ono inatengenezwa, simulizi za zamani za kale zinasimuliwa na kufanywa za kawaida ilimradi tu mazingatio ya Umma yanakengeushwa; kama lile suala la Shahada ya Tatu lilivyokuwa limeanzishwa ambapo kundi moja likawa lenye kuunga mkono na jingine likawa pinzani. Ni kwa mambo haya yasiyo na muhimu wa maana ambapo kwamba ile sauti ya Uislam wa kweli na halisi, yale mapinduzi na shauku ya kuelekea kwenye Mfumo wa *Wilaya* ndipo vinapata kukandamizwa na kuzimwa.

Ille simulizi ya *Anjuman al-Hujjatiyah* imetulia bwete baada ya yale Mapinduzi ya Kiislam ya ndani ya Iran, na pindi wakati Imam

(r.a.) alipokuwa yupo, wao walikuwa hawana hata ujasiri wa kuchukua jina lao kwa sababu Imam (r.a.) alikuwa macho sana kuhusu kundi hili. Wale wenye mawazo huru – maliberali na akina *Anjuman al-Hujjatiyah* wanazungumza jambo moja; tofauti tu ni kwamba mmoja anazungumza kwa mukhtadha wa kidini na mwingine nje ya dini. *Anjuman al-Hujjatiyah* wanasema kwamba dini haina uhusiano na siasa wakati ambapo uliberali pia unasema vivyo hivyo kwamba dini na siasa ni vitu mbali vilivyotengana. Hitimisho ni kwamba mmoja anasema dini imetengana na siasa wakiwa kama watu wa dini, ambapo wengine wanasema yayo hayo kwa kuingia kuwa mwansasiasa. Wote hawa wananolisema ni moja lilelile, hivyo nukta muhimu hapa ni kwamba wakati wowote watu wa dini na wasiokuwa wa dini wanapoungana, basi hakuna kuhusu dini litakalozungumziwa hapo. Ni kama kusema kwamba dini, kwamba waumini waungane na wasiokuwa waumini, na imani na ukafiri havina budi kuungana, kama inawezekana.

Kwa sasa hivi kuna haja kubwa sana kwa ajili ya uhifadhi wa njia ya kweli, ile njia ya mapinduzi na Mfumo wa *Wilaya*. Juu ya sifa zote kwa Mwenyezi Mungu, wale watu wenye uwezo wapo hapa wakiyalinda, ambao walileta yale mapinduzi, na watakuwa wakiyalinda huko baadaye pia. Mwenyezi Mungu atawajaalia na uimara na uvumilivu. Wakati watu mashuhuri wengi wamekengeuka, ili-kuwa ni rehema za Allah kwamba amelipa taifa hili Rais ambaye anazungumza kuhusu Mwenyezi Mungu tu, ambaye anazungumza kuhusu dini, mapinduzi na mfumo wa *Wilaya* tu, hawadanganyi watu na anaongea mambo yaliyonyooka moja kwa moja. Huu ni uthibitisho kwamba njia hii ya *Wilaya* itabakia hai hapa, lakini hakuna uthibitisho wa uhakika kuhusu sehemu nyingine ambako angalau sauti ya *Wilaya* haijafika sawasawa. Hivyo ni wajibu wetu kuihifadhi njia ya *Wilaya* katika sehemu hizi ambako kuna machafuko ya

kiitikadi. Hivyo pale inapokuja kwenye utambuzi wa dini na *Wilaya* panakuwepo na sehemu mbali ambamo watu fulani binafsi wana-hitaji kuja chini ya dini na kuihifadhi hiyo katika mazingira haya yaliyochafuka. Kama sio leo, basi ni kesho kwamba hii njia ya kweli itakuwa na manufaa kwa kizazi kijacho. Hii ni kwa sababu ni ahadi ya Mwenyezi Mungu kwamba kama hamtasimama na hamtatoka nje ya nyumba zenu, basi Mwenyezi Mungu atawaleta watu badala yenu ambao watampenda Mwenyezi Mungu, naye Mwenyezi Mungu atawaridhia. Watakuwa ni watu ambao kwamba watatembea kwenye njia hii na kuelekea kwenye sehemu za kuuliwa na kuchinjwa kwao kwa miguu yao wenyewe. Hivyo hatuna budi kuihifadhi dhamana hii kwa ajili ya watu hawa wanaokuja baadaye na ni wajibu muhimu juu yetu sisi. Hili lilikuwa ni jukumu ambalo Maimam wetu wote (a.s.) waliliwasilisha. Hebu tuchukue mfano kutoka kwenye zama za Imam Haadi (a.s.):

## MAMTUURA – JAHILI MCHAFU

Katika wakati wa zama za Imam Haadi (a.s.), fikra zote hizi tofauti tulizozijadili kabla zilikuwepo. Uliberali ulikuwepo, Usufi ulikuwepo na makundi mengi mengine yalikuwepo. Kulikuwa na madhe-hebu nne au tano za kiitikadi zenye nguvu sana katika wakati wake, ambazo ziliundwa na kusaidiwa na kuimarishwa na Bani Abbas ili kwamba Ush'ah uzimwe na msimamo wa Uimam upate kuzimwa pia. Walifanya yote haya kwa ushari kabisa na wakazalisha Mamullah wakubwa wengi na wasemaji fasaha ili waweze kutoka na kufanya makelele; na ndani ya makelele haya ile njia halisi na ya kweli iweze kukandamizwa na kuzimwa. Mionganoni mwa makundi haya yaliyoundwa, moja lilikuwa ni Usufi uliokengeuka na jingine lilikuwa ni la wakuza mambo – wapiga chuku (Ghulat). Haina budi

ifahamike kwamba mbele ya Imam (a.s.) walikuwepo watu ambao walikuwa wanazidisha ubora wa Imam Ali (a.s.). Kisha kulikuwa na waliojifanya kuwa ni upinzani, kwamba wangeweza kuleta upinzani juu ya Imam Ali (a.s.) na kumshutumu yeye kama mtu wa kupenda dunia, hajizuii na maisha ya kidunia, na shutuma nyingi kama hizo zilitolewa juu ya Imam Ali (a.s.).

Mbali na haya, upotofu mmoja zaidi ambao ulikuwa ukiendelea kwa nguvu wakati ule na ambao dhidi yake Imam Haadi (a.s.) alionyesha upinzani juu yake, ulikuwa ni chuki dhidi ya Ahlul-Bayt (Naasibiyat). Kundi hili lilikuwa ni urithi wa Bani Umayyah, lakini Bani Abbas hawakulifuta; ingawaje hao Bani Abbas walikuwa kari-bu zaidi na Ahlul-Bayt (a.s.) wakilinganishwa na hao Bani Umayyah lakini bado hawakuweza kuwaangamiza maadui wa Ahlul-Bayt (a.s.). Kundi hili liliundwa na Bani Umayyah na Bani Abbas badala ya kulisafisha kabisa waliliacha libakie na kwa kweli walilitumia katika matukio mbalimbali. Ni kama vile tu wanavyofanya wanasiasa wa zama zetu hizi; wanatumia vikundi fulani vya itikadi za kidini kwa kuwaweka mbele katika baadhi ya matukio.

Kwa hiyo hao “*Naasibi*” walipata fursa kutoka kwa Bani Abbas na wakawatesa vibaya sana Shi’ah wakati wa zama za Imam Haadi (a.s.). Kiwango cha ukatili kilichofanya juu yao na yale matatizo yaliyoundwa kwa ajili ya Imam Haadi (a.s.) yalikuwa kwa kiasi kwamba hata kama Imam (a.s.) angeyaacha majukumu yote mengine na akafanya kazi ya kuyapinga tu, ingekuwa ni halali. Kulikuwa na kundi jingine ambalo lilikuwa pia ni matokeo ya fikra za kisiasa za Bani Abbas na lilikuwa ni kikundi cha Shi’ah kilichopotoka. Kundi hili lilikuwa ni lile la Madhehebu ya *Waqfiyah* ambalo lilianzishwa wakati wa zama za Imam ar-Ridha (a.s.).

Kundi hili liliundwa na mmoja wa wawakilishi wa Imam Musa al-Kadhim (a.s.) baada ya Shahada yake. Kundi hili lilikataa kumtam-

bua Imam ar-Ridhaa (a.s.) kama Imam na likadai kwamba Imam Musa al-Kadhim hajafa na kwamba hajauawa kishahidi bali amekwenda kwenye ulimwengu usioonekana (Aalam al-Ghaib). Yeye (a.s.) atakuja kutokeza tena hivyo hatumkubali Imam Ridhaa (a.s.) kuwa kama Imam wetu. Walikuja kukabiliana na Imam Ridha (a.s.) kwa kuunda madhehebu ya kidini kwa jina la *Waqfiyah* na wakapata nguvu ya kutosha hadi zama za Imam Haadi (a.s.).

Imam Haadi (a.s.) alitumia jina maalum juu ya kundi hili. Hatuna rejea yoyote iwapo kama Imam Haadi (a.s.) alikuwa amewapa jina hili lakini vyanzo vya kuaminika vipo kwamba Imam Haadi (a.s.) aliwarejea kwa jina hili na aliwaelekeza watu kuwajua hao kwa jina hili. Kutowana na hili inaweza kufasiriwa kwamba Imam Haadi (a.s.) mwenyewe huenda aliwapa jina hili. Jina hili lilikuwa ni “*Mamtuura*.” Neno hili linatokana na neno la Kiarabu, *Mutir* ambalo lina maana ya mvua. *Mamtuura* maana yake ni kitu ambacho juu yake kimemwagikiwa na maji ya mvua; kitu ambacho kimeloana katika maji ya mvua yanayodondoka huwa kinaitwa *Mamtuura*. Jina hili la *Mamtuura* kwa lugha ya Kiarabu linatumika makhsusi kwa mbwa jike ambaye amesimama kwenye anga wazi, analoweshwa na maji ya mvua yanayodondoka kisha anatafuta kivuli ambacho chini yake anakung’uta mwili wake ambapo yale maji kutoka kwenye mwili wake yanaruka juu ya kila kitu kilicho karibu naye. Mbwa ni mchafu kiasi cha kuwa ni Najisi, na utakuwa umeliona hili la kwamba wakati mbwa anapoloa, basi kwa lengo la kukauka, huwa anatingisha na kukung’uta mwili wake; matone ya maji yanayoruka kutoka kwenye mwili wake na kisha kukifanya kila kitu karibu yake kuwa Najisi. Mbwa huyu aliyeloweshwa na maji ya mvua huwa anaitwa *Mamtuura*.

Imam aliwawekea jina hili na wafuasi waliomzunguka Imam (a.s.) walikuwa wakiliita kundi hila la *Waqfiyah* kwa jina la *Mam-*

*tuura.* Hawa ni wale watu wenye mawazo ya kijinga na machafu ambao wakati wowote ule, pale wanapoingia kwenye mkusanyiko wa waumini na kisha wakafungua midomo yao, basi wanalifanya kusanyiko lote kuwa Najisi. Hawa *Mamtuura* husababisha shaka, wasiwasi na dhana katika akili za watu waaminifu hususan kuhusu Uimam na Mfumo wa *Wilaya*. Hii ilikuwa ni kwa sababu fikra zao zilikuwa ni kwamba baada ya Imam Musa al-Kadhim (a.s.) hakuna Imam mwingine tena. Ni sawa na Imam Khomein (r.a.) ambaye ni mwakilishi wa Imam (a.t.f.s.), mwakilishi wa msimamizi wa mambo (*Uluul Amr*) lakini bado kuna baadhi ya wanaokuja kuuliza, ni kwa nini mnalitumia neno hili Imam juu ya Imam Khomein (r.a.)? Hili ni swali la kweli ambalo tunalihusisha kwa mtu asiyé Maasum kama Imam, na inatubidi kuwa na majibu juu ya hili, na majibu yenewe yapo. Lakini madhehebu hii ya *Waqfiyah* ilikuwa ikiuliza swali hilo-hilo la kwa nini watu wanawaita Imam Ridha, (a.s.), Imam Jawad (a.s.) na Imam Haadi (a.s.) kwa cheo cha Imam? Hii ilikuwa miongoni mwa ulinganio na mahubiri ya kundi la *Waqfiyah*, kwamba kwa nini watu wawaite hao kwa jina la Imam? Walikuwa wakisema kwamba Uimam umeishia kwa Imam Musa al-Kadhim (a.s.) na sasa cheo hiki cha Uimam hakimstahili mtu yejote mwingine. Hamuwezi kumwita mtu mwingine yoyote yule Imam tena. Hii ndio iliyokuwa sababu ya Imam (a.s.) kuweka jina hili la *Mamtuur* kwa ajili yao na wakati wowote ulipofanyika mjadala wowote kuhusu wao walikuwa wakitajwa kwa jina hili na sio lile jina lao halisi la madhehebu ya *Waqfiyah*.

Kama mtu angekuja na akauliza, ni nini kifanyike juu ya hawa *Mamtuur*? Mwelekeo wetu uwe ni upi kuwalusu wao? Msimuliaji mmoja anasema kwamba, nilimuuliza Imam Ali (a.s.) endapo kama ninaweza kuwalaani *Mamtuura* wakati wa du'a ya kunuti yangu? Imam (a.s.) akajibu kwamba kwa hakika unapaswa kuwalaani hasa.

Ni lazima umlaani *Mamtuura*, huyu mbwa jike aliyeloa mvua. Kwa nini? Hii ilikuwa ni kwa sababu hii madhehebu ya *Mamtuura* ili-kuwa ndio tishio kubwa kwenye Mfumo wa *Wilaya*, Uimam na njia ya *Wilaya*. Hii ndio madhehebu chafu kabisa na mahali popote walipokwenda hawa *Mamtuura* walieneza uchafu. Madhehebu hii imesababisha mkanganyiko mkubwa katika akili za watu kuhusu Uimam. Ni muhimu kuzingatia jambo hili kwamba *Waqqiyah* ilikuwa ni kundi la Shi'ah ambapo huko nyuma kulikuwa na vijitawi vingine vya makundi ya Shi'ah pia kama Ismailiya, Zaidiya, Fat'hiya, Sufiya, Ghaali na matawi mengine mengi ya Shi'ah; na yote yaliku-wepo wakati wa zama za Imam Haadi (a.s.) yakieneza upotofu na udanganyifu wao.

Wakati zilipofika zama za Imam Haadi (a.s.) makundi yote haya yalikuwa yakitema sumu zao na yalikubaliana juu ya hoja ya kwamba Imam Haadi (a.s.) hakuwa ni Imam. Zaidiya nao walisema vivyo hivyo, Ismailiya wamesema hivyo, Fat'hiya, Sufiya na hata hao Ghaali wamesema hayo hayo, kwamba Imam Haadi (a.s.) sio Imam hasa. Bani Umayyah na Bani Abbas, wote walikuwa na maoni hayo hayo ya kwamba hawa Maasumin sio Maimam. Ni lazima ikumbuk-we kwamba uadui kati ya Bani Umayya na Bani Abbas ulikuwa wa kiasi kwamba hawakuweza hata kukaa katika meza moja na kunywa gilasi ya maji, lakini inapokuja kwenye kuukataa Uimam, wao wanakubaliana kwamba Imam Haadi (a.s.) sio Imam. Haya ndio hasa yale yanayotokea leo hii pia ambapo haya makundi tofauti ndani ya Shi'ah ambayo yana uhasama binafsi dhidi ya kila mojawapo, yanaungana inapokuja kwenye kuushambulia Mfumo wa *Wilaya* na hususan huo Uongozi.

## UTARATIBU WA IMAM HAADI (A.S.) WA KUHIFADHI *WILAYA*

Zama alimoishi Imam Haadi (a.s.) zilikuwa ni kipindi cha zahama kali kupita kiasi, Serikali ya Bani Abbas iliendelea kubadilika kwa kasi na watawala wapya walikuwa wanafikia idadi ya 8 au 9 waliobadilishwa wakati wa kipindi cha Imam Haadi (a.s.). Mtawala aliye kuwa dhalimu mno, katili na muonevu kabisa aliyewahi kuja katika zama za Imam Haadi (a.s.) kutoka kwa Bani Abbas alikuwa ni Mutawakkil Abbasi. Kama ukitaka kumfananisha Mutawakkil na mtu mwingine leo hii, basi mtu huyo atakuwa ni George W. Bush. Huyu alikuwa ni mnyama, na ukatili alioufanya juu ya Ahlul-Bayt (a.s.) na wafuasi wao hauwezi kupimika. Wingi wa uhamaji wa kizazi cha Maimam (yaani, Masayyid) ulitokea hasa wakati wa zama hizi. Mutawakkil alikuwa ametoa amri kwamba popote pale kizazi cha Ahlul-Bayt (a.s.) kinapoonekana inapaswa kiangamizwe.

Mutawakkil alimhamisha Imam Haadi (a.s.) kutoka Madina kwenda Samarra na alikuwa amefanya mipango kamilifu na utaratibu wa kumuua Imam Haadi (a.s.) hapo Samarra. Baadhi ya watu walikwenda kwa Imam (a.s.) na wakamwambia kwamba kuna njama za namna hii ambazo zimepangwa kwa ajili yako. Imam (a.s.) akasema kwamba huyo hatafanikiwa kuniwa mimi na sitauliwa kwa mkoно wake. Watu wakashangaa wakimwambia kwamba hao maadui wamefanya mipango kamili kabisa na wewe unakuwa husikilizi na wala hujali kabisa! Imam (a.s.) akasema wao hawawezi kufanya chochote, na hilo kweli likatokea kwamba siku moja au mbili kabla ya utekelezaji kivitendo wa mpango huo, yeye mwenyewe Mutawakkil akauawa na mtu wa familia yake mwenyewe au kaka yake. Ingawa hakufanikiwa kumuua Imam Haadi (a.s.) lakini alimuweka chini ya mashinikizo mazito na makubwa.

Sababu ya kuyataja yote haya ni kwamba chini ya ukatili na unyama wa serikali hizi, shinikizo hili, masuala ya ndani kutoka kwenye machipukizi ya madhehebu ya Shi'ah, na maadui wa kiiitkadi wa Ahlul-Bayt (a.s.), Imam Haadi (a.s.) aliyapinga na kupigana katika kila uwanja wa mapambano. Lakini alama ya msingi ya makabiliano kutoka kwake ambayo tunayo pamoja nasi sasa ni Orodha ya Mpangilio wa Uongozi – manifesto. Hii ni kwa sababu mashambulizi makubwa kabisa yalikuwa juu ya Uimam. Makundi yote ya kisiasa na yasiyo ya kisiasa pia na madhehebu yameleta suala la Uimamu kwenye mjadala ili kuzusha ghasia na vurugu. Ingawa Imam Ridha (a.s.) alikuwa ameuwasilisha Uimam kwa namna nzuri kabisa kiasi kwamba mavumbi yote yaliyokuwa yamewekwa na watu juu ya kuwepo kwa Uimamu yaliondolewa. Hadith hii iliyotolewa na Imam Ridha (a.s.) kwenye Hotuba ya Ijumaa aliyoitoa wakati wa Muharram haikuacha uwezekano wowote ama shaka na dhana. Lakini bado hizi madhehebu kumi au kumi na moja na haya makundi potofu kwa pamoja yanajaribu kuushinda Uimam.

Imam Haadi (a.s.) chini ya mazingira kama haya alifanya kitendo cha kimujiza kabisa; kitendo cha kiongozi, mwongozu ambao ulilinda na kuudhibiti Uimam hadi leo hii. Uimamu hautakabiliwa na tatizo la kiiitkadi au kimuono baada ya hili. Na hii ilikuwa ndio *Orodha ya Mpangilio wa Uongozi – manifesto.*, inayo julikana kama *Ziarat al-Jamia al-Kabiir*.

Ni bahati mbaya sana kwamba Ziarat hii imeandikwa katika *Mafatih al-Jinaan*, kwa sababu hiyo *Mafatih* imegeuzwa kuwa ni kitabu cha visomo vya mdomo tu ili kujipatia thawabu. Sio kitabu cha kisiasa bali ni kitabu cha ukumbusho wa mdomo juu ya Allah kupita du'a. Hapana shaka kwamba watu wazima hawa wamefanya kazi ya kutukuka mno ya kukusanya du'a na Ziarat hizi pamoja, bali kwa bahati mbaya imegeuka kuwa ni chanzo cha kujipatia thawabu

tu basi. Ndio kitabu kinachosomwa sana miongoni mwa Shi'ah. Na kwa vile *Ziarat al-Jamia al-Kabiir* imo ndani ya *Mafatih*, basi tunaisoma hii pia kwa ajili ya kuvuna thawabu tu ambapo Imam Haadi (a.s.) mwenyewe amesema kwamba wakati wowote mnapotembelea kaburi la Maasum yoyote yule basi mnapaswa kusoma hati hii. Hii ndio manifesto ya utaratibu wa Uimamu ambamo ule mtiririko halisi wa Uimam umehifadhiwa na Imam (a.s.) katika hati hii. Ni msiba ulioje kwamba tumeigeuza manifesto hii kwenye visomo vyta mdomoni tu kwa ajili ya kusaka thawabu. Imam aliihifadhi itikadi ya Uimamu na *Wilaya* ndani ya hati hii; na akawapa habari wafuasi wake na Shi'ah kwamba wakati wowote wanapotembelea kaburi la Maasum yoyote yule basi wanapaswa kusoma hati hii.

---

## MFUMO WA WILAYA – MFUMO WA UIMAMU NA UMMAH

---

**H**ati hii ina sehemu mbili; sehemu ya kwanza ni utambulisho wa Maimam ambamo baadhi ya uadilifu, tabia, sifa bainifu, hadhi na cheo cha Maimam vimeainishwa. Sehemu ya pili ni kuhusu Umma. Kwa maneno mepesi wakati unapotembelea kaburi la Imam yoyote yule (a.s.) na kusoma sehemu ya kwanza ya hati hii; mwenye kuzuru anapaswa kujua amesimama mbele ya nani? Ambapo sehemu ya pili itamjulisha ni kwa nini amekuja? Kama vile tunavyomtembelea mtu, huwa linaulizwa swalii la kwa nini umekuja. Kama majibu ni sijui, basi yule mtu aliyetembelewa anaweza akakuambia kwamba kama huna shughuli yoyote ni kwa nini umekuja hapa?

Sehemu ya kwanza ya *Ziarat al-Jamia al-Kabiir* inatambilisha watu hawa ni akina nani hasa, tumesimama mbele ya hadhira ya nani? Kisha ni lazima tutambue, ni kwa nini tumekuja kwenye kaburi Tukufu hili? Hatukuja kuangalia ni uzuri kiasi gani kaburi hili na ujenzi wa msikiti huu vilivyojengwa. Tumekuja mbele ya kiongozi, mwongozaji, Imam; hivyo ni nani anayekuja kwa Kiongozi? Ni Umma ndio unaokuja kwa Kiongozi. Kwa nini? Sio kwa ajili ya kupata tiba ya maradhi yetu ya kimwili. Kaburi hili sio hospitali. Watu wengine wanadhani kwamba Haram ya Imam ni Hospitali na kwamba tunakuja kutibiwa kwa ajili ya matatizo yetu ya kiafya; hasa kwa vile ni Haram ya Imam ar-Ridhaa (a.s.). Watu wengine wanatengeneza orodha ya matatizo yao ya kiafya magonjwa waliiyonayo wao wenyewe, wazazi na ndugu zao; na wanakaa mbele ya kaburi wakichukua jina la kila mwanafamilia na maradhi yake na kumuombea shufaa. Hapana shaka kwamba hii ni familia yenye ukarimu sana na yejote anayekuja na imani thabiti kwao akiomba

chochote wao wanatoa, Alhadulillah. Hii ni sehemu ya ukarimu wao Ahlul-Bayt (a.s.). Lakini Maimam hawa wanahitaji Umma, sio watu wagonjwa wanaotafuta tiba kutoka kwao. Hawatarajii watu wag-onjwa wenye matatizo ya kiafya kuwatemebelea na kusoma *Ziarat al-Jamia al-Kabiir*; wanakutarajieni ninyi mje kwao kama Umma. Viongozi huwa wanahitaji wafuasi. Leo kama unapata fursa ya kumtembelea Kiongozi Mkuu (Rahbar) utafanya nini? Kwa nini utakwenda kwake? Kupiga na kutengeneza picha, na ni ukweli ulio wazi kwamba kila tunapotembelea watu wakubwa, mashuhuri kama hao tunawaomba wasimame karibu nasi ili tupige nao picha. Tutafanya nini na picha hii? Tutawaonyesha watu kwamba sisi tuna uh-siano na Kiongozi huyo. Kwa hiyo hii ndio iliyokuwa sababu yako ya kwenda kwa Kiongozi huyo? Kutengeneza picha kadhaa? Wakati Umma unapomtembelea Imam, unafanya hivyo kwa sababu mbili. Huu ndio mukhtasari wa sehemu ya pili ya manifesto – hati hii ya *Uimamu*:

Moja ni kwamba: “Mimi ni mfuasi wako, ninakutambua wewe, na ninajua kwamba wewe ni nani. Nimekuja mbele yako kuwasilisha taarifa ya shughuli zangu nilizofanya hadi sasa hivi.” Tunamtembelea kiongozi wetu kwa sababu hii ambayo ni kuwasilisha yale yote tuliyoyafanya hadi kufikia wakati huu. Na sababu ya pili ni kupata mpangilio na shughuli za kufanya kuanzia sasa na kuendelea. Haya ndio mambo mawili hasa. Kwa hiyo mtu ni lazima awe na cha kuwasilisha na anapaswa kurejea na ahadi kwamba nitafanya yote haya. Wale wanaotembelea makaburi haya wakiyachukulia kwamba ni Mahospitali, wanaporejea wanawaambia watu kwamba mimi nimetibiwa, na fulani bin fulani ameponyeshwa kutokana na maradhi haya na yale.

Niko mbele ya Imam wangu, kiongozi wangu, mwongozaji wangu ambaye alidhulumiwa na kuonewa katika zama za Bani Abbas.

Nimekuja mbele ya Imam huyo ambaye hakuweza kupata Umma. Nimekuja mbele ya mtu yule ambaye alikuwa na shauku kubwa ya kuwaona watu wakigeukia kwenye Umma wake. Leo nimekuja kwake kama Umma wake. Moyo wa Imam umefurahi kwa mambo haya mawili tu. Imam anafurahi pale anapoziangalia shughuli zako. Sasa, tunatembelea kaburi Tukufu kupata tiba na kurejea. Tumepata na kupokea kitu, lakini je ni zawadi gani ambayo tumempatia Imam (a.s.)? Tunatumbukiza fedha kwenye hifadhi ya hapo kaburini; je, Imam (a.s.) ana mahitaji na fedha hizo? Imam anahitaji shughuli zako. Imam anataka kujua kile ulichofanya katika miaka hii ishirini, thelathini, arobaini au hamsini ya maisha yako. Ni wapi ulikotumia maisha yako haya? Ni katika mwelekeo gani wa kidini ulimokuwa wewe? Na niambie, ni kitu gani utakachokwenda kufanya baada ya kurejea kutoka hapa? Utakwenda kufanya yaleyale uliyokuwa uki-fanya hapo kabla? Hii ndio sababu ya kwamba imesemekana kuwa wewe unapaswa bila shaka kuwatembelea Maimam (a.s.) na ukae hapo na uzungumze nao.

Imam Haadi (a.s.) alitaka kuihifadhi njia ya haki iliyonyooka. Isije ikatokea kwamba kwenye haja, kusihu kwa ajili ya du'a, tiba ya matatizo na mengineyo visababishe ile njia halisi hasa ya dini ipotee. Uimamu haupaswi kupotea ndani ya du'a hizi, wajibu wa Umma usije ukapotea. Hivyo Imam Haadi (a.s.) aliikusanya manifesto hii sahihi na ya kivitendo. Hii sio ya kisomo cha mdomo tu, hivyo unapaswa kuisoma kwa tafsiri ya kivitendo. Kwa kweli, hata kabla ya kutembelea kaburi la Imam yoyote Maasum, unapaswa kujizoesha mwenyewe na manifesto hii. Na baada ya kuisoma ni lazima ujiulize na kujua: kwa nini mimi nimekuja hapa na nimekuja kusema nini? Nimekuja kutafuta nini?

Sehemu ya pili ni kwa ajili ya ahadi ambayo inahusisha madhumi ya ukusanyaji wa Imam (a.s.) wa manifesto hii ambayo yaliku-

wa ni ule mwanya au kile kiungo cha Umma kilichokosekana. Imam alikuwepo lakini alikuwa hana Umma, na hii ndio sababu kwamba Bani Umayyah na Bani Abbas walikuwa madarakani; kwa sababu Uimamu na Mfumo wa *Wilaya* havikuweza kutekelezwa.

Wote tunajua kwamba Bani Abbas waliwashinda Bani Umayyah kwa kutumia jina la Ahlul-Bayt (a.s.) na wakapata utawala. Lakini walipoingia madarakani hawakutekeleza Uimamu, waliimarisha ufalme na ukatili uleule, utawala wa kionevu na kidhalimu wa mtindo wa Bani Umayyah. Kwa hiyo, wakati Mamuun alipoutoa Ukhalfifa kumpa Imam ar-Ridha (a.s.), kwa nini Imam Ridha (a.s.) alikataa kuukubali? Hii ni kwa sababu Uimamu haupitii kwenye mlango huu (wa madhalimu). Kama ukipitia kwenye mlango huu basi mimi nitakuwa mrithi wa wakandamizaji. Uimam ni haki yetu, lakini haki hii ipatikane kutoka wapi? Haki hii ni lazima itolewe na Umma. Huo Umma ni lazima usimame; uanzishe uasi wa mageuzi ili tuweze kuitata haki hii ya uongozi. Haki hii ilihuishwa na kutolewa katika ardhii ya Jamhuri ya Kiislam ya Iran. Imam Khomein (a.s.) alifanya tafsiri halisi ya *Ziarat al-Jamia al-Kabiir* kwa ajili ya Umma huu; sehemu zote, ya kwanza na ya pili. Imam Khomein (a.s.) alionesha kwamba Imam Haadi (a.s.) ni mwongozaji wa kweli kweli na wala sio mwongozaji kwa ajili ya zama zake tu bali ni kiongozi wa vizazi vyote hadi Siku ya Kiyama. Ameonyesha njia, mwelekeo na ubainifu wa dini.

Lakini Imam (a.s.) alipata shida nyingi sana na majanga kwa ajili ya njia ya haki. Kila kundi na hususan la Naasibi walifanya ukatili mkali sana juu ya Imam Haadi (a.s.), Bani Abbas walimkandamiza. Bani Abbas walimtilia sumu, na uhasama wa Naasibi dhidi ya Imam Haadi (a.s.) haukuisha siku hiyo. Kaburi lililodhuluiwa la Samarra ni ushahidi unaozungumza wa ukatili huu.

Kwa nini kaburi hili lilipigwa mabomu na kugeuzwa kuwa

magofu? Kama Umma kwa ajili ya Imam ungekuwepo pale basi usingeruhusu majengo ya kaburi hili kuanguka. Wajibu wa Umma sio kukusanya fedha kwa ajili ya kujenga upya hilo kaburi lililoharibiwa bali badala yake wajibu wao ni kulinda Haram hiyo ya Imam. Umma unakuwa ni Umma tu pale unapokuwa na ulinzi uliojizatiti na utetezi wa Uimamu na haram zake, sio kulalamika tu baada ya kuwa jengo lake limeanguka chini. Kwa nini haram hii ilibomolewa? Umma ulikuwa wapi? Nchi ambamo mna mamilioni ya Shi'ah mtu anaweza kwenda kwa urahisi kabisa na kuligeuza kaburi na lile Haram la Imam Haadi (a.s.) kuwa gofu. Haya ni mashambulizi kwenye Uimamu na *Wilaya*, na Umma unawajibika juu ya hili. Tusiwalamu tu hao Naasibi na kuosha mikono yetu kwenye jinai hii.

Hao Naasibi ni maadui, Wamarekani ni maadui na Uimamu hauwezi kulindwa chini ya kivuli cha maadui. Uimamu unaweza kuwa salama tu pale Umma utakapoliwa upo pamoja nao. Kama Umma ungekuwepo ukatili mbaya kama huo usingetokea pale Karbala. Bibi Zainab (s.a.) alisema maneno yayo hayo katika hotuba yake mjini Kufah kwamba kuomboleza kwenu sasa hakuna faida yoyote; kama mngekuja Karbala tusingeomboleza sisi wala ninyi pia. Mlikuwa wapi wakati ule? Wapi mlikuwa wakati kaka yangu alipouawa Shahidi? Wakati Shimr alipopanda juu ya kifua kitukufu cha ndugu yangu ninyi mlikuwa wapi? Mlikuwa wapi wakati tulipovuliwa hijab? Mlikuwa wapi wakati vitoto vichanga vilipokuwa vinaomba maji? Ninyi mlikuwa wapi wakati wanawake walipokuwa wakisihii kuomba msaada na mahema yalipochomwa moto? Mlikuwa wapi wakati farasi wa ndugu yangu alipokuwa anapiga makelele, enyi watu! dhulma imekwisha fanyika!? Mambo yote haya yanauhitajia Umma. Haram iliyobomolewa ya Samarra inauita Umma. Mlikuwa wapi wakati Maimam (a.s.) walipokuwa wanauawa kwa kupewa sumu? Kwa mujibu wa baadhi ya watu wazima ni kwamba, uchungu

wa kuuliwa kishahidi kwa sumu ni mkali sana kuliko kuuawa kwa upanga. Sumu huwa inakatakata ini vipande vipande. Wakati baba yake Imam Haadi (a.s.) alipopewa sumu, ini lake lilikuwa likichanika chanika na hapakuwa na mtu wa kumpelekea maji vile vile. Na kisha hata Imam Hasan pia aliuawa kwa sumu na mke wake mwe-nyewe.

Ukatili wote huu, machungu yote haya, vifo vyta kishahidi hivi na sasa huku kuuliwa kishahidi kwa minara na kuba za Haram, kunaита mataifa yenye kuheshimika na kuyataka yawe Umma ili ukatili wote huu upate kufikia mwisho wake. Hili linaweza kutokea tu kama kwanza tutatambua na kukubali kwamba Uimamu sio ni itikadi tu; bali ni Mfumo wa *Wilaya*, mfumo wa kisiasa wa Kiislam wa utawala; mfumo wa uongozi na Umma.

---

## MASWALI NA MAJIBU

---

**S**wali la kwanza: *Ni vipi tutakavyoanza mchakato wa utekelezaji wa Mfumo wa Wilaya katika jamii yetu?*

**Majibu:** Kwanza kabisa inatubidi tujielewe sisi wenyewe. Wakati mwininge hutokea tukasimama dhidi ya mfumo fulani, lakini hatuna utambuzi wowote wa mfumo ambaa utachukua nafasi yake huo. Nitaielezea hali hii katika namna ya mzaha au kichekesho.

Wakati mmoja kulikuwa na Mwislam mmoja na kafiri. Wali-kuwa wote wakibishana kuhusu dini. Yule Mwislam kwa namna fulani aliweza kumlazimisha yule kafiri kutambua kwamba imani yake ni potofu na anapaswa kuibadilisha. Yule kafiri akakubali na akamuomba yule Mwislam amfundishe Kalimah (kushahidia juu ya imani) ili kwamba aweze kusilimu. Yule Mwislam akajishi aibu na akajilaani mwenyewe na akajisemea mwenyewe: “Natamani ningejjua hiyo Kalimah mimi mwenyewe, angalau ningeweza kufanikiwa kumbadilisha kafiri mmoja kuwa Mwislam.”

Tusije tukaishia kwenye hali kama hiyo kwamba tunaanza kusi-mama dhidi ya udikteta na demokrasia, na kuelezea kwamba mi-fumo hii sio ya kidini na kuwa ni masanamu ya Saamiri, lakini papo hapo atakapotuuliza mtu kuhusu mfumo mbadala, tukajihisi kusiki-tika kwamba hatujui lolote kuhusu mfumo wa Uimamu. Kwanza ujaribu kujitambua na kujielewa wewe mwenyewe kuhusu mfumo huu. Utaratibu ni kama huu uliofanya kwa kuandaa semina. Uimamu hauna budi uwe ni sehemu ya mukhtasari wa mafunzo yetu kwenye semina hiyo na inatupasa tuwe tunatumia muda kiasi fulani kwa kila siku katika kuuelewa huu mfumo wa Uimamu.

Amua juu ya jambo hili kwamba Uimamu sio ni itikadi tu, bali badala yake ni jina la mfumo wa utawala ambao unahitaji kutekeleza katika jamii. Katika zama za Maimam watukufu (s.a.) wao wali-kuwa wametengwa; baadhi yao walifanywa mateka, wakahamishwa nchini mwao na wakauliwa kishahidi. Je, kulikuwa na sababu gani nyuma ya ukatili wote huu? Sababu ilikuwa ni kwamba, Umma, wale wafuasi wa Maimam hawa (a.s.) hawakuweza kuuelewa mfumo huu, na kwa hiyo Maimam walikuwa katika hali ya muflisi. Kama katika zama zile Umma ungekuwa umeielewa Uimamu basi leo hii dunia yote ingekuwa inatawaliwa na kuongozwa na mfumo wa Uimamu!

Hivyo kwanza ujaribu kuuelewa mfumo huu, na ndipo uanze kuutangaza na kuueneza mionganoni mwa watu. Hatuna budi tusubiri fursa, wasaa na sababu za kufanya tabligh ya ukweli na haki. Ni wajibu juu ya kila mmoja wetu sisi kufanya tabligh na hususan wanawake wa jumuiya yetu. Kwa bahati mbaya jumuiya yetu imeten-geneza mazingira ya namna ambayo kwamba kuna fursa chache sana kwa wanawake kufanya tabligh. Nazungumza kuhusu wanawake wa kidini, sio kuhusu wale wengine ambao tayari wamo kwenye mbio za marathoni (ghururi za dunia). Wanawake wa kidini wasikae wakibweteka huku wakingojea mtu mwingine aje kuwatoa kwenye makucha ya maovu. Ni wajibu wenu kusimama na kuwafanya watu waelewewe huu mfumo wa *Wilaya*. Isije ikageuka kuwa kwamba kila Majlisi au programu za simulizi za visa zinazoandalialiwa na ninyi mkashiriki mkidhani kwamba huo ndio wajibu wenu tu basi. Hamna budi kutambua na kuelewa wajibu wenu hasa na kwa vizuri zaidi vilevile. Inatupasa sisi tuelewe na kisha tuwaeleweshe na wengine kuhusu mfumo huu wa Wilaya. Hamkujua kwamwe chochote kuhusu elimu ya taaluma pale mlipozaliwa, lakini baadae kidogo kidogo mkaanza kuelimika. Kulikuwa na mambo mengi sana ambayo mli-

kuwa hamyajui, lakini baadae mkaja mkayajua. Kadhalika kama hu-  
ijui dini, basi anza sasa kujifunza. Ndipo baada ya hayo tu tutaweza  
kuonyesha tabia na wajibu wa heshima ya hali ya juu kabisa.

**Swali la pili: Ni jinsi gani mwanadamu atakavyoweza kuwa  
mwenza wa siri za Uimamu ili kwamba aweze kuelewa huo mfu-  
mo wa Uimamu?**

**Majibu:** Nimesema mapema kwamba hili linaweza kufanyika kwa utambuzi – maarifa. Kwa kukaa tu mahali pamoja huwezi kuwa mwenza wa hizo siri za Uimamu. Unaweza kuwa na utambuzi wa siri hizo wakati ule tu utakapokuwa karibu na dini, ukajifunza misingi ya nje na ya ndani ya dini, na ndipo tu utakapoweza kugundua siri zilizofichika humo. Unaweza ukatumia sehemu ya kutosha ya mai-sha yako katika hili kuipa dini muda. Ninyi wote mnampenda Imam wenu (a.s.), lakini mapenzi juu yake yanawafanyeni kuwa wapenzi tu bali sio watambuzi wa siri za Uimamu. Ni maarifa ambayo yataku-fanya wewe utambue kuhusu hizo siri za Uimamu. Ni pale tu mapenzi yatakapoandamana na utambuzi ndipo tu utakapoweza kuelewa siri za Uimamu zilizofichika. Ni bahati mbaya sana kwamba tuna mapenzi na dini hasa, lakini utambuzi wetu ni mdogo sana.

**Swali la tatu: Je, sio wajibu wa Ulamaa wetu kushughulikia  
mada kama hizo na kuanzisha kiungo chenye nguvu cha mada  
hii pamoja na sisi, na kama wao hawafanyi hivyo, ni nani basi  
anayepaswa kulifanya hili?**

**Majibu:** Ni dhahiri kabisa kwamba Ulamaa ndio wanapaswa kuan-  
zisha kiungo hiki cha somo hili mionganoni mwa watu. Kuna methali  
ya Kiajemi isemayo: “Kama kitu kikipata kutu, weka chumvi juu

yake na kitakuwa safi. Lakini huzuni ni siku ile chumvi itakapoharibika.” Kama Ummah ukiharibika basi Ulamaa wanapaswa kuusahihisha na kuurekebisha, lakiini kama Ulamaa wenyewe wakiharibika, basi ni nani atakayewarekebisha wao?

### **Swali la nne: Tutawezaje kuubaini mfumo wa Kifirauni katika maisha yetu ya kawaida?**

**Majibu:** Athari za mfumo wa Kifirauni ziko dhahiri kabisa sio tu katika nchi yetu bali kwa kiwango cha kidunia. Ulimwengu wote leo hii unatawaliwa na mfumo huu. Unaona kwamba katika dunia nzima ni nchi moja tu ambayo haiko tayari kuukubali mfumo huu wa Kifirauni na kwa hiyo maadui wa Uislam wameizunguka nchi hiyo kutoka kila upande. Kila siku wanaitishia nchi hiyo. Kwa bati mbaya dunia yote iko chini ya kivuli cha mfumo wa Kifirauni na nchi yetu iko mstari wa mbele katika kuuendeleza huu mfumo wa Kifirauni.

Kama bado hujaridhika na hili, basi hebu zichambue athari za mfumo huu. Katika siku zilizopita yule msoma habari wa kike katika TV alikuwa akivaa skafu kwenye shingo yake. Hii ilianza kuteleza kidogo kidogo, kisha zile mbio za marathoni, usafihhi, kukaa uchi na uharibifu wa maadili. Athari zote hizi zinakuja kwenye maisha yetu na zinaongezeka kila uchao. Unatarajia kufahamu na kubaini nini zaidi, wakati Rais wa nchi anajitokeza na kuwaunga mkono wanawake walioko uchi wakikimbia kwenye mitaa. Yeye alisema kwamba, wale wasiotaka kuyaona haya basi wafumbe macho yao au wazime TV zao. Huu sio Uislam hata kidogo. Tumesahau kwamba nchi hii ni taifa la Kiislam, taifa la heshima na la watu safi na waung-wana. Kuzembea, kutojali kwetu na ukimya vinasaidia kuuendeleza mfumo huu wa Kifirauni!

**Swali la tano:** Umesema kwamba nchi hii ina mfumo wa Kifirauni, hivyo tunapaswa kuondoka nchi hii. Lakini swali langu ni kwamba misingi ya uundaji wa taifa hili ulikuwa madhubuti sana, yule kiongozi aliyelifanya taifa hili alilifanya juu ya kanuni za Kiislam, basi ni kwa nini hali iko kama hivi?

**Majibu:** Mimi sikuwaambieni mwondoke nchini humu. Nchi hii iliumbwaa katika jina la Uislam, lakini kamwe hajakabidhiwa kwenye Uislam na huo Uislam haujatekelezwa kamwe katika nchi hii. Kwa kweli leo hii wanazungumza na kujadili kwamba hatari kubwa kabisa na tishio la taifa hili lililonalo linatoka kwenye Uislam. Kwa hiyo wanataka kupata uhuru kutoka kwa Uislam katika nchi hii. Mimi sisemi kwamba hamna budi kuondoka nchi hii na mwende zenu. Ninachokisema mimi ni kwamba ile misingi ambayo nchi hii ilisimamishiwa juu yake ilikuwa sahihi na tunahitajia kuirudisha kwenye kanuni za misingi hiyo. Hatupaswi kukaa kizembe na bila kujali. Hatuna budi tujitokeze na kutambulisha mfumo wa dini kwa watu, kuifanya dini iwasilishike ili kuwavutia watu kwenye dini. Haiwi kwamba tunaondoka na kwenda zetu, popote tutakapokwenda hali itakuwa mbaya zaidi ya hivi, kwa hiyo inatubidi tubakie hapana kujirudisha sisi wenewe, ardhi hii na jamii hii kuelekea kwenye dini. Kama Imam Husein (a.s.) angetaka kuokoa maisha yake angekwenda mahali pengine popote pale, lakini basi ni nani angeuangamiza u-Yazid. Ili kuubomoa u-Yazid unapaswa lazima kubakia hapo hapo. Ma-kosa mengi yamefanyika katika nchi hii. Swali ulilouliza linahitaji ufanuzi mwangi na inaweza kuwa inahitaji semina ya siku nzima kulielezea kirefu. Wakati nchi hii ilikuwa na waongozaji kama vile Allama Iqbal, sasa ni kwa nini jambo kama hili litokee? Hili linahitajia mjadala mrefu.

## Swali la sita: Kwa nini watu wengine hawaikubali hii *Wilayatul-Faqiih*?

**Majibu:** Kuna sababu nyingi sana nyuma ya hili. Watu wengine ni kutokana na ujinga, wengine kwa shaka za kuundwa, wengine kuto-kana na sababu nyinginezo na wengine wamepotoshwa na maadui. Kwa maneno mengine, baadhi ya watu wanapotoshwa na mawakala wasaliti ambao wamepandikizwa mionganini mwetu ili kuiziba njia hii. Mawakala hawa wanapandikizwa kutokea nyuma na wanapelekwa kwenye mimbari zetu ili kubadili mwelekeo wa jumuiya hii, lengo kuu ni kuukengeusha Umma huu kutoka kwenye mfumo wa maisha wa kimungu.

Ninawasilisha hapa kisa cha kweli kama mfano kwa ajili yako ili upate kuelewa yale yote yaliyofanywa ili kuwapotosha watu kutoka kwenye *Wilayatul-Faqiih*. Ungezunga na habari pia jana kwamba, ili kubadilisha mfumo wa utawala nchini Syria, serikali ya Marekani imetenga bajeti ya dola milioni tano za kimarekani. Na ili kubadili serikali nchini Iran Marekani imetenga dola za kimarekani milioni ishirini na moja kwa kila mwaka. Pesa hizi wanampa nani? Wanazitoa kwa mawakala kama hawa ambao watakuja kuzungumza dhidi ya mfumo huu wa *Wilaya*, kuandika chochote na kuendelea kufanya chochote dhidi ya Mfumo wa *Wilaya*.

Waliunda baraza huko Marekani kwa jina la UMAA chini ya mwongozo wa Paul Wolfowitz. Huyu Paul Wolfowitz alikuwa ndiye mtaalamu wa ushauri wa mashambulizi ya Marekani huko Iraq. Yeye alibuni shambulizi hili na kisha akalipanga yeye. Chini ya uongozi wake waliunda kamati yenye Ulamaa, Makhatibu wa Kidini na wenye kushikilia mimbari. Lengo la baraza hili ni kufanya kazi kuelekea kwenye kuyasafisha mawazo ya Imam Khomein (r.a.) ku-

toka kwenye madhehebu ya Shi'ah. Wao walisema kwamba mambo fulani ndani ya madhehebu ya Shi'ah yameingia kutoka nje na haya ni lazima yaondolewe.

Paul Wolfowitz wakati akiwa Mkuu wa Benki ya Dunia alijitokeza kwenye TV akiwa na sura zinazojulikana sana za watu wa jumuiya ya Shi'ah wakiwa wamekaa pamoja naye. Alisema kwamba mawazo ya Imam Khomeini (r.a.) yanapaswa kuondolewa kutoka kwenye jumuiya ya Shi'ah. Wametenga mamilioni ya dola kwa ajili ya shughuli hii. Kwa hiyo sio kwamba kama mtu akikaa kwenye mimbari na kuzungumza dhidi ya *Wilaya*, basi huo ni uharibifu wa mawazo na akili yake mwenyewe, laahaha. Ukifuatilia mahusiano ya mtu kama huyo yatarudi nyuma mbali kabisa, baadhi ya ofisi za Kibalozi, au NGO fulani zitakuwa nyuma yake huyo. Hivyo inatubidi tuwe na tahadhari na uwerevu.

**Swali la saba: Umesema kwamba kama tukipiga kura zetu ni kama kumsaidia Saamiri. Katika nchi yetu hakuna serikali ya chama ambacho ni sahihi na kizuri, basi ni nani tutakayempa kura zetu sasa?**

**Majibu:** Wajibu wetu sio kupiga kura tu; wajibu wetu ni kuandaa mazingira kwa ajili ya mfumo sahihi. Kama nilivyosema kabla kwamba kwanza tambueni zile kanuni za msingi ambazo juu yake ndimo ilimoundiwa nchi hii na kisha jaribuni kulirudisha taifa kueleke kwenye kanuni hizo. Wajibu wetu sio kupiga kura, bali hasa wajibu wetu ni kutekeleza mfumo wa *Wilaya*. Kama mnadhani kuwa kuna mtu fulani, ingawa yumo kwenye huo mfumo dhalimu, lakini bado anaitumikia dini, basi mnaweza kupiga kura zenu kumpa yeye. Wale ambao wamekaa sasa hivi hawastahiki kura zetu.

**Swali la nane: Je, sio lazima kwamba ni muhimu tabia za wanawake zipaswe kuelezwu kwa wanaume pia, kwa vile mwanimke katika dini yetu hawezi kufanya chochote bila ya ruhusa kutoka kwa mumewe?**

**Majibu:** Hiki ulichokisema ni sahihi kabisa. Hii ni sawasawa na uleaji wa mtoto ambapo ni muhimu kwamba wazazi wanafanywa kuutambua. Hata kama tukichukua watoto wa mtu, tukawalea halafu baadaye tukawarudisha kwake, haitakuwa na athari yoyote. Ni muhimu kwamba wazazi wabakie na watoto wao. Kwa hiyo ni muhimu kwa wanawake kwamba walezi wao, iwe ni mume au baba, ni lazima wafanywe watambue tabia zao. Ni jambo lillelo dhahiri kwamba mpaka watakapotambua majukumu ya wanawake, ndipo wanawake watakapokuwa na uwezo wa kutimiza majumu yao ipasavyo hasa. Utamaduni wetu unashangaza. Kwa hali halisi sisi hatuishi maisha ya kidini, bali tunaishi maisha ya kimila na utamaduni. Tunaoa ili kwamba huyo mke awatumikie wazazi wetu, hivi ndivyo ulivytengenezwa utamaduni wetu. Kama huyo mkamwana akiishia kusema kwamba hao wakwe zake wajishughulikie wenyewe, basi hata huyo mumewe atamlazimisha awahudumie wazazi wake. Ni wajibu wa kijana wa kiume kuwashudumia wazazi wake, sio huyo mkamwana. Kama suala la kimaadili tu, anapaswa kuwashudumia wazazi wa mume wake, anapaswa kuwachukulia kama wazazi wake mwenyewe tu, awaheshimu na awatimizie mahitaji yao ya halali. Lakini kuna tofauti kati ya mtumishi na mkamwana, hivyo usijaribu kuo na kufanya kana kwamba umeleta mtumishi ndani ya nyumba yako. Ni mila na desturi zetu kwamba tunapotafuta msichana wa kuo, kigezo chetu sisi ni kuona iwapo kama atawahudumia wazazi wetu au hapana. Huyu ni mke wako, mkamwana wa wazazi wako na yeye anazo haki zake pia. Sasa mlolongo huu unaendelea, mkamwana

huyu huyu anakuwa mtu mzima na anakuwa mama mkwe, na hapo sasa anachukua hatua za kulipiza kisasi chake juu ya mkam-wana wake.

Hiki ndicho kilichofanywa na utamaduni wetu, wamewatoa wanawake kutoka kwenye majukumu yao halisi na kuwahusisha kwenye mambo kama hayo. Ni wajibu wa wanawake kuwalea watoto wao na kushughulikia elimu yao, na malezi ya kitabia ya kizazi kipywa. Kwa kweli sehemu ya elimu inapaswa kuwa kwa wanawake kwa sababu wao wanaweza kutekeleza vizuri zaidi jukumu hili. Lakinii tumewapa fagio, vyombo vichafu vya jikoni na vyakula vya kupika. Sasa imetokea hivyo kwamba hata wanawake wenyewe pia wanazipenda sana kazi hizi kuliko kitu kingine chochote tena. Hawako tayari kujitokeza na kuongoza mipango ya elimu kwa ajili ya watoto. Wao wamekuwa wataalamu wa shughuli za nyumbani. Lakinii ni muhimu vilevile kufanya hiso kazi za nyumbani. Sio iwe kwa sababu nimesema hivyo basi mziache kazi za nyumbani. Cha muhimu kuelewa hapa ni kwamba mnapaswa kugawana majukumu ya nyumbani kati yako na mume wako. Isije kutokea kwamba tunazichukulia hiso kazi za nyumbani kama kisingizio cha kukwepa wajibu wa kijamii, hilo halitakubalika.

**Swali la tisa: Ni vipi mtu atawea kuleta mageuzi kwenye nyumba yake mwenyewe kabla ya kuleta mapinduzi kwenye serikali ili kwamba tofauti kati ya halali na haramu iwe dhahiri?**

**Majibu:** Ulichokisema ni kweli kabisa, serikali ni mfumo mkubwa zaidi na nyumba ni mfumo mdogo zaidi. Kama mtu hawezu kurekebisha mfumo mdogo hawezu akarekebisha mfumo mkubwa. Hata kabla ya hili ni nafsi yako mwenyewe. Wale ambao hawawezu kutekeleza Uislam katika nafsi zao wenyewe ni vipi wataweza ku-

utekeleza Uislam katika jamii. Katika muktadha huu nitakuelezeni tukio la wakati Jenerali Zia ul-Haqq alivyokuja kukutana na Imam Khomein (r.a.). Katika siku zile za vita kati ya Iran na Iraq, iliundwa kamati ya Kiislam ya kusimamisha vita. Jeneral Zia ul-Haqq alikuwa na shauku kubwa ya kuwa kiongozi wa ulimwengu wa Kiislam; hivyo alikwenda kwa Imam Khomein (r.a.). Akatambulishwa kwake kama mtu anayejitahidi kutekeleza mfumo wa Kiislam katika nchi yake Pakistan. Imam (r.a.) akamwangalia usoni mwake na akasema kwamba, mtu ambaye hawezi kuutekeleza Uislam usoni mwake ni vipi atawezekutegemewa kuutekeleza katika nchi yake? Sisi nasi tuko vivyo hivyo; kwanza inatubidi tutekeleze Uislam katika maisha yetu, katika nyumba zetu na kisha taratibu tusonge mbele kuelekea kwenye kuutekeleza kwenye jamii. Kwa hiyo, kama tutaondoka nyumbani kwetu na kuanza kulingania nje na kutarajia mabadiliko katika jamii, basi kwa hali kama hiyo hayawezi kupatikana mabadiliko yoyote aslani.

**Swali la kumi:** Huu mfumo wa sasa hivi ndani ya nchi hii unawapeleka watu kuelekea wapi?

**Majibu:** Nimelisema hili hapo kabla na limedhihirishwa wazi kabisa katika maneno ya Qur’ani “**Wanakuteseni adhabu mbaya**”. Ni kuupeleka Umma kuelekea Jahannam. Mfumo huu uliopo sasa umeegemea kwenye hali ya kiulimwengu, dunia iliyojitenga na dini (secularism), mawazo ya kisasa ya kielimu, Uislam poa usiojifunga kimtazamo, ambamo wanawake wanaruhusiwa kutoka nje mitaani kwa namna wanayotaka, na hapo kwa makusudi mmomonyoko wa maadili unaenezwa. Kama ukiwachukulia wanaume, kwa kuchukulia Msimu wa Majira ya Kuchipua (spring) kama kisingizio, wanajingiza katika kuimba, kucheza muziki, ulevi na ufahari mkubwa. Matendo yote haya yanaanzishwa moja baada ya jingine kwa maku-

sudi kabisa ili kuharibu mazingira ya kijamii na kuvunja maadili. Unapaswa kutokuwa na shaka kuhusu hili kwamba wale wanaotawala mfumo huu wana dhamiri za wazi kabisa za kuliondoa taifa hili kutoka kwenye dini na kuanzisha kutopenda na chuki kwenye maadili ya Kiislam ndani ya jamii.

**Swali la Kumi na Moja: Kama tuko chini ya kumfuata Marjaa fulani katika fatwa, basi ni kwa namna ipi amri za Faqih zinavyoteklezwa juu yetu?**

**Majibu:** Swalii hili pia linaweza kusemwa hivi, iwapo tunaruhusiwa kumfuata Marjaa mwingine katika fatwa mbali na Wilii al-Faqih, au wakati Wilii al-Faqih yupo tunaweza kufuata fatwa za Marjaa mwingine. Hebu ngoja nijaribu kutatua suala hili katika misingi yake.

Mfumo halisi ambao Allah Aza wa Jallah ameuanzisha ni Mfumo wa *Wilaya*. Bila kujali zama ya Utume, Uimamu (Uimamu) au kipindi cha ghaibu, katika kila zama kuna mfumo mmoja tu wa utawala uliotengenezwa na Allah Aza wa Jallah na huo ni Mfumo wa *Wilaya*. Mfumo wa Kidini kamwe hauwezi kuwekwa kando katika zama yoyote imma kwa sababu ya kifo cha Mtukufu Mtume (saww) au ghaibu ya Imamu wa mwisho (a.t.f.s). Haiwezekani kuweka Mfumo wa Dini kando na mipaka iliyowekwa na Allah Aza wa Jallah. Mfumo huu wa *Wilaya* ni mfumo ule safi ambao kwamba kwawo watu lazima wauendee, waufuate na kuishi maisha yao chini yake. Wakati ambapo kwa upande mwingine hali ambayo tunakabiliana nayo leo ni ile ambayo badala ya kuukubali mfumo huu, kuishi maisha yetu chini yake na kuutekeleza, tunakuwa tayari kukubali na kujizoeza kwenye mfumo mwingine wowote unaowekwa juu yetu. Kwa kweli tunajaribu vilevile kuifanya dini ni yenye kunyambulika

na kurekebishiha kwa kiasi kwamba tunahalalisha mifumo hii ili-yowekwa juu yetu kuwa ya Kiislamu. Juhudi ambayo tunafanya ili kujizoeza na kujioanisha wenyewe na mifumo iliyopo, ni nusu tu ya juhudhi kama hizo huhitajika kutekeleza mfumo wa kweli wa Mungu.

Kwa mfano katika Iraq leo idadi ya watu wanaopoteza mai-sha na mauaji ya kikatili yanayotokea yote hayo ni kwa ajili ya kurekebishiha na kuafikiana na mfumo uliopo. Hata nusu ya watu hawa wengi waliopoteza maisha yao isingefika kama wangeamua kuvunjilia mbali mfumo uliopo na kugeuka kuelekeea kwenye kutekeleza mfumo halisi wa utawala. Imamu Khomein (ra) alikuwa na mwelekeo huo huo, wakati Shah alipowasilisha njia mbalimbali za maafikiano kwa Imamu (ra) na akamwambia aseme analotaka na kwamba Shah alikuwa yuko tayari kutekeleza matakwa yake na kufanya marekebisho fulani na maafikiano katika mfumo uliokuwepo. Imamu (ra) alisema kitu kimoja tu, kwamba madai yangu na madai pekee ninayotaka ni kwamba lazima uondoke na kuicha nchi hii. Kama wakati ule Imamu (ra) angeafikiana na Shah, leo hali ya Iran ingekuwa mbaya kuliko ile ya Iraq. Mfumo uliopo kwa kiasi chochote unavyofanya kazi haufai kuwa na mwafaka au marekebisho. Tunajaribu kuleta unyambulisho katika dini ili kwamba ikubaline na mifumo iliyopo. Mfumo halisi ni Mfumo wa *Wilaya* na Uimamu.

Kama mfumo huu unakuwa haupo basi pia kwa hali yoyote lazima tujizoeze wenyewe na mfumo mwingine wowote wa utawala. Hata kama ukiangalia kwenye sheria za Fiqh za Mujtahid wote vilevile wanaelekeza kwenye Mfumo wa *Wilaya*. Hakuna ubishani kabisa, hivi ni vita tu vya kisaikolojia ambavyo hatupaswi kuvishindwa, kama mtu yejote anakuja na kusema kwamba utawala wa Kiislamu, *Wilayatul-Faqih* ni saula la kiubishani, hakika msiache tu na kuweka silaha zenu chini, mwanadamu lazima awe imara na

thabiti angalau kwa kiasi ambacho anaweza kupima na kuthibitisha mabishano hayo.

Kwa uwazi tunaweza kuona kwamba kuna hukumu mbalimbali zinazohusiana na Mtawala wa Kisharia. Sheria zinazozungumza kuhusu jukumu la Serikali ya Kiislamu katika masuala mengi, na katika sura za ibada za utakaso, Swala, Saumu, Hijja, na Zaka, na katika kila sura kwenye sehemu, nyingi sheria hizi hutegemea juu ya Mtawala wa Kisharia. Sasa kama tukiwa katika eneo au nchi, ambako hakuna Hakim, yaani hakuna serikali ya Kiislamu inayotekelizwa huko na hakuna *Wilayatul-Faqih*, ingawa inaweza kuwa jamii ya Kiislamu, basi chini ya mazingira hayo mfumo mbadala ni ule wa Marjaa. Hivyo katika zama na nyakati hizo wakati kulikuwa hakuna mfumo wa *Wilaya* unaotekelizwa popote, huko mfumo huu wa Marjaa uliwasilishwa wakati ambapo tuliruhusiwa kufuata wanachuoni wale ambao wanakidhi masharti fulani ya dini ya kuweza kuridhiwa kufuatwa.

Lakini wakati mfumo halisi wa *Wilaya* upo, basi mfumo huu mbadala hautekelezeki kwa akili ya moja kwa moja. Ni kama vile wakati Imamu Maasum (as) akiwepo basi mfumo wa *Wilayatul-Faqih* unakuwa haupo. *Wilayatul-Faqih* ni mfumo mbadala wakati wa pindi cha ghaibu, mpaka kujitokeza tena kwa Maasum (a.t.f.s.). Kila mtu pamoja na Faqih, Marjaa, wanachuoni na wanadamu wa kawaida watamfuata yeye (a.t.f.s.) tu. Lakini wakati Maasum (a.t.f.s.) akiwa hayupo, basi wakati wa kipindi hiki cha ghaibu *Wilaya* ni ya Faqih, hiyo pia ni katika mipaka mahususi iliyohanishwa. Wakati *Wilaya* ya Faqih inapokuwepo, kila mtu lazima amkubali na kumfuata yeye hususan katika masuala ya kijamii. Lakini katika masuala ya kibinafsi ya ibada inaruhusiwa na Imamu Khomein (ra) na Kiongozi Mkuu mwenyewe kwamba unaruhusiwa kumfuata Mujtahid yeyote mwingine ambaye ana ujuzi mkubwa wa sheria za dini. Kwa

uwazi imeainishwa kwamba kufuata ni lazima iwe ni kwa Mujtahid ambaye ana ujuzi mkubwa wa vipengele vyote vya sheria za dini na sio Mujtahid yule ambaye ana kundi lenye nguvu lenye kutangaza jina lake. Hili ndilo hutokea leo, kuna baadhi ya Mujtahid halisi wazuri, lakini hakuna anayewafuata katika fatwa zao kwa sababu hawatangazwi. Marjaa hatakiwi kujitambulisha yeze mwenyewe kwa watu; ni watu wenyewe ndio watamtafuta Marjaa na kumfuata. Wafuasi lazima wamtafute Marjaa na sio Marjaa huyo (au watu wa karibu yake) kwenda kwa wafuasi kwenda kumtangaza Marjaa huyu kwa ajili ya kuwashawishi wamfuate.

Hivyo katika masuala yako ya binafsi na ibada unaweza kufuata fatwa za Marjaa yejote, lakini katika mambo ya kijamii na kisiasa, katika mambo yale ambayo yanahusiana na watu katika maana pana, itakupasa kufuata *Wilayatul-Faqih*. Katika mas’ala haya hata Marjaa analazimika kumfuata Walii al-Faqiih. Hivyo katika hili, kama Walii al-Faqiih akitoa amri ambayo sio fatwa yake kama Marjaa, ni lazima kwa mtu kutii amri hiyo. Kwa mfano, kama Walii al-Faqiih akitangaza Jihadi inakuwa ni wajibu juu ya kila mtu, hata kwa Marjaa. Na hili linakubaliwa na wanachuoni wote na Mafaqih, na katika utaratibu pia wanachuoni na Mafaqih wanatoa maoni yao katika mambo ya kibinafsi lakini katika mas’ala ya kijamii wanatutaka tumrejee Walii al-Faqiih. Huu ni mfumo kamili ambamo hata Marjaa anakuja chini ya Walii al-Faqiih. Hata katika uhai wa Imam Khomeini (r.a.) kulikuwa na wengi wa wafuasi wake ambao wali-kuwa wakimfuata yeze kama Marjaa na pia wengine wakiwafuata Marjaa wengine, lakini hii ilikuwa ni kwa sababu Imam Khomeini (r.a.) alikuwa ametoa ruhusa ya kumfuata yoyote kama Marjaa katika mas’ala ya Fiqhi.

---

## **ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION**

---

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuuy ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swalaa
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia

18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeesi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
- 39 Upendo katika Ukristo na Uislamu

40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipyta
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza

62. Nahju'l-Balaghah - Juzuuy ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )

83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma sura zenyе Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii

105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Maarifa ya Kiislamu
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Johari zenyе hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vyatya kweli sehemu ya Kwanza

127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)  
(Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)  
(Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)

148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
- 153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Mshumaa.
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka

170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Jihadi ya Imam Hussein ('as)
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)

192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Mwonekano wa Upotoshaji katika Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina ('as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwanendo wa Imam 'Ali ('a)
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu na vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Mwanachuoni wa Kishia (*Al-Muraja 'aat*)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Upotoshaji dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) –  
Sehemu ya Kwanza

213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Kuvunja Hoja Iliyotumika Kutetea Uimamu wa Abu Bakr
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Maeneo ya Umma na Mali Zake
220. Nahjul-Balagha – Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala,  
Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Hu-  
sein (as) hapo Karbala
222. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
223. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebishi na Mageuzi

---

## **KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA**

---

1. Amateka Na Aba' Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi